**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera |
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa |

| | | |
|---|---|---|
| | | na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni |
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil | - | Uteuzi wa Rais |
| 33. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 34. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 36. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 39. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Jimbo la Wawi |

42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

| | | |
|---|---|---|
| 83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Nafasi za Wanawake |
| 84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 85. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| Ndugu Raya Issa Msellem | - | Katibu wa Baraza la Wawakilishi |

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 21 Februari, 2018**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, katika Kikao cha Baraza cha tarehe 12 Februari, 2018, Mhe. Mohamed Said Mohamed alitoa hoja ya dharura kuhusu suala la Kuadimika kwa Mafuta Zanzibar na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira aliahidi kulifuatilia suala hilo na kulitolea ufafanuzi. Kwa mnasaba huo sasa tunamuomba Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji,

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira**: Ahsante Mhe. Naibu Spika**,** kwa ruhusa yako naomba kutoa taarifa ya Hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae. Naomba kuwajulisha Wajumbe wa Baraza lako Tukufu hali halisi juu ya kupungukiwa na mafuta ya petroli. Kwa ujumla mafuta ya petroli yalikuwepo katika vituo vya *GAPCO* na *ZP* ila upungufu ulikuwa kwa kampuni ya *United Petroleum (UP).* Sababu iliyopelekea hali hiyo ni kuchelewa kupakia mafuta kwa meli ya *United Spirit 1* ya kampuni hiyo katika Bandari ya Dar es Salaam kulikotokana na mabadiliko ya mfumo wa kupokea na upakiaji mafuta katika bandari hiyo ambao umesababisha kuongezeka kwa foleni na usumbufu wakati wa upatikanaji na ushushaji wa mafuta.

Mhe. Naibu Spika**,** hali hiyo pia ilipelekea wenye vituo vya mafuta vya *GAPCO* na *ZP* ambao walikuwa na mafuta kuzuia kuuza mafuta na kutengeneza ukosefu kwa kuwatia hofu wananchi ili waweze kuuza kwa njia na bei za ulanguzi. Kutokana na hali hiyo wizara yangu kupitia

mamlaka ya *ZURA* inaendelea kufanya juhudi za kukabiliana na changamoto hizo na kuhakikisha kuwa *UP* inapata nafasi ya kupakia mzigo katika Bandari ya Dar es Salaam na leo hii inatarajia kushusha mafuta katika bohari ya Mtoni. *ZURA* pia ilifanya ufuatiliaji vituoni kwa kuhakikisha kuwa mafuta yanauzwa ili kuwaondoshea wananchi usumbufu.

Katika ufuatiliaji huo, jumla ya vituo 15 vilitozwa faini kwa makosa ya kuzuia mafuta na kukiuka taratibu zilizowekwa na mamlaka.

Hali ya mafuta iliyopo nchini kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

**Kampuni ya *GAPCO***

- *Petrol*: lita 502,723
- *Diesel*: lita 476,766
- *Kerosene*: lita 309,048

**Kampuni ya *ZANZIBAR PETROLEUM (ZP)***

- *Petrol*: lita 564,793
- *Diesel*: lita 243,570

**Kampuni ya *UNITED PETROLEUM***

- *Petrol*: lita 96,072
- *Diesel*: lita 1,050,246
- *Kerosene*: lita 556,116

Kwa ujumla mafuta haya yanatosheleza kwa matumizi ya Zanzibar kwa kipindi hichi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano naomba kuweka Hati Mezani Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 32

### Mkopo wa Fedha kwa Ujenzi wa *Terminal Airport*

**Mhe. Simai Mohammed Said** - Aliuliza:

Ni kiasi gani cha fedha SMZ imekopa *Chinese Exim Bank* kwa ujenzi wa *Terminal* na *Airport* ya Zanzibar na ni lini serikali itaanza kulipa huo mkopo na kwa utaratibu upi na kwa kiasi gani kwa mwaka.

**Mhe. Waziri wa Fedha** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake Nam. 32
kama ifuatavyo:-

i. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeingia mkataba wa mkopo kutoka benki ya *China Exim Bank* wenye jumla ya Dola za Kimarekani 70.4 milioni sawa na Yuan 465,028,248.96 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria *(Terminal II).* Utekelezaji wa mkopo wa awali ulianza rasmi Julai 1, 2010.

   Aidha, kutokana na changamoto zilizobainika wakati wa utekelezaji wa mradi zilizopelekea mabadiliko makubwa ya usanifu wa jengo na eneo lake, serikali inategemea kuongezewa mkopo huo wenye thamani ya Dola za Kimarekani 58 milioni, na

kufanya jumla ya mkopo huo sasa kuwa Dola za Kimarekani 128 milioni.

ii Malipo ya mkopo huo yameanza rasmi kuanzia Novemba 21, 2017 baada ya kumalizika kwa *Grace Period*.

iii. Serikali inatakiwa kulipa kila baada ya kipindi cha miezi sita kwa miaka ishirini na tano (25) hadi Julai 01, 2035.

iv. Utaratibu wa malipo hayo ni kama ilivyo kwa utaratibu kwa kawaida, mkopo huu unalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

v. Jumla ya Yuan 25,834,902.72 zinahitajika kulipwa kila baada ya mwaka, ambapo kwa kila
kipindi cha miezi sita serikali hutakiwa kulipa kiasi cha Yuan 12,917,451.36.

**Mhe. Simai Mohammed Said**: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na swali la nyongeza lakini kidogo labda tungepata ufafanuzi. Swali langu Mhe. Waziri anaposema katika majibu yake kwamba utaratibu wa malipo hayo ni kama ilivyo katika utaratibu wa kawaida na mkopo huu unalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

a) Je, ina maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitashiriki kulipa mkopo huu na kwamba
utakuwa unalipwa moja kwa moja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Kwa kuwa *airport* yetu inapokea kodi tofauti zilizopo kwa mfano *airport tax* ambayo ni Dola 40 pamoja ile *safety fee* ambayo ni shilingi 8,000. Sasa je, serikali haiangalii ikafanya mkakati maalum ikiwa SMZ ndio itakuwa inasimamia kwa kushirikiana na SMT kulipa mkopo huu wakafanya utaratibu wa *retainship*

kwa upande wa *Zanzibar Airports Authority*, ili wao wasimamie mkopo huu kwa sababu mara nyengine fedha zinazoingia serikalini zinakwenda katika mahitaji ya wananchi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Fedha**: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza mikopo ya nje yote ni jukumu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba. *External Borrowing* ni jukumu la *United Republic of Tanzania.* Kwa hivyo, wao ndio wanaowajibika kulipa mkopo na hadi sasa sisi hatujalipa mkopo huu, lakini mkopo huu unalipwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa yapo mambo ambayo hivi sasa yanafanyika kupitia ile *Joint Finance Commission* ambayo itaweka utaratibu wa kuchangia masuala ya Muungano, lakini vile vile kulipia gharama. Sasa hadi hapo utaratibu huo utakapokamilika ndio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakapojua *share* yake katika ulipaji wa mkopo huu.

**Mhe. Hamza Hassan Juma**: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Waziri wa Fedha kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyojibu katika jibu la msingi kuhusu swali la mkopo wa *Exim Bank* wa Uwanja wa Ndege wa *Terminal II* kwamba kiutaratibu unalipwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na kama alivyoeleza vile vile Mhe. Waziri kwamba suala la mkopo huu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hailipi kutokana na makubaliano kama Katiba inavyosema ya Jamhuri ya Muungano, kwamba kutaundwa *Joint Finance Commission* ambayo itakuwa inazingatia mapato na matumizi, lakini vile vile mgawanyo wa mapato wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, hatuoni kwamba kwa kuwa hizo taratibu za hicho kipengele cha Katiba mpaka leo hakijafuatwa. Kwa kuangalia mapato ya Muungano na mgawanyo wa mapato ya Muungano hatuoni kwamba miradi mingi mkubwa ya Zanzibar inachelewa kusainiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu wanahisi kwamba labda tunawabebesha mzigo.

**Mhe. Waziri wa Fedha**: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hamza Hassan Juma kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu mama kwamba maswali ya mikopo ya nje ni jukumu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ki-Katiba na hakujatokea kwa fahamu yangu mimi kwamba miradi hii inacheleweshwa kwa sababu ya mzigo mkubwa ambao unaibeba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kulipa mikopo hiyo. Mfano mzuri ni kwamba ujenzi wa *Terminal II Building* bado serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua dhamana hiyo na hata katika fedha za ziada ambazo ni Dola Milioni 58 hivi karibuni tu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekubali kuchukua dhamana hiyo. Sasa hiyo sio sababu ya msingi ya kwamba wao au miradi ya Zanzibar inachelewa kwa sababu ya mzigo mkubwa deni ambalo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalibeba.

**Mhe. Omar Seif Abeid**: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tumeona ujenzi wa *Terminal II* unaendelea lakini mimi nilitaka nijue ni kiasi gani cha gharama zimeongezeka katika ujenzi huo na ni kazi gani ambazo zimeongezeka kwenye mradi huo wa ujenzi wa *Terminal II.*

**Mhe. Waziri wa Fedha**: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba gharama za awali za mradi huu zilikuwa Dola za Kimarekani milioni 70.4 lakini zimeongezeka sasa kwa Dola za Kimarekani milioni 58. Ongezeko

hilo limetokana na kwanza kuongezeka kwa *scope ya* mradi wenyewe kwamba ile *Terminal Building* imebidi iongezwe na imeongezeka takriban kwa *square meter 2,200*. Pale mwanzo jengo lilikuwa na uwezo wa kuchukua abiria milioni 1.1 kwa mwaka, lakini baada ya kuongezeka sasa lina uwezo wa kuchukua abiria milioni 1,600,000 kwa mwaka.

Lakini swali la pili *design* ya mwanzo ilikuwa hairuhusu ndege kubwa aina ya *type E* kuegesha katika jengo letu na wakati tayari ndege hizo zinatua katika huu. Kwa hiyo, imebidi iongezwe na kwa sababu hiyo eneo la kusini mwa uwanja *apron* yake ilibidi iongezwe ili kuwezesha ndege aina ya *type E* kuweza kuegeshwa bila ya matatizo. Lakini vile vile kuna sehemu ya *parking* ya magari nayo imeongezeka lakini pia tumeongeza ule mfumo wa *security* ya ku-*handle* mizigo ya abiria, kwa hiyo hayo yote yamechangia katika kuongeza gharama za mradi.

**Nam. 19**

**Mpango Uliopo wa Kuyahifadhi Maji ya Mvua**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said** - Aliuliza:

Zipo kauli ya kuwa Zanzibar ina uhaba wa chemchem zenye kutoa kiwango kikubwa cha maji na pia kuongezeka kwa wakulima wa kilimo cha umwagiliaji maji. Zanzibar imejaaliwa kuwa na mvua kubwa zinazosababisha mafuriko na maafa, lakini maji hayo tumeshindwa kuyahifadhi ili kutusaidia katika maeneo ambayo maji yanahitajika kwa wingi.

a) Je, serikali haioni sasa umefikia muda muafaka wa kuweza kuyatafutia ufumbuzi wa kuyahifadhi maji hayo ili yasipotee kwa muda mchache kwa kuyaongoza na kuyapeleka baharini ili kuepuka maafa na mafuriko.

b) Je, serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kutafuta vyanzo vya kuyahifadhi maji hayo kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa maji tulionao.

c) Je, serikali imeangaliaje maziwa, mashimo ya maji na mito iliyojifukia ili kuifukua na kuweza kuhifadhi maji kama zamani, ili maji hayo yaweze kukaa katika ardhi na maeneo ambayo yatahifadhiwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake Nam. 19 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kutoa ufafanuzi kwamba kwa faida ya Mhe. Mjumbe na Wajumbe wengine walioko katika Baraza lako tukufu kwamba Zanzibar haina ukosefu wa vyanzo vya maji wala uhaba wa chemchem, isipokuwa kiwango cha maji kimepungua katika chemchem zilizopo kutokana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi. Pia napenda kutoa ufafanuzi kwamba serikali imeona umuhimu mkubwa wa kuyahifadhi maji hayo tangu mwanzoni mwa miaka ya 1980 kupitia utafiti uliofanywa na *FAO* na kuendelezwa na utafiti uliofanywa na *Halcrow* mwaka 1994. Vile vile mnamo mwezi Mei, 2007 Shirika la *UNDP* lilifanya utafiti juu ya Uvunaji wa Maji ya Mvua, tafiti zote hizo zimeainisha umuhimu huo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali ili kulipatia ufumbuzi tatizo hilo, ikiwa ni pamoja na kufanya mradi wa majaribio wa uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo ya Unguja na Pemba kupitia mradi wa *AfDB.* Vile vile Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imeshafanya mazungumzo ya awali na kampuni ya Kichina na tayari wamewasilisha *Concept Note* kwa

ajili ya ujenzi wa mabwawa kwa kuanza na Mto Kipange ili kuweza kuhifadhi maji.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said**: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nimuulize Mhe. Waziri kwamba maji ya mvua ambayo zamani yalikuwa yana mito mingi sana kwa hapa kwetu na ilikuwa mpaka kiangazi yanaweza yakabakia mpaka yakakutana na masika mengine na ukaona kwamba tulikuwa na miti mingi na kukosa kuwa hatuna joto ambalo limeongezeka kwa kipindi kirefu kwa ukosefu wa maji.

(a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba sasa hivi umefika wakati wa kuichimbua ile mito ya zamani iliyojifukia pamoja na mabwawa kama ya Mwanakwerekwe ili yaweze kuhifadhi maji mengi sana kuliko kuyaruhusu maji yale kwenda baharini kwa kukaribisha ukame.

(b) Ukiachia chemechem ya Mwanyanya iliyopo hapa Zanzibar ambayo tumeirithi kutoka kwa serikali nyengine za huko nyuma. Je, kuna chemchem nyengine ambayo tumeitayarisha au iko tayari au tuna dhana ya kwamba chemchem hii iko tayari kwa ajili ya kusaidia nguvu za maji hayo.

**Mhe.Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Ni kwamba serikali inaona umuhimu wa kuhifadhi hayo maji na ndio maana nimesema kwamba tumefanya mazungumzo na kampuni ya Kichina na tayari wamewasilisha *concepts note* kwa ajili ya kuhifadhi mabwawa na kufukua hiyo mito ambayo wanayoisema.

b) Ni kwamba tuna chemchem Gawani Bungumi kwa upande wa Wete na Kwapweza kwenye Jimbo lako la Chake Chake. Lakini kama nilivyokuwa nimesema mwanzo kwamba mabadiliko ya tabia nchi yanatuathiri kwa sababu tulikuwa tuna moja pale Machui lakini imekauka. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Ali Suleiman Ali swali la pili la nyongeza.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa majibu yake mazuri. Lakini pia niulize swali kwamba wananchi wa Zanzibar hasa Mkoa wa Mjini Magharibi tatizo letu ni kilio cha maji na kwa bahati nzuri tumeambiwa katika jibu lake siku za mvua tunapata maji mengi katika mabonde mbali mbali moja wapo likiwa la Mwanakwerekwe na Ziwa Maboga. Kwa kuwa kuna kampuni ya Kichina imefanya utafiti na maji haya yatapata suluhisho zuri kwa manufaa ya wananchi. Je, Mhe.Waziri maji hayo yatafanyiwa utaratibu wa kunywa au yatafanyiwa utaratibu wa kuhifadhiwa tu kwa kazi nyengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira**: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba utafiti ndio utaonesha haya maji yatafaa kwa namna gani. Lakini ni kwamba serikali inajitahidi kuhakikisha kwa wananchi wake wanapata maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi yao.

**Mhe.Hamad Abdalla Rashid:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe.Waziri wizara yake inahusika na kutoa vibali vya viwanja kwa wananchi.

a) Sababu kubwa ya maji kukauka kutoka vyanzo vyetu vya chemchem ni ujenzi wa nyumba karibu na maeneo ya

chemchem. Je, ni hatua gani wanazochukua kwa wale waliojenga chini ya vyanzo vya maji.

b) Wizara yake inahusika na kutoa viwanja. Kwa nini inawapa viwanja hivyo kujenga sehemu zile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Kwanza tunafanya ukaguzi na tunapokuwa tunagundua, lakini kabla ya kugundua tanafanya jitihada sasa ya kujenga uzio, lakini tunapogundua kama kuna uvamizi hatua tunazichukua.
b) Lakini unasema kwa nini vinatolewa vibali. Ni kwamba wanaojenga maeneo haya wanakuwa hawana vibali, hawajaomba vibali. Kwa sababu unapoomba kibali kile chombo ulichokiomba wanakuja kukagua wapi unataka kujenga, panaruhusiwa kujenga, lakini ni sehemu ya wale watu ambao hawafuati sheria ndio wanaojenga hivyo. Ahsante sana.

**Nam. 30**

**Hasara ya Kukosekana kwa Huduma ya Nishati ya Mafuta**

**Mhe. Simai Mohammed Said -** Aliuliza:

Katika kuanzisha mfumo wa *BPS* (*Bulk Procurement System*) ulisababisha matatizo ya kukosekana huduma ya nishati (*Petrol na Diesel*) na kupelekea kukosekana kwa huduma hizo katika vituo mbali mbali.

(a) Je, ni hasara gani serikali imepata katika kipindi hicho katika kukuza uchumi.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kimekosekana au kimepotea katika makusanyo ya kodi na katika huduma.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira -** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kimsingi serikali haijapata hasara yoyote katika kuanzisha mfumo wa uingizaji mafuta kwa pamoja *(BPS)*, na kwa maana hiyo pia serikali haijapoteza makusanyo yoyote yanayotokana na kodi ya mfumo huo moja kwa moja.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Naibu Spika, kimsingi nilikuwa nitumie kanuni ya 37 juu ya suala hili kwa sababu unashindwa kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu mfumo wa *BPS* ulisababisha vituo kukosa mafuta lakini serikali katika kila lita inayouza inapata makusanyo karibu ya shilingi 600 au na kidogo. *ZURA* ambayo ni taasisi inayosimamia chini ya wizara hii inapata shilingi 100 kwa kila lita inayouzwa. Sasa tunaposema kuwa serikali haijapata hasara, lakini mbali ya hilo kukosekana kwa mafuta imeleta *triple effect* kwamba uchumi pia kwenye sekta ya utalii na maeneo yote. Sasa tunaposema kwamba serikali haijapata hasara majibu haya sio sahihi na ninashindwa kuuliza swali la nyongeza. *(Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa maelezo ya ziada baada ya yale aliyotoa Mhe. Naibu Waziri. Amesema kwamba serikali haijapata hasara yoyote, hiyo inatokana na zile kodi zinazoingia kupitia uagizishiaji wa

mafuta. Mfano ni kwamba katika mwezi Septemba, 2017 kulikuwa na upungufu na upungufu huo ulitokea katika wiki mbili za mwanzo, lakini tarehe 18 Septemba mafuta yaliingia lita karibu 12 milioni, mafuta hayo yote yaliuzwa katika mwezi wa Septemba. Lakini vile vile Disemba mwishoni hadi mwanzoni mwa Januari kulikuwa na *crisis,* lakini yaliingia mafuta karibu lita 16.6 milioni na yanauzwa katika kipindi hicho ziada ya ile *average* ambayo tunaagiza kwa kila mwezi. Sasa kwa maana ya ada za kodi hakuna hasara kwa sababu yale mafuta yanaingia na yanauzwa yote.

Lakini kwa maana ya *indirect cost* hasara ambazo ni *indirect* hizo zipo katika ofisi kwa sababu mafuta yanapokosekana na shughuli za kiuchumi nazo zinasimama. Alichokisema Mhe. Naibu Waziri ni yale mapato ya serikali na ndivyo jibu lilivyokuwa. Kwa hivyo, kwa mapato ya serikali hakuna hasara lakini kwa maana ya uchumi kwa zile shughuli ambazo zinakwama hasara hiyo ipo. *(Makofi*)

**Nam. 40**

**Kupata Ujauzito Nje ya Ndoa**

**Mhe. Omar Seif Abeid -** Aliuliza:

Kwa kuwa kuanzia kipindi cha Julai, 2016/2017 jumla ya kesi 51 za matunzo ya watoto ziliripotiwa sambamba na kesi 42 za mivutano ya malezi ambao uhalisia wake ni mkubwa zaidi kuliko ilivyoripotiwa. Kwa kuwa kesi hizo zinawagusa zaidi wanawake kutokana na kuvunjika kwa ndoa na wasichana wengi hupata ujauzito nje ya ndoa na badala yake mzigo wa ulezi unaachiwa familia ya mwanamke.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kupambana na tatizo la wasichana kupata ujauzito nje ya ndoa.

(b) Je, wizara inachukua hatua gani za kisheria kupambana na watu wanaowapa ujauzito wanawake na kuwatelekeza na kuongeza mzigo wa malezi kwa familia ya mwanamke.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto -** Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye na yeye kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukaweza kukutana hapa tukiwa wenye afya njema.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sasa kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Jimbo la Konde swali lake Nam. 40 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali imejipanga na inaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto katika kipindi cha mwaka 2017 - 2022. Mpango ambao umezingatia juu ya namna ya kukinga wasichana kupata ujauzito nje ya ndoa kwa kutoa elimu katika maeneo mbali mbali ikiwemo familia, maskuli, madrasa, shehia. Vile vile imekuwa inaendelea na kazi ya utoaji elimu kupitia vyombo vya habari ili kukuza uelewa na madhara ya udhalilishaji likiwemo suala la athari za ujauzito kwa familia.

Wizara imeandaa kipindi maalum cha Stadi za Maisha kwa Vijana ambapo
mafunzo yametolewa kwa wanahabari kutoka vyombo 17 ili kuviwezesha kuifikia jamii kubwa zaidi kwa ajili ya

kuandaa vipindi mbali mbali na kuifikisha taaluma hiyo kwa vijana na wasichana. Lengo ni kuwawezesha kujielewa na kuwa na uthubutu wa kupambana na changamoto zinazowakabili kama vile kubakwa, kupewa ujauzito na ndoa za utotoni.

Mhe. Naibu Spika,Viongozi kutoka Taasisi 27 za vijana wamepatiwa mafunzo ya stadi za maisha, vijana 300 kutoka Wilaya tatu (3) za Unguja ikiwemo Wilaya ya Magharibi 'A', Magharibi 'B' na Kusini na vijana wa CCM 41 wa Wilaya ya Mjini. Kwa upande wa Pemba, Taasisi 16 za vijana na vijana wengine 150 walio nje ya skuli za Wilaya ya Mkoani, Wete na Chake Chake pia wamepatiwa mafunzo hayo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa hatua za kisheria ambazo wizara inachukua kwa wanaowapa ujauzito wanawake na badala ya kuwatelekeza na kuongeza mzigo wa malezi kwa familia ya mwanamke ni kama ifuatavyo:-

i) Kwa watoto kuwafungulia kesi za jinai watu waliowapa ujauzito watoto hao.

ii) Kwa watu wazima kuwapa msaada wa kisheria kufungua kesi za matunzo kwa Mahakama ya Kadhi na Mahakama ya Watoto pale inapofaa.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa ameeleza vizuri kwanza nachukua fursa hii kwa kumpongeza kwa mujibu yake mazuri ambayo yanatoa muelekeo jinsi gani wizara imejipanga kupambana na mambo haya. Lakini nilitaka kujua je, kuna kesi ngapi zilizokwisha kufunguliwa na ambazo wizara inazisaidia zinawapa msaada wa kisheria kwa wasichana hawa

waliopata mimba na kukatisha masomo yao kwa kipindi hichi cha Januari hadi Disemba, 2017.

Lakini pia ni msaada wa kisheria alioutaja kwamba kwa wasichana wanafunguliwa kesi za jinai na kwa watu wazima wanawapeleka kwenye Mahakama ya Kadhi. Je, wanashiriki vipi kuwasaidia hawa kuhakikisha kwamba haki inatendeka ili kuweza kupata haki kwa hao watu waliopata athari hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kuhusiana na suala la wizara kesi ngapi wamefungua na kuweza kusimamia. Napenda kumjibu kwamba hivi sasa hakuna kesi iliyofunguliwa na wizara ya msichana aliyetiwa mimba akiwa yupo skuli.

b) Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba inapotokea suala hili na tukawaelekeza hawa waathirika kwenye vyombo hivi vya sheria ambavyo nimevitaja, basi inakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba mtu yule sheria inatendeka na haki yake anaweza kupata kama sheria inavyoeleza.

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba wizara yake imechukua hatua kwa wale wote waliowapa ujauzito wanawake na kuwatelekeza lakini pia na kuwaongezea mzigo mzito wa malezi. Je, kwa mwaka 2016/2017 ni kinamama

wangapi ambao wameshasaidiwa na msaada huu wa kisheria na kufungua kesi za matunzo ya watoto.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chambani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa upande wa wanawake ambao wizara tumewapa wamenanii kesi hizo ni wanawake 35 ikiwa Unguja 7 na Pemba 28.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii nikaweza kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri, hivi karibuni kulitokea baba mmoja kisiwani Pemba kuwabaka watoto wake wa watatu wa kambo na mmoja kupata ujauzito. Je, Mhe. Waziri wizara yako yule ambaye alipata ujauzito ilimsaidia vipi.

b) Mhe. Waziri tulisikia kama kesi hii kila mtuhumiwa alipokuwa anapelekwa mahakamani alikuwa anazimia. Je, Mhe. Waziri kesi hii imefikia hatua gani katika kutolewa hukumu. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Vijana Kaskazini Pemba swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba suala lilitokea na lipo katika vyombo vya sheria mahakama. Lakini kwa vile sheria zinatubana kwamba suala likiwepo mahakamani hatupaswi kulizungumza. Lakini naomba

kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba mzee huyo anayesemakana kwamba akifika mahakamani alikuwa anazimia sio kweli na kwa awamu ya kwanza kwa sababu mzee yule amehukumiwa kwa kesi tatu, kwa kesi ya mwanzo tayari hivi sasa anatumikia miaka kumi jela kwa kesi ya mtoto wa kwanza.

b) Na suala la pili la mtoto aliyempa ujauzito kama wizara imesaidia vipi. Mhe. Naibu Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba baada ya kadhia ile sisi tulifika kwa mama yule na tukaiona ile hali na tukamtaka basi mama yule tuweze kumsaidia yule mtoto ambaye ni mjamzito kwa kipindi kile kutokana na mazingira anayoishi nayo pale mtaani walikuwa hawana raha. Lakini mama yule alisema kama yeye ana familia yake hawezi kutoa majibu kwa haraka mpaka akakae na familia yake wajadili. Kwa hivyo, sisi tunasubiri jibu la mama la mtoto yule.

Na kuhusu jambo jengine kama wizara kutokana na familia ile ilivyo duni basi tumeweza kuitia kwenye hesabu zetu za kuwa familia ile inaishi katika mazingira magumu na kuweza kuwapatia msaada huo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 46**

**Kuporomoka Maadili Kutokana na Utandawazi**

**Mhe. Omar Seif Abeid** - Aliuliza:

Kwa kuwa viongozi wetu wa Kitaifa nchini akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamekuwa wakikemea sana kuporomoka kwa maadili kutokana na athari za utandawazi

zilizoenea duniani na wazee kukosa muda wa malezi ya watoto wao majumbani.

(a) Je, ni kwa kiasi gani kwa sasa wizara imejipanga kuhakikisha kwamba inaweka sheria kali kwa mtu yeyote atakayevunja maadili yetu ya Kizanzibari.

(b) Je, kwa upande wa watalii na wageni ambao ni moja ya biashara yetu, kuna mpango gani wa kuwataka wavae mavazi ya kujistiri wakati wakiwa kwenye matembezi humu mjini.

(c) Je, kwa kazi zilizofanywa na zinazofanywa na wasanii wetu, kuna utaratibu gani wa kuzichuja na kuziondoa katika masoko na kuwasihi wasanii wetu kufanya kazi zao ambazo zinafuata maadili ya Kizanzibari.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo -** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa Jimbo la Konde swali lake Nam. 46 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, hatua inayochukuliwa na wizara ni kuendelea kuwaelimisha wananchi wetu juu ya umuhimu wa kulinda na kudumisha maadili ya utamaduni wao. Na pia sera yetu na sheria kali zinazoongoza Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni Sheria Nam. 7/2015 ambapo kati ya maeneo makuu yaliyotiliwa mkazo ni udhibiti wa maadili ya jamii kuanzia mavazi, uundaji wa sanaa, uandishi na uwasilishaji, ili kuhakikisha maadili ya jamii yanalindwa.

(b) Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii imesambaza taarifa katika mahoteli karibu yote ya kitalii na kuwatembeza wageni kuhusiana na namna watalii na wageni wanavyotakiwa kuvaa, wanapotembelea maeneo mbali mbali ndani ya kisiwa chetu. Jambo hili ni endelevu na hufanyika kwa kushirikiana na wamiliki wote wa hoteli na waongozaji wa watalii.

(c) Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba moja ya kazi za msingi zinazofanywa na wizara yangu kwa kupitia vyombo vyake, likiwemo Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni, ni kuhakikisha kazi yoyote inayotakiwa kuoneshwa kwa wananchi ni lazima ikaguliwe. Ukaguzi huu hufanywa katika ngazi zote kabla ya kuonesha kwa hadhira. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ya swali nililouliza, lakini nina swali moja dogo nataka kumuuliza. Ningependa tu nijue kwa kuwa kulikuwa na vile vikundi vya ngoma vya asili kule Pemba ambavyo kwa sasa havionekani katika kutekeleza zile shughuli zake za kuwaburudisha wananchi wetu.

Je, wizara ina mpango gani wa kuvishajihisha vikundi vile kuanza kurejea kufanya shughuli zake za kuburudisha kama pale asili.

Lakini kuhusiana na vile kutembeza wageni tumeona kwamba bado kuna baadhi ya sehemu chache kidogo, wengi wameitikia ule wito wa mavazi, lakini wengine bado. Je, wizara ina mpango gani ili kuhakikisha kwamba yale malengo yanafikiwa ya kwamba watalii wetu wakifika hapa wawe wanavaa mavazi yanayostahiki kwa ajili ya kulinda mila, desturi na silka zetu za Kizanzibari. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) vyote kwa pamoja.

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hivi wizara imo katika uendelevu wa kuvishajihisha vikundi hivi, ili kuona kwamba kwa upande wa Pemba vikundi hivi navyo vinafanyakazi vizuri, kama vikundi ambavyo vipo kwa upande wa Unguja.

Mhe. Naibu Spika, kwa ushahidi wa hii, kuna vikundi mbali mbali ambapo inapofika wakati wa shughuli zetu za kiserikali, lakini hata za kijamii vikundi hivi tayari sasa hivi vinaonekana vikifanya shughuli hii ya ushajihishaji wa shughuli zetu za kiserikali.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wageni wanapokuja hapa Zanzibar wanatembea ambapo utamaduni wetu hawatakiwi watembee vile. Lakini Mhe. Naibu Spika, nilisema kwamba katika jibu langu mama kwamba kuna elimu ambayo tumeitoa kwa baadhi ya mahoteli, wana taarifa ambazo tumezitoa kuhusiana na utamaduni wa mavazi kwa wale wageni wetu wanapoingia Zanzibar. Lakini sisi wenyewe pia tunatakiwa tulinde utamaduni wetu na inaonekana sasa Mhe. Naibu Spika, sisi wenyewe hatuutunzi utamaduni wetu, bali sisi tunawaiga wageni. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi na nitoe wito kwa jamii tuendelee kuendeleza tamaduni zetu ili na wageni watuige wao na sio sisi tuwaige wageni. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Hamida Abdalla Issa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kuna hizi *local tour* mbili ambazo ni *Excerpede* na *Flash Tour*, hizi ni

*tour* ambazo *shareholders* wake sio Wazanzibari na sheria ya utalii katika *local tour* inawataka wenye sifa wawe wazawa yaani Wazanzibari.

Je, Mhe. Waziri wizara yako inalitambua hili kwamba *shareholders* wa hizi *tours* mbili sio Wazanzibari. Kama inalitambua ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii Utamaduni, na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba swali hili halihusiani na swali mama. Swali ambalo nimelijibu ni la kiutamaduni sio la kiutalii. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba pale itakapofika suala la kiutalii basi swali lake aliweke na nitamjibu kadri ninavyoweza. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Said Omar Said:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa na mimi nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, watalii wanapotembea katika mji wakiwa na mavazi ya kwao huwa hawajamuiga mtu, lakini Wazanzibari watakavyovaa kama watalii huwa wameiga wageni. Je, wizara yako ina mpango gani wa kukomesha huu wigo wa utamaduni usiowahusu. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Said Omar Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe Naibu Spika, katika swali la nyongeza ambalo nimejibu hivi punde nilisema kwamba sisi Wazanzibari tunatakiwa tuutunze utamaduni wetu yakiwemo mavazi, lakini na mila, silka na desturi za Kizanzibari au Tanzania kwa jumla. Kwa hivyo, nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kukomesha kwa tabia hii, bali tabia hii

naomba sana isiendelee na sisi tuwe makini tutunze utamaduni wetu, kwa sababu kama nilivyosema kwamba sisi hatutakiwi kuwaiga wageni, wageni ndio watuige sisi. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy:** Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Nadir ninaposimama mimi na wewe ukae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea naomba niwakaribishe wageni ambao wamehudhuria hapa leo. Wageni wenyewe ni wa Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele na hawa ni viongozi wa Matawi ya CCM Jimbo la Kijitoupele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, naanza na Tawi la Melinne, Ndg. Husda Haji Ameir ambaye ni Mwenyekiti wa UWT Jimbo, Ndg. Wanu Sengeru Haji ni Mwenyekiti wa Tawi la Melinne, Ndg. Asha Nassor Hassan ni Katibu Mwenezi, Tawi la Kwarara, Ndg. Haruna Haji Ame ni Mwenyekiti, Ndg. Juma Mohammed Ali ni Katibu, na Ndg. Tatu Salum Kajo ni Katibu Mwenezi, Tawi la Kijito Upele. Ndg. Said Mtindo Ngalapa ni Mwenyekiti, Ndg. Salma Muombwa Ali, Katibu Tawi la Tomondo Uzi, Ndg. Mwatima Khamis Ameir ni Katibu Mwenezi, Tawi la Tomondo 'B', Ndg. Khamis Hamza Abdalla ni Katibu na Ndg. Rose Mary Pyusi Mtoka ni Katibu Mwenezi. Karibuni sana ndani ya Baraza la Wakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo jengine ni kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, anawatangazia wajumbe wa kamati hiyo wakutane kwenye

ukumbi namba 3 hapo juu mara baada ya kipindi cha maswali na majibu kumalizika. Ahsanteni. *(Makofi)*

## UTARATIBU

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy:** Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Kuhusu utaratibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wady:** *Bismilah Rahman Rahim.* Mhe. Naibu Spika, nasimama na kanuni ya 42 kuhusiana na hoja ya dharura.

**Mhe. Naibu Spika:** Sawa, kaa kwanza nisikilize na nyengine. Mhe. Simai Mohammed Said.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na nikushukuru sana kwa hekima na busara zako za meza yako unavyoendesha vikao vyetu. Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa kanuni ya 46, lakini pia nakazia kwa mujibu wa kanuni ya 49(1) na (27), pia na kifungu cha 88 cha katiba yetu ambacho kinazungumzia Kazi za Baraza la Wawakilishi. Naomba ninukuu:

Kifungu cha 88:

"Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake za kutokana na vifungu vya katiba hii, itafanyakazi kwa mambo yafuatayo ya utekelezajia:

(a) Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitajika kuwepo kwa sheria hiyo,

(b) Kujadili shughuli za kila wizara wakati wa kikao cha mwaka wa bajeti katika Baraza la Wawakilishi,

(c) Kuuliza maswali mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi,

(d) Kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya serikali katika njia ile ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, jana wakati mjadala wetu unaendelea niliomba utaratibu wakati Mhe. Waziri wa Afya anatoa michango yake kuhusiana na hoja ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii. Nilipoomba utaratibu kiti chako ambapo Mwenyekiti aliyekuwa anaendesha sio wewe, alininyima fursa ya kuomba utaratibu bila kujua nilitaka muongozo gani kutaka kutoa kiti chako.

Lakini mbali na hayo pia Mhe. Waziri wa Afya alitamka kwamba utaratibu utafuata baadae. Dhamira ile kwanza nilinyimwa haki yangu ya kuweza kutoa utaratibu na kupata muongozo wa kiti.

Pili, Mhe. Waziri wa Afya kitendo cha kusema kwamba utaratibu utafuata baadae, imeonesha dhahiri kwamba amemu-*intimidate* mwenyekiti ambaye anaendesha kikao kile. Kwa hivyo, mimi niombe tu kwamba sina malengo ya kumpeleka mwenyekiti kwenye Tume ya Maadili. Kwa hivyo, niombe kiti chako na busara zako kwamba serikali iendelee kukiheshimu kiti chako na wasifanye matendo ya kuweza kuwanyima fursa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pale wanapotaka utaratibu. Nakushukuru sana kwa kunisikiliza, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe Naibu Spika:** Mhe. Simai Mohammed Said, mimi jana nilikuwepo hapa na nafikiri Mhe. Mwenyekiti alijibu hoja yako

vizuri sana. Alichokueleza ni kwamba utaratibu mheshimiwa aliusema kabla kwamba utafuata baadae. Kwa hivyo, alikuwa anakutaka kutokana na utaratibu ambao tumeuweka hoja zote ambazo zinakuja katika kipindi hiki zitajadiliwa mwezi wa Septemba.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Naibu Spika, …

**Mhe Naibu Spika:** Aa! tusiendelee na malumbano. Sitaki kuendelea na wewe na malumbano, lakini sidhani kama pia una nafasi. Kama unavyosema, hutaki kumpeleka Mwenyekiti katika Kamati ya Maadili. Hatupelekani. Kama kupelekana kwenye Kamati za Maadili basi tutapelekana sana humu ndani, sio wewe tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nafikiri wewe utulie jibu ambalo litakuja mwezi wa Septemba, hapo ndio utaweza kuuliza maswali. Lakini haki ya kukusikiliza nimekupa hapa usiseme kwamba sijakupa haki ya kukusikiliza na hayo ndio majibu yangu sasa hivi. Endelea.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na ndio maana nilitanguliza maneno ya awali kwamba ninakushukuru sana kwa hekima yako na busara yako. Mimi nilichoomba ni kwamba Waziri wa Afya kumwambia Mwenyekiti kwamba utaratibu utafuata baadae, sio hoja ya mwezi Septemba. Kitendo cha Mhe. Waziri wa Afya kumwambia Mwenyekiti utaratibu utafuata baadae wacha niendelee, kwa hivyo alininyima mimi fursa. Kwa hivyo, mimi lengo ni kwamba serikali isifanye *intimidation* ya kukifanyia kiti. Kiti kiheshimike na ndio maana nikasema sina malengo ya kumpeleka Mwenyekiti katika Kamati ya Maadili. Nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Nashukuru, tuendelee. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Waheshimiwa Wajumbe, sitaki tena kusikiliza kuhusu utaratibu. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. *(Makofi/Vicheko)*

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wady:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mimi hapa nimesimama kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chaani upande wa Kandwi na Pwanimchangani kwa jumla. Nimesimama hapa wameniagiza kwamba hawana tena imani na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, wameshachoka kudanganywa, wameshachoka kustahamili na hivi sasa wamefikia hatua wanaomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aende akawaone ili atoe kauli yeye kuwa mtu wa mwisho waweze kumuamini.

Mhe. Naibu Spika, nikizungumza hivyo sasa hivi ni mwezi wa tisa wananchi wangu hawana maji kisa mashine tu, mashine ile ambayo inasemekana haikosi hata zaidi ya milioni 10. Leo mwezi wa tisa watu zaidi ya 5,000 hawana maji na wameshapata maradhi ya matumbo ya kuharisha.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Naibu Spika, nipate kauli kutoka serikalini ya uhakika kabisa. Mimi na Mhe. Mbunge wangu tumekuja hapa na mpaka jana usiku saa 5 tupo na wananchi, tupo tayari kuchangia kwenye mfuko wa jimbo milioni 5, ili na wao waweze kutoa hizo fedha kwa kupitia serikali ili mashine ikafungwe wananchi wapate maji. Sehemu ambayo walikuwa wakiitegemea bwawa ambalo ni la *reserve* limeshakauka maji hakuna. Mhe. Naibu Spika, naomba kauli kutoka serikalini.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Serikali naomba majibu. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kama alivyosema Mhe.

Nadir Abdul-latif Yussuf, alikuja juzi yeye na Mbunge wake wa Jimbo la Chaani, tukakubaliana twende *ZAWA* kwa ajili ya kutafakari kwa pamoja. Lakini kwa bahati mbaya sana tunataka kutoka yeye akaghairi tukaenda na Mbunge wake mpaka *ZAWA*, tulikubaliana baada ya kuona tatizo ni nini.

Kwa hivyo, sasa hivi mamlaka wanatafuta zile fedha kwa ajili ya kununua *pump* ya pale. Kama tayari yeye anazo hizo nyengine, basi hata leo *Bismillah* na zitolewe ili tulimalize hilo tatizo, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Mhe. Naibu Waziri nashukuru sana kwa majibu. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Naibu Waziri tayari ameahidi kwamba…

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wady:** Mhe. Naibu Spika, mimi niliomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kauli hii mimi siridhiki nayo. Nimeomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itujibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Sawa. Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na pia namshukuru mtoa hoja Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Naamini Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ametoa maelezo mazuri kuhusu kushughulikia tatizo la maji katika eneo la Kandwi, ni wajibu wa serikali kuondoa matatizo ya wananchi. Suala lake tumelipokea tutawasiliana tena na wizara husika, na kwa ile dhamira njema waliyonayo wizara husika pamoja na *ZAWA* ya kulimaliza tatizo hili, basi naamini tatizo hili litamalizwa na tutalisimamia ili limalizike na wananchi wa Kandwi wapate maji. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

## HOJA ZA KAMATI

### Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Mwaka 2017/2018

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima wa afya.

Kabla sijaendelea na hotuba yangu Mhe. Naibu Spika, naomba hii glasi iwekwe maji ili sauti ikinikauka niweze kunywa maji.

**Mhe. Naibu Spika:** Wasaidizi tunaomba maji kwa Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *Subhanahu Wataalla* kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kufika hapa katika kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kikatiba ya kuisimamia serikali na kuwakilisha wananchi wa Zanzibar katika kufanya maamuzi muhimu ya kitaifa. Aidha, naomba nimshukuru Mhe. Spika pamoja na wewe Mhe.Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama

inavyoelezwa na Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza lako tukufu (Toleo la 2016).

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano pia nataka niendelee kukushukuru tena wewe pamoja na Mhe. Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Mratibu wa Shughuli za Kamati na watendaji wako wote kwa kuiwezesha kamati yangu kufanya kazi zake zote bila ya matatizo yoyote katika kipindi chote cha kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutoa pongezi zangu na shukrani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mashirikiano makubwa waliyonipa katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi zetu za kamati. Ni ukweli usiopingika kuwa mashirikiano yao ndio nyenzo pekee iliyoifanya kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106 kama nilivyoeleza hapo awali ya Baraza lako Tukufu (Toleo la 2016). Aidha, majukumu ya kamati hii yamefafanuliwa katika jadweli la kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Katika utekelezaji wa majukumu yake kamati hii imepewa dhima ya kusimamia wizara mbili (2) zifuatazo:

1. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, na
2. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe, huu ninaosoma hapa ni muhtasari tu lakini naomba sana waangalie ripoti yetu kwenye kitabu, kwa sababu changamoto karibu zote tumezieleza katika kitabu hichi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Muundo wa Kamati, kamati hii imeundwa na wajumbe nane (8) pamoja na makatibu wawili

(2) na kama nilivyoeleza hapo awali kuwa kamati imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa baina ya wajumbe pamoja na makatibu wake. Hivyo, kwa kuthamini mchango wao mkubwa, naomba kuwatambulisha majina yao ili muweze kuwafahamu. Mhe. Naibu Spika, kamati yangu kama nilivyosema inaundwa na wajumbe 8 na makatibu 2 ikiongozwa na:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Suleiman Sarahan Said | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Khadija Omar Kibano | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohamedraza Hassanali | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Said Omar Said | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 10. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo hao wote ni timu ambayo tuliyofanyakazi kwa pamoja kuwasilisha ripoti hiyo. Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Pia kamati ilipata nafasi ya kwenda tena Tanzania Bara kwa ajili ya ziara za kimafunzo kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira mnamo mwezi wa Oktoba, 2017.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni wizara muhimu katika mfumo wa utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafaidika na huduma bora za maji, matumizi bora ya ardhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira pamoja na upatikanaji bora wa huduma za nishati iliyo

salama na endelevu kwa ustawi wa maisha ya wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo, kamati inaomba sana serikali kufanya jitihada za makusudi zitakazowezesha kazi za wizara hii kupata fedha za kutosha hususan katika kazi za maendeleo, ili ile kauli mbiu ya "Kuondoa Migogoro ya Ardhi" iweze kutekelezwa kwa vitendo. Kwani kwa vyovyote vile asilimia ndogo sana ya fedha za maendeleo iliyopatikana hadi Disemba, 2017 idadi ya fedha hizo ni finyu, na haiwezi wizara kutimiza yale majukumu yake waliyojiwekea hasa ikiwemo kuondoa migogoro ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, **k**amati imesikitishwa sana kuona kazi ya kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa Ng'ambo Tuitakayo katika eneo la Mwembeshauri imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu. Mpaka hivi sasa mradi huo umeshindwa kutekelezeka na hii itapelekea kuendelea na ujenzi usio salama katika maeneo yetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hali hii inatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa licha ya idara hizi kubeba majukumu makubwa ya shughuli za uendeshaji wa wizara nzima, lakini bado bajeti inayotengewa ni ndogo hali ambayo inapelekea baadhi ya shughuli kutotekelezeka ipasavyo kama vile ilivyopangwa kwa mwaka husika.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu hii ya Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi inatekelezwa kupitia Sekta ya Ardhi hapa Zanzibar. Aidha, sekta hii imeundwa na Idara ya Ardhi na Usajili (Mahakama ya Ardhi, Afisi ya Mrajis wa Ardhi na Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi), Idara ya Upimaji na Ramani na Mipango Miji na Vijiji.

Mhe. Naibu Spika, ambapo Idara na Taasisi hizo kwa pamoja zinaunda Kamisheni ya Ardhi inayoongozwa na Katibu Mtendaji ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa idara hizo.

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Ardhi ni wakala wa Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria Nam. 6 ya mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuanzishwa kwake ni kusimamia utawala wa ardhi na kupanga matumizi bora ya ardhi. Aidha, haki ya kulinda rasilimali muhimu ya ardhi iliyo chache na isiyoongezeka kwa maslahi ya Taifa na maendeleo ya jamii ni jambo la msingi lililozingatiwa katika uanzishwaji wa Kamisheni hii ya Ardhi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, **k**amati inasikitishwa sana na kuwepo kwa mamlaka mbili (2) tofauti katika usimamizi wa eka tatu, ambapo kwa upande wa Unguja suala la eka tatu linasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira lakini kwa upande wa Pemba linasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, jambo sio sahihi kwa sababu Unguja na Pemba wizara ndio hizo hizo ndio maana tukasema kwamba suala la eka tatu tunaomba kamati lisimamiwe Wizara ya Ardhi kwani wao ndio wanaotoa hatimiliki za umiliki wa maeneo na Wizara ya Kilimo ibakie na jukumu lake la msingi la kusimamia matumizi ya eka tatu kwa ajili ya kilimo na sio vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kadhia hii kamati inaitaka serikali kwa kushirikiana na wizara husika kupitia Kamisheni ya Ardhi kuandaa utaratibu maalum wa usimamizi wa maeneo yote ya eka tatu kwa upande wa Unguja na Pemba, ili kuweza kufikia yale madhumuni makuu yaliyoanzishwa na Kamisheni hiyo kwa utekelezaji bora na vile vile kwa kufuata kauli mbiu ya CCM ya

kuondoa kabisa migogoro ya ardhi iliyokuwepo hapa nchini kwetu.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ya Ardhi imeanzishwa kwa madhumuni ya kupokea, kusikiliza na kuamua kesi mbalimbali zinazohusiana na migogoro ya ardhi inayofikishwa katika mahakama hizo kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, **k**amati haijafurahishwa hata kidogo na utaratibu wa malipo ya wazee ya posho za ma-*assessor* yaani lile Baraza la Mahakama kwamba wamepata agizo kutoka serikalini hivi sasa walipwe shilingi 20,000 posho yao ya siku kwa kuendesha vikao badala ya shilingi 10,000 ambayo imepelekea kuathiri hali ya bajeti ya mahakama hiyo kulingana na bajeti iliopangwa katika mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika**,** kamati pamoja na kuwa imeridhika na ongezeko la posho la Wazee wa Mahakama (*Accessors*) kulipwa shilingi 20,000 badala ya shilingi 10,000 kwa siku kwa kufanya kazi ya usikilizaji kesi lakini ni vyema bajeti hiyo itengwe maalum isiingiliane katika *OC* za idara husika.

Mhe. Naibu Spika, kwani kumejitokeza tatizo hilo, kamati yangu imetaka wizara kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuweza kulitafutia ufumbuzi suala hilo linalohusiana na ongezeko la asilimia 100 ya malipo ya posho za Wazee wa Mahakama ya Ardhi ambalo linatokana na agizo la serikali, kwamba wazee walipwe 20,000 ambapo haikuwemo kwenye Bajeti hapo mwanzo, ambapo mahakama imeshindwa kununua hata *stationeries* kwa kutumia katika uendeshaji wa kesi zake kama vile zilivyopangwa kwa sababu karibu nusu ya bajeti ilikwenda katika kuwalipa ma-a*ccessors*.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kuweza kuwatengea fungu maalum Mahakama ya Ardhi kwa Wazee yaani ma-*accessors* ili kuwasaidia kuondokana na matatizo yaliyojitokeza hivi sasa katika hii bajeti inayokuja ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na serikali pamoja na wizara husika bado kamati yangu hairidhishwi na ukosefu na uchakavu wa nafasi za kutosha katika majengo ya Mahakama za Ardhi Zanzibar hali inayopelekea kutokufanya kazi kwa ufanisi. Mfano halisi Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja ambayo hadi leo kazi zake inafanya katika jengo la *Majestic* ambapo lipo mjini Unguja ambayo pia ni Ofisi ya Mahakama ya Ardhi Mkoa na Mjini Magharibi. Hii inatokana na Mahakama ya Ardhi ya Mkoa wa Kaskazini jengo liliopo Gamba kushindwa kuanza kazi kutokana na jengo lake kukosa fedha za matengenezo ili liweze kuendana na shughuli za mahakama.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na changamoto hiyo, kamati inaiomba serikali pamoja na wizara husika kutenga fungu maalum la fedha katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kulifanyia matengenezo jengo la Mahakama ya Ardhi liliopo Gamba ili kuwarahisishia wananchi walioko katika Mkoa huu wa Kaskazini kupata huduma hiyo kwa urahisi. Pamoja na hayo kamati inaipongeza sana Mahakama ya Ardhi kwa kuvuka lengo ya ile idadi ya kesi ambazo iliyokusudia kuzisikiliza.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mrajis wa Ardhi ni moja kati ya taasisi zilizo chini ya Kamisheni ya Ardhi. Taasisi hii imeanzishwa chini ya Sheria ya Ardhi Nam. 10 ya mwaka 1990. Kazi kubwa ya taasisi hii ni kusajili ardhi na kuweka kumbukumbu za uhaulishaji wote unaofanywa katika ardhi iliyosajiliwa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo, kamati hadi inapokea taarifa hii utendaji wa afisi hii na hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa kazi zao za ardhi na kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi inayoibuka siku hadi siku. Kutokana na mapungufu hayo kamati inaitaka Kamisheni ya Utumishi Serikalini kuwapatia Afisi ya Msajili wa Ardhi watumishi wa kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, licha ya upungufu huo, pia afisi hii inakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa usafiri wa kudumu na wa uhakika. Hali inayopelekea gari la mkurugenzi kutumika na mhasibu pamoja na wafanyakazi wengine kwa kazi za usajili na utambuzi wa ardhi. Kutokana na mwenendo huo, kamati inaiomba serikali kuwapatia magari ya kutosha ili kuweza kufuatilia kazi zao za usajili pamoja na utambuzi wa ardhi katika maeneo yote kwa upande wa Unguja na Pemba, ili waweze kufikia lengo kuu la ile Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi ya kuhakikisha kwamba mazingira ya kazi zao muda mwingi yanatumika nje ya maeneo kwa hivyo usafiri ni jambo la lazima.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi kidogo, naomba ukae ili niweze kuwatambulisha wageni wetu waliofika hapa. Leo wageni wetu waliofika hapa ambao ni wageni wa Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhim), na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kupitia kampuni *ya Drums of Africa* ambao wanatokea Korea ya Kusini na ambao wanatokana na kampuni ya *U & I International* ya Korea Kusini wamekuja kwa shughuli za "Ng'ambo Tuitakayo" na ujenzi wa Kiwanda cha Simu wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndg. Shaaban Juma na Mkurugenzi Mtendaji Haroun Mohammed. Wengine waliopo katika msafara huu ni Ndg. Wang Youn Youg, huyu ni *Executive Vice President,* Ndg. Lee Mong Chou, *Director General,* Lee Bok Souk, *Chairman,* Tean Joan Chee ni *Chief of Finance,* Ndg.

Juon Hangjoune, Ndg. Rou Young, Ndg. Chou Huon Houng, Ndg. Hong Joung Mou. *You are mostly welcome.* Tuendelee. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kututambulisha wageni wetu. Karibu Zanzibar ee! tupo tayari kupokea mipango yenu yote mliyokuja nayo kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea Idara ya Mipango Miji na Vijiji inafanyakazi ya utekelezaji wa Sheria ya Mipango Miji na Vijiji, Sura 85 ya 1995. Lengo kuu la idara hii ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inajiwekea mipango mizuri na endelevu ya matumizi ya ardhi na kusimamia utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, **i**dara hii bado inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa bajeti jambo ambalo linapelekea kazi zinazopangwa kushindwa kutekelezwa kwa wakati. Hii inatokana na kutegemea *OC* moja inayoingizwa kwa Kamisheni ya Ardhi igawanywe katika idara zote nne (4) zilizo chini yake jambo ambalo ni wazi kabisa si rahisi kuweza kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa.

Mhe. Naibu Spika, **k**amati yangu inaiomba serikali kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kulitafutia ufumbuzi suala la mbadala wa tatizo la uwezeshwaji wa uingizwaji wa *OC* katika wizara zote za serikali pamoja na taasisi zake.

Mhe. Naibu Spika, katika kulipatia ufumbuzi suala hili ni vyema kila idara ikawa na fungu lake la matumizi kwani kutokufanya hivyo kunapelekea kazi nyingi kushindwa kutekelezeka. Ndio maana maeneo mengi hapa Zanzibar hujengwa kiholela kwa

sababu idara inashindwa kuipanga miji na vijiji vyetu kwa wakati, ukizingatia kwamba kasi ya maendeleo na ujenzi imekuwa kubwa kulinganisha na kasi ya upangaji wa miji yetu.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inahimiza kutengwa kwa bajeti ya kutosha ili idara hii iweze kufanya kazi zake kwa wakati na ufanisi pamoja na kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya nchi. Pia, ili migogoro ya ardhi imalizike hapa Zanzibar, kamati inaomba tena kupatiwa bajeti ya kutosha Kamisheni ya Ardhi ili iweze kupanga na kupima miji na vijiji vyetu na kuzitambua ardhi zote zilizokuwepo hapa Zanzibar, ili kila mhusika apatiwe hati yake ya kumiliki ardhi na majengo ambayo itapelekea kuondoa kabisa hiyo migogoro ya ardhi iliyokuwepo hapa Zanzibar.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI**
**MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR *(ZAWA)***

Mhe. Naibu Spika, mamlaka hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kulinda na kuhifadhi rasilimali ya maji. Kamati hii imepokea taarifa bado kuna baadhi ya miradi ambayo utekelezaji wake unasuasua na hatimae kupelekea wananchi kuvunjika moyo. Miongoni mwa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

(a) Mradi wa Uchimbaji wa Visima unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;
(b) Mradi wa Maji Safi na Salama wa Mazingira Mkoa wa Mjini Magharibi – *ADF* 12;
(c) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji katika Mkoa wa Mjini na Magharibi - *JICA;*
(d) Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar - wa *Exim Bank* ya India; na

(e) Mradi wa Utekelezaji wa Uchimbaji wa Visima vya Ras al Khaimah.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, hatua mbalimbali za uendeshaji na uchimbaji wa visima hivyo kwa kazi za upelekaji wa umeme, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu na ulazaji wa mabomba makubwa na madogo na juhudi za Serikali kuipatia Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* zimekuwa zikiendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vilevile, mamlaka bado inakabiliwa na changamoto kubwa za ucheleweshwaji wa ulipaji fidia kwa wananchi katika maeneo ambayo miradi mbali mbali ya maji inapotekelezwa pamoja na kuchelewa kuunganishwa kwa mtandao wa maji wa visima vya Ras al Khaimah hiyo ni moja wapo ya sababu iliyopelekea ukosefu mkubwa wa maji katika maeneo yetu mbali mbali ya mijini na vijijini. Hivyo basi, kamati inaitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* kuharakisha zoezi la kuviunganisha visima vilivyochimbwa na Ras al Khaimah kama agizo la serikali linavyoelekeza. Kamati hii inaamini kwamba visima hivi vya Mradi wa Ras al Khaimah vikiunganishwa vyote tatizo la maji kwa kiasi kikubwa litaweza kupungua sana kwa sababu tatizo letu tumechimba visima vingi lakini tumeshindwa kuviunganisha, halafu bado tunaendelea kuchimba visima vyengine wakati kumbe ilikuwa tuelekeze nguvu zetu nyingi katika kukamilisha vile visima vya mwanzo ili maji yaweze kutumika.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa tatizo la uvamizi wa vianzio vya maji, kamati yangu inaishauri serikali kuanzisha Mamlaka ya Uhifadhi wa Mabonde na Vianzio vya Maji hapa Zanzibar, ili kuhakikisha kuwa suala la uvamizi na uharibifu wa vianzio vya maji linadhibitiwa na kuweza kuipunguzia majukumu Mamlaka ya Maji. Pia, kutenganisha majukumu ya Idara ya Uzalishaji wa

Maji na Idara ya Usambazaji wa Maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo muhimu ya maji.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kamati yangu inaiomba tena serikali pamoja na wizara husika kuunda chombo kingine kwa ajili ya kushughulikia usambazaji wa huduma ya maji na kuiachia Mamlaka ya Maji kubuni na kupanga miradi mikubwa na masuala ya kiutawala ili kuleta ufanisi wa upatikanaji wa huduma hii katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, kamati inaitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* kuharakisha zoezi la kuviunganisha visima vilivyochimbwa na Ras al Khaimah kama agizo la Serikali lilivyotaka kutokana na ripoti ya utekelezaji wa Mamlaka ya Maji iliyowasilisha katika Mkutano wa Baraza.

Mhe. Naibu Spika, tunashukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kamati ilifanya jitihada za kuionba serikali kutoa fedha maalum za dharura kwa *ZAWA* ili kuweza kuviunganisha visima vya maji na serikali imekubali kutoa fedha hizo. Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Waziri akija aje atuambie je, ni hatua gani Mamlaka ya Maji imeweza kutekeleza ile ahadi ambayo serikali ilikubali.

**SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR *(ZECO)***

Mhe. Naibu Spika**,** miongoni mwa majukumu makubwa ya Shirika la Umeme Zanzibar ni kuhakikisha kwamba huduma ya umeme inapatikana wakati wote katika hali ya ubora na salama kwa mijini na vijijini.

Mhe. Naibu Spika, **k**amati hadi inapokea taarifa hii, mamlaka bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo madeni sugu yanayolikabili Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO).* Licha ya

kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo madeni sugu yanayoikabili Shirika la Umeme la Zanzibar *(ZECO),* licha ya kukabiliwa na changamoto hizo bado kamati inafurahishwa na kuona kwamba bado Shirika la Umeme kwa miaka ya hivi karibuni limekuwa likifanya kazi zake kwa vizuri sana kwa upande wa Unguja na Pemba, ambapo umeme umekuwa ukisambazwa karibu katika Wilaya zote za Unguja na Pemba hadi visiwa vidogo vidogo kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, Sekta ya Umeme hapa Zanzibar bado inakabiliwa na tatizo la ongezeko kubwa la madeni kwa upande wa Shirika la Umeme yanayotokana na baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wateja binafsi kwa upande wa Unguja na Pemba hali inayopelekea shirika kusuasua katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa muktadha huu, kamati inasikitishwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutokulitekeleza ipasavyo agizo la kamati katika bajeti iliyopita la ukataji wa *OC* katika taasisi mbali mbali za serikali zinazodaiwa na Shirika la Umeme ili kuilipa moja kwa moja *ZECO* na kuipa nguvu kuweza kujiendesha kibiashara na sio kutoa huduma tu kama ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kamati yangu inaitaka serikali kwa hivi sasa kubeba mzigo wa kulilipa deni la Mamlaka ya Maji hadi hapo *ZAWA* watakapoweza kujitegemea wao wenyewe kwani kila siku deni hilo limekuwa likiongezeka na kulipa mzigo mkubwa Shirika la Umeme *(ZECO)* jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za shirika katika kujitegemea na kuendesha shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu pia inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhusiana na deni la *ZECO* kwa

*TANESCO,* fedha hizo zilipwe moja kwa moja *ZECO* na Serikali na wao ndio waweze kuwalipa *TANESCO* kwa sababu inayodaiwa ni *ZECO* na sio Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika**,** kamati yangu kwa uhakika inaunga mkono hatua zilizoanza kuchukuliwa na Shirika la Umeme kwa kuvifungia baadhi ya visima mita za TUKUZA kama *Pilot Project* ili Mamlaka ya Maji iweze kubuni mbinu mbadala ya kuongeza ukusanyaji wa mapato pamoja na kumudu kulipa madeni ya umeme yanayotokana na visima hivyo vya usambazaji wa maji mijini na vijijini. Hii ni kuutilia nguvu msemo unaosema "Kila Tone Moja la Maji ni Gharama Hivyo Tutumie Maji kwa Uangalifu" lakini vile vile tuweze kulipia.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza sana *ZECO* kwa kuweza kusimamia vizuri mapato yao hasa katika miaka ya hivi karibuni na kudhibiti upotevu wa mapato na kuanza kulipa gawio serikalini, hongera sana *ZECO*. Lakini pamoja na hayo bado, kamati inaitaka *ZECO* kutokubweteka kuendelea kuwa wakala wa kusambaza umeme kutoka *TANESCO,* bali ni vyema kutafuta vianzio vipya vyao wao wenyewe vya umeme mbadala ili kuweza kujitegemea kwa umeme wa uhakika hapa Zanzibar.

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR *(ZPRA)*

Mhe. Naibu Spika, mamlaka hii ina jukumu kubwa la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, aidha, mamlaka kwa sasa inakabiliwa na tatizo la kuchelewa kuundwa kwa Kampuni ya Petroli Zanzibar *(ZPDC)* pamoja na kuchelewa kuundwa kwa Bodi ya Mamlaka ya Utafiti

na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar kama sheria tuliyoitunga inavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na uchelewaji huo, kamati inaiomba sana serikali pamoja na wizara kuhakikishwa uundwaji wa Kampuni ya Mafuta ya Serikali ili kuweza kutimiza masharti ya Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta hapa Zanzibar, ili kuondokana na mfumo usio na tija kwa Taifa.

Mhe. Naibu Spika, naomba ifahamike kuwa kuharakishwa kwa kuundwa kwa taasisi hizo kutaanza kuwapa uzoefu wa kazi watendaji kwani majukumu yao ni makubwa kwaTaifa letu hasa kwa kuzingatia kuwa baadhi ya shughuli za utafutaji wa mafuta zimeanza kwa kasi na hivyo inahitajika maamuzi sahihi ya bodi. Lakini vile vile kunahitajika kwa kampuni hiyo itakayoanzishwa kwa mujibu wa sheria kuingia mikataba na makampuni yatakayokuja Zanzibar katika kutekeleza masuala ya mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia, kamati inaitaka Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuharakisha mchakato wa uajiri kwa *ZPRA* ili vijana hawa waanze kupatiwa uajiri lakini vile vile kupatiwa mafunzo ya kazi, kwani kazi hii inahitaji wataalam waliobobea lakini vile vile wenye uzoefu.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI *(ZURA)***

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati *(ZURA)* ni taasisi iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2013 ambapo jukumu lake kubwa ni kusimamia upatikanaji wa huduma bora za maji na nishati kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majukumu yanayowakabili, kamati bado haifurahishwi na hali ya utekelezaji wa kazi za ushushaji wa mafuta katika Bandari ya Mtoni, kutokana na utekelezaji wa mfumo wa *BPS* ulioathirika sana kwa kiasi kikubwa kutokana na kina cha maji katika eneo hilo la bandari ya Mtoni kutokidhi haja ya kufunga gati kwa meli kubwa. Kwani kama inavyoeleweka uwezo wa bandari ya Mtoni kwa meli kubwa ni wa meli zisizozidi uzito wa tani 3,500. Kwa hiyo hii hupelekea kwamba meli kubwa haziwezi kufunga katika gati hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, kamati inaishauri Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuweka miundo mbinu mbadala kwa ajili ya kuingiza mafuta ndani ya nchi kupitia bandari zetu za  hapa Zanzibar pamoja na eneo lililotengwa katika eneo la Mangapwani.

Mhe. Naibu Spika,  aidha, kamati inasisitiza kwamba kwa kuwa tayari limetengwa eneo la Mangapwani kwa ajili ya kuweka miundo mbinu ya kuteremshia na kuhifadhia mafuta, basi ni vyema serikali ikashirikiana na wawekezaji binafsi ambao wako tayari kushirikiana na serikali kuandaa utaratibu wa kuanza ujenzi wa miundo mbinu hiyo ya kuhifadhia mafuta huko Mangapwani, ili kuondoa tatizo la upatikanaji wa mafuta hapa Zanzibar lakini vile vile kuweza kupunguza bei ya mafuta hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika,  kutokana na hali hii, kamati inaitaka Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar kushirikiana kikamilifu pamoja na kuwashirikisha wawekezaji wanaoingiza mafuta hapa Zanzibar kushauriana nao juu ya namna watakavyoweza kushirikiana na serikali katika kuendeleza eneo tengefu la Mangapwani kwa ajili ya kuingiza mafuta na gesi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni kukosekana kwa bohari kubwa ambayo itawezesha muagizaji na muingizaji wa mafuta kuweza kuhifadhia mafuta yake baada ya kufika hapa Zanzibar, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu, hali inayopelekea upungufu wa mafuta mara kwa mara kutokea hapa Zanzibar kutokana mahitaji makubwa ya mafuta lakini *storage* tulizokuwa nazo ni chache.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na tatizo hilo, kamati inaiomba serikali kama tulivyoeleza hapo mwanzo kupitia Tume ya Mipango pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na wadau wanaoingiza mafuta na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika eneo la Mangapwani, kuweza kuweka mkakati wa matumizi ya eneo la Mangapwani lililotengwa kwa ajili ya shughuli za mafuta ili wananchi waweze kuondokana na changamoto hiyo ya kuadimika kwa mafuta siku hadi siku.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

## MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR *(ZEMA)* NA IDARA YA MAZINGIRA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, kamati wakati wa kupokea taarifa ilifurahishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar *(ZEMA)* ambayo katika robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2017) imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 15,300,000/= sawa na wastani wa asilimia 142 ya kiwango kilichopangwa kukusanywa katika robo hiyo ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, ongezeko hilo la makusanyo, kamati bado inasikitishwa na kuwepo kwa ufinyu wa Ofisi ya Mkurugenzi, pamoja na Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi wa Idara ya

Mazingira kwa Unguja na Pemba, hali inayopelekea kufanyakazi zao katika ofisi moja. Nafikiri suala hili Mhe. Naibu Spika, tumeongea na wizara wametuahidi kwamba kuna mpango wa kuweza kuwatenganisha wakurugenzi wale kwa hivyo tunaomba suala hili wizara iliharakishe.

Mhe. Naibu Spika, kamati imezidi kusononeshwa hadi tunawasilisha ripoti hii, bado Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mazingira pamoja na Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira kuendelea kukaa katika ofisi moja jambo ambalo haliendani na hadhi na taswira ya kazi zao. Hali hii inapelekea mamlaka hii kutotambulika uwepo wake. Hivyo basi, kamati inaitaka wizara kuangalia suala hilo kwa jicho pana na kuondoa tatizo hilo mara moja.

Mhe. Naibu Spika, **s**ambamba na hilo, kamati inaishauri tena serikali pamoja na wizara kuangalia upya sheria kwa upande wa wanaoingiza mifuko ya plastiki, wanaokamatwa nayo wakati wa matumizi, pamoja na kuandaa kanuni za kulipa faini kubwa tena za papo kwa papo ili kuondokana na tatizo hilo kupeleka kesi hizo ndogo ndogo mahakamani ambapo kunapelekea urasimu, lakini vile vile usugu wa wananchi katika kutumia mifuko ya plastiki.

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI**

Mhe. Naibu Spika, kama inavyofahamika kuwa wizara hii imepewa majukumu makuu ya kusimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafiri Zanzibar. Aidha, taasisi zinazosimamiwa na wizara hii zinatekelezwa kupitia Idara, Mashirika na Mamlaka zifuatazo:

1. Ofisi Kuu Pemba
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
4. Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara
5. Idara ya Usafiri na Leseni
6. Idara ya Mawasiliano
7. Mamlaka ya Usafiri wa Baharini
8. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege
9. Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe
10. Shirika la Meli na Uwakala
11. Shirika la Bandari
12. Shirika la Nyumba pamoja na Wakala wa Majengo.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI**
**SEKTA YA UTAWALA**

Mhe. Naibu Spika**,** sekta hii inaundwa na Ofisi Kuu Pemba, Idara ya Mipango na Utumishi na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Jukumu kubwa la sekta hii ni kusimamia masuala ya kiutumishi, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika**,** sambamba na hilo, kamati inasikitishwa na utendaji wa baadhi ya kazi zinazosimamiwa kupitia sekta hii kukosekana kwa mawasiliano mazuri katika Idara ya Mawasiliano na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara hasa katika wakati wa uwekaji wa Mkonga wa Taifa, ambapo kila panapofanywa utanuzi wa barabara mkonga huu unaathirika. Suala hili tumelizungumza kwenye kamati naamini watendaji wataweza kulishughulikia ili lisijitokeze tena na kuitia hasara serikali.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kadhia hiyo, kamati yangu inaiomba wizara kushirikiana na idara husika kujenga mahusiano

na ushirikiano wa karibu katika kutekeleza kazi zao, ili kuondoa sintofahamu katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi mbalimbali zilizo chini ya wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine inayoikabili wizara hii ni kukosekana kwa mtambo madhubuti wa kutengenezea lami. Hivyo, kamati inaiomba serikali kwa kushirikiana na wizara kuharakisha ununuzi wa mtambo wa kutengenezea barabara kwani iliyopo sasa hivi ni ya muda mrefu na kupelekea kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa ujenzi pamoja na matengenezo ya barabara kwa wakati unaopangwa. Mtambo uliopo sasa ni wa muda mrefu na kupelekea kushindwa kufanya kazi za ujenzi pamoja na za matengenezo ya barabara kwa wakati uliopangwa na hatimaye kusababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi na kupelekea serikali kuingia katika hasara kubwa ya kiutendaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli, serikali imekusudia kununua mtambo mpya kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Kamati yangu inaendelea kuisisitiza serikali kwa kushirikiana na wizara husika kununua mitambo yenye ubora na sio kuangalia mitambo kwa bei ya chini ili isije kununuliwa mitambo ambayo viwango vyake viko chini. Kamati yangu hili inaendelea kulisisitiza na itahakikisha inalisimamia.

**PROGRAMU YA UHIFADHI NA UIMARISHAJI WA MAKAAZI**

**SEKTA YA NYUMBA**

**SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Zanzibar ni taasisi inayojitegemea ambayo inafanyakazi zake kwa mujibu wa Sheria

Nam. 6 ya mwaka 2014. Sheria hii inaipa mamlaka Shirika la Nyumba Zanzibar kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusiana na ujenzi, uuzaji na ukodishaji nyumba za kuishi na za biashara.

Mhe. Naibu Spika, shirika hadi linatoa taarifa hii kwa kamati linakabiliwa na changamoto ya kutokukamilisha zoezi zima la kutathmini majengo yote yanayosimamiwa na serikali kwa upande wa Unguja na Pemba. Kutokana na tatizo hilo, kamati inalitaka shirika kuyafanyia tathmini na uhakiki majengo yote ya serikali yaliyopo katika eneo la Mji Mkongwe pamoja na maeneo mengine kwa upande wa Unguja na Pemba, ili kuweza kuzitambua na kupatikana kwa idadi halisi ya nyumba hizo jambo ambalo litaweza kusaidia pia kusimamia na kukusanya kodi kama ipasavyo.

## WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, malengo makuu ya Wakala wa Majengo ni kuwapatia Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali makaazi ya uhakika, bora na salama, kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa ujenzi wa majengo ya serikali kulingana na mahitaji husika, kutayarisha utaratibu endelevu wa matengenezo ya majengo ya serikali, kuweka mpango mzuri wa kuhakiki makadirio ya ujenzi katika miradi ya serikali, pamoja na kusimamia na kuendeleza majengo yote ya serikali ikiwa ya makaazi, biashara au ofisi.

Mhe. Naibu Spika, licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na Wakala wa Majengo bado inakabiliwa na ukosefu wa ofisi ya uhakika kwa ajili ya kufanya kazi za kila siku, kwani hivi sasa wameanzimwa jengo la *ZSSF* liliopo Kilimani na hadi kamati inapokea taarifa hii wakala imeshapokea barua kutoka *ZSSF* ya kuwataka wahame katika jengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na tatizo lililojitokeza, kamati yangu inaitaka Wakala wa Majengo kuendelea kubaki katika jengo hilo na wasihame hadi *ZSSF* watakapowalipa fidia kutokana na kubomolewa na kuhamishwa kwenye jengo lao hapo Michenzani bila ya kulipwa fidia. Kwa hivyo, *ZSSF* kama wanataka kuwahamisha Wakala wa Majengo basi wahakikishe kwamba wanawalipa fidia ili waweze kujenga au kukodi jengo jengine kuweza kufanya shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, Wakala wa Majengo pia ina uchache wa wafanyakazi hususan katika kada ya maseremala na wataalam wenye fani maalum za majengo katika ofisi zake kwa Unguja na Pemba. Wataalam hao kama vile *Civil Engineers, Architects, Quantity Surveyors*, *Electrical Engineer* pamoja na *Mechanical Engineer.*

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo, kamati inaishauri Wakala wa Majengo kupitia bodi inazozisimamia kuandaa Muundo wa Utumishi kwa Ofisi na kuuwasilisha Tume ya Utumishi Serikalini ili kupata idhini ya kufanya uajiri wa wafanyakazi wa kudumu katika fani maalum za majengo, ili kuondokana na tatizo la wafanyakazi wa muda.

**PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**

**SEKTA YA NCHI KAVU**

**IDARA YA UTUNZAJI NA UENDELEZAJI BARABARA (UUB)**

**Mhe. Naibu Spika**: Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa nimuachie Mhe. Mwenyekiti, ili aweze kuendelea na shughuli yetu hii ya leo.

*Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwenyekiti endelea.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kuendelea kumalizia hotuba yangu Sekta ya Nchi Kavu.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utunzaji na Uendelezaji Barabara ni taasisi ambayo inafanyakazi za kujenga na kuzitunza barabara za visiwa vya Unguja na Pemba. Hali ambayo inapelekea kupatikana kwa mafanikio mbali mbali ikiwemo miundo mbinu bora ya barabara inayopitika muda wote wa misimu ya mwaka pamoja na kupungua kwa gharama za usafirishaji mizigo na abiria.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa ulipaji fidia kwa wananchi walioathirika katika ujenzi wa barabara zikiwemo nyumba na vipando, jambo ambalo linapelekea kushindwa kutekelezwa kwa baadhi ya miradi pamoja na kuchelewa kwa uingizwaji wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwenda Idara ya Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfuko wa Barabara kuacha urasimu wa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara, kwani fedha wanazokusanya madhumuni yake ndio hayo na sio kitu kingine isipokuwa kuzienzi na kuzihami barabara zetu za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati inaishauri pia serikali kutenga fedha za kutosha ili kuitia nguvu Idara ya Utunzaji na Uendelezaji

wa Barabara (UUB) kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa katika kuleta maendeleo kwa jamii. Kama tulivyoeleza kuharakisha ununuzi wa mitambo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, kwani mitambo waliyokuwa nayo sasa hivi kwa kweli ni michakavu sana na wanasumbuka sana katika utendaji wa kazi zao.

## SEKTA YA USAFIRI WA MAJINI

Mhe. Mwenyekiti, **s**ekta hii inajumuisha Shirika la Bandari, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini *(ZMA)* na Shirika la Meli na Uwakala.

## SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

Mhe Mwenyekiti, kamati inatambua kwamba Shirika la Bandari lina jukumu la kuziendesha, kuzisimamia na kuziendeleza bandari tano (5) za Zanzibar ambazo ni Bandari ya Malindi, Mkokotoni, Wesha, Mkoani na Wete.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasikitishwa na madeni makubwa wanayodai Shirika la Bandari kutoka *Tanzania Port Authority* yanayotokana na huduma za utumiaji wa minara na maboya kwa meli zinazokwenda Tanzania Bara jambo ambalo linaongeza idadi ya changamoto za Muungano. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa sana kuna mapato ya minara ambayo sasa hivi zaidi ya miaka miwili Shirika la Bandari la Zanzibar halijalipwa na Shirika la Bandari la Tanzania. Kwa hivyo, tunaomba serikali ihakikishe kwamba deni hili linasimamiwa na linapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia inaishauri Shirika la Bandari kukaa pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kumaliza changamoto za upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo yote yaliyo chini ya Shirika la Bandari. Kwani kitendo cha kukosekana

kwa hatimiliki katika bandari zote za serikali kwa upande wa Unguja na Pemba kunapelekea wananchi kuvamia pamoja na kujimilikisha maeneno hayo kinyume na taratibu, ukizingatia bado taasisi inayohusika inaendelea kutoa hati hizo kwa wananchi kwa ajili ya matumizi ya makaazi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mapungufu hayo, kamati inaiomba serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kukamilisha zoezi zima la upatikanaji wa hatimiliki kwa maeneo yote ya bandari na minara kwa Unguja na Pemba, ili kuweza kuyahami maeneo hayo na uvamizi unaoendelea kushamiri unaofanywa na wananchi kwa kujenga makaazi pamoja na kufanya shughuli zao za kibiashara katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na Ofisi za Halmashauri, Wilaya na Masheha kuyalinda maeneo ya bandari kwa upande wa Unguja na Pemba na kutotoa vibali vya ujenzi katika maeneo hayo bila ya idhini ya waziri anayehusika na masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile, shirika linakabiliwa na uchelewaji wa malipo ya huduma zinazotolewa kwa baadhi ya makampuni na mashirika yakiwemo *Azam Marine* na Shirika la Meli la Zanzibar, hivyo kupelekea kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu kwa shirika yanayosababisha kuzorota kwa kazi za shirika. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba wale wote wanaohusika kuweka kukaa pamoja na Shirika la Bandari ili kuweza kusawazisha madeni yao.

## MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR *(ZMA)*

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri Baharini ina jukumu la kusimamia safari za baharini, uchunguzi wa ajali baharini, uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa maeneo ya Zanzibar,

usimamizi wa maslahi ya mabaharia, pamoja na kusajili na kutoa vibali na leseni kwa taasisi zinazotoa huduma za meli na bandari.

Mhe. Mwenyekiti, kusitishwa kwa zoezi la usajili wa meli za nje kufuatia meli zilizokamatwa ambazo zilisajiliwa Zanzibar na kupokea agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumepelekea kusimama kwa ufanyaji kazi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini *(ZMA)* katika suala zima la usajili wa meli za nje, jambo linalosababisha kupunguza vianzio vya makusanyo ambayo mamlaka ilikwisha kuyapanga katika bajeti yake ya mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na changamoto hiyo iliyoanza kujitokeza kwenye usajili wa meli za nje hasa kukiuka Sheria za Kimataifa ikiwemo kupakia magendo ya silaha pamoja na madawa ya kulevya, ni vyema *ZMA* izungumze na Makampuni ya Meli tuliyofunga nayo mikataba kuheshimu makubaliano hayo lakini pia kuweka masharti magumu kwa meli mpya ambazo tunazisajili kwa kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka pia inakabiliwa na kikwazo cha matayarisho ya usajili wa *VAT* ambapo kuanzia mwezi Januari, 2018 Serikali ya *UAE* imeanza kutoza kodi kwa biashara mbali mbali zinazoendeshwa nchini humo. Aidha, *ZIMS* hadi kufikia sasa haijafanya usajili wa kodi ya *VAT* lakini kwa taarifa Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa hii kodi tayari imeshasajiliwa lakini vile vile mkataba wa uwakala baina ya *ZMA* na *ZIMS* ambao upo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali unafanyiwa kazi tangu tarehe 22 Novemba, 2017 na kuchelewa kumalizika kwa mkataba huo kutapelekea *ZIMS* ambao ni wakala wa *ZMA* Dubai kuweza kutozwa faini. Kwa hivyo, tunaomba sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuhakikisha kwamba mkataba huu unakamilishwa ili kuhakikisha kwamba *ZMA* wanafanya kazi zao kwa utulivu kule Dubai.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuepukana na kikwazo hicho, kamati inaiomba serikali kuhakikisha kwamba suala hili linaharakishwa au linakamilika, tunaamini Mhe. Mwanasheria Mkuu suala hili ataweza kulitolea kauli na sio kusubiri mpaka Septemba. Mhe. Mwenyekiti, Tawi la Dubai la ZMA sasa hivi limekuwa katika mtihani mgumu wa kufanya kazi zake kama mkataba huo utakuwa haujakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwa kipindi kirefu sasa, mamlaka hii inakabiliwa na ukosefu wa vyombo vya kudumu vya uokozi baharini hali inayoweza kupelekea kushindwa kudhibiti janga lolote linaloweza kutokea katika nchi yetu. Kutokana na hali hii, kamati inaiomba serikali kutenga fedha kwa ajili ya kununulia vyombo hivyo vya uokozi pamoja na taasisi zinazohusika kuchangia kiasi cha asilimia kwa mamlaka hiyo kutimiza wajibu wao ili kujiweka tayari pindipo majanga ya bahari yatakapotokea.

**SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR**

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli Zanzibar limepewa jukumu la kusimamia na kuendesha meli zote za serikali pamoja na kutoa huduma za uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika bandari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa meli ya MV Mapinduzi II, changamoto kubwa inayojitokeza ni usimamiaji na uendeshaji wa meli hiyo unaotokana na uharibikaji wa mara kwa mara unaopelekea kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi kama ilivyotegemewa. Aidha, kukosekana kwa ushirikishwaji wa watendaji wataalam katika hatua za mchakato mzima wa manunuzi ya meli mpya jambo ambalo sasa hivi athari zake tumeanza kuziona.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri serikali kupitia Shirika la Meli kusomesha wataalam wa kuzihudumia meli zote mpya zinazonunuliwa na zitakazonunuliwa na ikiwezekana hivi sasa kuandaa utaratibu wa kuanza kuwapeleka kwenye mafunzo wafanyakazi, ili meli nyengine zitakazonunuliwa waje waweze kuzihudumia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapenda kuishauri serikali tena kwa mara nyengine pamoja na wizara husika kupitia Shirika la Meli Zanzibar kutafuta meli nyengine mbadala itakayoendana na mazingira ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba na kuondosha usumbufu uliopo pindipo meli ya MV Mapinduzi II itapokumbwa na tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa kuwa tunazo taarifa za mipango ya serikali kununua meli nyengine mpya ya abiria, kamati inaiomba serikali pamoja na wizara husika kuanza kusikiliza maoni ya wataalam wa shirika juu ya aina ya meli tunayoihitaji na ambayo itaendana na mazingira ya bandari zetu na mahitaji ya abiria wetu hapa Zanzibar.

**SEKTA YA ANGA**

**MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR**

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria Nam. 9 ya mwaka 2011 ambayo awali ilikuwa ikijulikana kama Idara ya Anga. Aidha, mamlaka inaendesha, inasimamia usalama kwa safari za abiria na mizigo na kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka inakabiliwa na ukosefu wa mashine za kukagua mizigo mikubwa katika Uwanja wa Ndege wa Amani

Abeid Karume pamoja na upungufu wa mashine za kukagulia abiria na mizigo midogo midogo, hali inayopelekea baadhi ya mashirika ya ndege kukataa kabisa kubeba mizigo kutoka Zanzibar kutokana na ukosefu wa mashine ya uchunguzi wa mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, katika huduma zinazotolewa katika uwanja, mamlaka inakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa mikanda ya mizigo *(conveyer belt)*, pamoja na kutokuwepo kwa idadi na taarifa kamilifu za abiria pale zinapohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na matatizo yanayoikabili mamlaka, kamati inaiomba wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuimarisha maeneo ya kupitishia mizigo *(conveyer belt)* ili kuondosha usumbufu kwa abiria hususan wakati wa kushuka kwa abiria hasa kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati inaishauri wizara kushirikiana na mamlaka kuliangalia kwa makini suala la *scanner* ambalo hutumiwa na wafanyakazi kupitisha mizigo tofauti hali inayopelekea hata kupitishwa kwa baadhi ya vitu kinyume na taratibu za kisheria. Mfano halisi ni tukio ambalo limeweza kujitokeza hivi karibuni katika viwanja vyetu vya ndege vya Zanzibar.

**HITIMISHO**

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na wafanyakazi wote wa wizara hizo mbili zinazosimamiwa na kamati yetu hii pamoja na taasisi zao kwa juhudi kubwa walizozichukua katika kutekeleza majukumu yao. Kamati pia inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa

Kamati hii pamoja na wale wote waliofanikisha kazi yetu ya kamati kufanikiwa kwa mwaka 2017/18.

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wewe mwenyewe kunipa nafasi hii. Pongezi za mwisho kabisa naomba kuzitoa kwa Mawaziri wote wawili wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, lakini vile vile na Wizara ya Mawasiliano, Ujenzi na Usafirishaji, pamoja na Manaibu wao kwa mashirikiano makubwa waliyotupa katika kipindi chote tulichokuwa tukifanya kazi nao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Mawaziri hawa pamoja na Manaibu wao pamoja na Makatibu Wakuu walitupa mashirikiano makubwa, walitupa kila tunachohitaji katika kuhakikisha tunatekeleza malengo yetu. Nawaombea kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao, Mwenyezi Mungu awajaalie kazi zao walizozipanga ziweze kwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naishukuru Kamati pamoja na Wajumbe wote na Makatibu wangu, pamoja na wananchi wa jimbo langu la Shaurimoyo kwa kuweza kunipa nguvu ya kuweza kusimama hapa kuwasilisha hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa uwasilishaji wako, hoja imetolewa na inaungwa mkono. Sasa Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na michangio ya hoja iliyopo mbele yetu. Mchangiaji wa mwanzo atakuwa Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajitayarishe.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kwa heshima zote kwa kunipa nafasi na *Alhamdulillah* sisi sote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uwezo huu na kutupa pumzi.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii ambayo muda mchache tu amemaliza hotuba yake ambayo imejaa hekima, busara na usikivu. Mimi nikiwa mjumbe wa kamati hii ya wizara hii aliyoisoma ndugu yangu namheshimu sana Mhe. Hamza Hassan Juma naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa nataka nizungumze pamoja na wenzangu Wawakilishi kwamba kazi yetu kubwa iliyotuleta humu ndani ni kutekeleza ahadi za wananchi, lakini kuiunga mkono serikali, tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mwenyekiti wa Kamati amezungumza changamoto nyingi maji, barabara, umeme, mambo mengi na yote alikuwa akigusia ufinyu wa bajeti, hali ya fedha, hali ya uchumi. Haya yote ukitizama uki-*wind up* unakuta kwamba tatizo ni hali ya fedha tuliyokuwa nayo ndani ya serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiwa mwananchi nikianza kusimama nianze kusema kwamba Uzini sina maji, sina barabara, tutakuwa sote huku tutakuja na hoja binafsi huenda tukaleta mpaka wananchi, mimi nikaleta wananchi kutoka Uzini waje kufanya maandamano. Lakini kama tunataka *problem* tutatue ni lazima tushirikiane tutizame namna gani ya kuweza kuisaidia Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na sisi tukiwa Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa mwezi wa Ramadhan unakaribia kuwepo

*inshaallah* kwa uwezo wake na tatizo kubwa sugu katika mwezi huu wa Ramadhan ni maji na hali yetu ya fedha *ZAWA*. Wizara yenyewe kama unavyojua *ZAWA* mpaka wakusanye ili waweze kununua. Kuna mashine nyingi katika majimbo ya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Waziri wa Fedha leo asubuhi Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed alisema serikali imeweza kukopa pesa pamoja na riba katika kujenga Uwanja wa Ndege ule wa *Terminal III* na mkopo utakuwa wa riba. Mimi nikiwa kama mwananchi *Alhamdulillah* serikali hii ndiyo iliyonifanya nifike hapa, basi na mimi nataka nitoe mchango wangu kwa sababu ya mwezi wa Ramadhan. Sawa wana matatizo ya mashine inaweza ikawa ile *ZAWA* hali yao ya fedha ya makusanyo hawawezi kupata kwa mara moja hizo pesa. Naomba kupitia Waziri anayehusika niko tayari kuisaidia wizara mkopo usiokuwa na riba, usiokuwa na masharti, ni kuambiwa tu kwamba nitoe mkopo kwa muda wa miezi minne mpaka Ramadhan iishe, *ZAWA* kupitia waziri nitoe hizi mashine zilizokuwa zinahitajika ili wananchi wetu waweze kufaidika na maji.

Mhe. Mwenyekiti, Ramadhan kwa Zanzibar ni sawa sawa na Kikwajuni kuuliza asumini. Ninachoomba mimi nikiwa kama mfanyabiashara kupitia kampuni yangu niko tayari kupitia Wizara inayohusika ya maji kuipa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia *ZAWA* milioni mia mbili (200) ili waweze kununua mashine za maji kwa visiwa vya Unguja na Pemba bila ya masharti, bila ya riba, ili wananchi wetu waweze kufaidika baada ya Ramadhan nirejeshewe pesa zangu bila ya masharti yoyote zikanunuliwa mashine. Naomba Mhe. Mwenyekiti, niwasilishe barua yangu hata kama hizi peza kupitia wizara, *ZAWA* wakiihitajia basi nipo tayari nitoke nikawape benki.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu inachopata ndio inachotumia, lakini tukikaa humu tutaanza kusema na kujenga vitu ambavyo tutakuwa hatufanyi kitu. Tatizo la mashine kama lipo mashine moja haizidi milioni 15, kwa hivyo hii karibu mashine 17. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya familia yangu, kampuni yangu naona nitangulize kutoa pesa hizi zisizokuwa na riba, masharti, wala chochote, ikisha Ramadhan nirejeshewe. Naomba niwasilishe mbele yenu kupitia Mhe. Waziri barua hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kama kawaida yetu mimi nimuunge mkono Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magufuli kwa hatua alizochukua pamoja kwa kushirikiana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, kushirikiana na Serikali ya Zanzibar katika kutizama usajili wa meli zetu zote za Bara na Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, unapoita Tanzania, maana yake Zanzibar na Tanganyika unaita Tanzania lazima heshima ya ulimwengu ibakie. Hatua aliyochukua Rais John Pombe Magufuli na akawepo shahidi Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Ali Abeid Amani Karume siku ile kwa kuona hizi meli zisajiliwe, zitizamwe halafu tuchukue hatua. Lakini nataka kuiambia serikali niombe hii *ZMA*, serikali imefaidika katika usajili, serikali imefaidika mamilioni mangapi, pesa ngapi serikali imefaidika kwa mradi huu wa *ZMA* waje watwambie humu ndani.

Hilo Mheshimiwa naona ni changamoto lakini namuunga sana mkono Rais John Pombe Magufuli pamoja na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambaye alikuwa mkono wake wa kulia kwamba Zanzibar ilishirikishwa kikamilifu. Sio kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ilikuwa ni kauli ya serikali mbili.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili sisi sote hapa Wawakilishi tunapaswa kulinda maslahi ya serikali, kuisemea serikali na

kulinda Katiba ya Viongozi wetu wastaafu. Mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano na kabla sijapata taarifa hii *ZECO* walitoa taarifa kwamba katika watu wanaodaiwa umeme ambao ni sugu, naomba Wawakilishi hili mnisaidie. Wawakilishi sugu wanaodaiwa Shirika la Umeme ikapata madeni ni Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Salmin Amour Juma na Rais Amani Abeid Karume.

Mhe. Mwenyekiti, nilichokifanya baada ya usambazaji wa waandishi wa habari kupata jambo hili mimi kama mwananchi kwa sababu ni kiongozi. Mhe. Mwenyekiti, japo unanitizama mimi kama Mohammedraza lakini nina ukoplo humu ndani, ndio maana nikakaa, ndio maana nikawepo ndani ya Baraza la Wawakilishi. Nilichokifanya nilikwenda *ZECO* kutaka kujua uhalali wa wadaiwa sugu, nikaambiwa kwamba Dkt. Salmin Amour Juma, Rais mstaafu yumo ndani ya katiba anadaiwa milioni mbili laki nane na Dkt. Amani Abeid Karume anadaiwa laki sita arubaini na sita. Nikawaambia nipeni risiti nikiwa kama mzalendo ninaipenda nchi yangu hao viongozi wamo ndani ya katiba, baba zangu, nikawalipia bili hizi zote ambazo nitawasilisha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kilichonisikitisha nikamuandikia barua Katibu Mkuu Kiongozi, Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee kumuelezea kadhia hii na nikamwambia sio kama nataka kurejeshewa pesa zangu, sio kama nataka kudai pesa zangu ila kumpa taarifa tu kwa kadhia hii iliyotokea kwa sababu hawa viongozi wamo ndani ya katiba.

Mhe. Mwenyekiti, Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu Mkuu Kiongozi alinijibu mimi hivi. “Wewe umejifurahisha tu kwenda kulipa”. Amenijibu maneno ya kifedhuli kwenye barua. Nimefanya kwa uchungu wa nchi yangu, mimi sina mti wa kuchuma pesa, lakini hawa ni viongozi wenzangu nina uchungu

na nchi. Dkt. Ali Mohamed Shein, huyu Balozi Makamu wa Pili wa Rais alikuwepo kwa Dkt. Salmin Amour Juma juzi Jumatatu nyumbani kwake. Viongozi wetu hawa Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa mstari wa mbele, sasa ndio hofu ingelikuwa sijalipa mheshimiwa hujafa hujaumbika. Awamu ya Sita hii ya CCM ilimzimia taa Dkt. Salmin Amour ikamnyang'anya magari, hii hii Awamu wa Sita ya CCM, kwa hivyo nikahofia wasije wakawazimia taa viongozi wetu hawa wamo ndani ya katiba, namuandikia barua Katibu Mkuu Kiongozi ananijibu hivyo, eti umependa mwenyewe kwenda kufanya.

Kwa bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, mimi Mjumbe katika ripoti hiyo majina yao yamo wanaodaiwa sugu, Mhe. Hamza Hassan Juma bosi wangu huyu hapa, hujafa hujaumbika. Mimi nafikiri Rais lazima tuwe wakweli. Ninachotaka kuzungumza kwamba hii nchi ni yetu sisi sote, nimuombe Dokta kwa hili asinione mimi Mohammedraza kama Raza tu mhindi, mimi nina ukoplo hapa nyuma, asinione tu kwa sababu ya ubaguzi. Mimi naomba nyaraka hizi zote niziwasilishe mbele yako, seti kumi naomba zipeleke nilizokuwa nimezilipia na barua hii hapa niliyokuwa nimejibiwa ziwe kama kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, kazi yetu kubwa sisi Baraza la Wawakilishi ni kusimamia Sera ya Chama lakini na kusimamia viongozi wetu. Kama nilivyosema Awamu wa Sita ya CCM Dkt. Moh'd Gharib Bilal akiwa Waziri Kiongozi kule Pemba, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Kassim Tindwa, walimzuia mpaka magari asiende kupokelewa, mimi nilikuwepo kwenye msafara kwenda kufungua msikiti. Lazima tuwe wakweli unapopata jambo pima, unapopata jambo pita, halafu ndio utumie wino.

Mhe. Mwenyekiti, bado nina uchungu na nchi nitaendelea kuisaidia serikali yangu kwa hali na mali, nipo tayari hata kuuza majumba yangu lakini nchi yetu iende mbele. Dkt. Ali Mohamed

Shein nitamuunga mkono kwa kazi zake kubwa anazozifanya sitorudi nyuma, sitovunjwa moyo, nitaisaidia nchi yangu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nishukuru vituo vyetu hivi vya *ZAA*, Idara ya Barabara, *ZECO* kwa usambazaji wa umeme. Mhe. Mwenyekiti (Mhe. Hamza Hassan Juma) alisema tatizo la barabara ni nyenzo za kufanyia kazi, mashine, hali ya fedha, ukija kwenye *ZECO transformer* na mambo mengi mengineyo. Kwa hivyo, hata *transformer* na mambo mengineyo *ZAWA* wana changamoto yao pale, bajeti yao inabidi. Nazipongeza taasisi zote zilizokuwa na wizara mbili hizi zinazohusika kwa kazi yao kubwa na kwa uzalendo, lakini niombe tu taasisi zote hizi panapotokea na hitilafu wananchi wapewe taarifa katika sehemu zao, iwe maji, iwe barabara, iwe umeme. Mategemeo yangu tutaendelea kuisaidia nchi yetu na mimi napongeza kwa dhati kabisa na mambo yote haya na kama kuna changamoto nyengine yoyote basi niletewe tusaidiane ili kujenga nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache nawashukuru Mawaziri wote, Makatibu Wakuu wote, Manaibu Makatibu Wakuu wote na viongozi wote kwa kazi kubwa wanayoifanya kiuzalendo, wamekuwa wasikivu, kazi yetu ni kutafuta bajeti ya kuweza kusaidia. Nashukuru sana na ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali, sasa namwita Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) akifuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia machache sana kwa Wizara zetu mbili hizi. Kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Makamo Mwenyekiti na Kamati nzima kwa jumla na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya

katika upembuzi wao wa mambo mbali mbali juu ya maendeleo ya nchi yetu.

Pili Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara mbili, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wengine wote wa Wizara hizo kwa kazi zao nzuri wanazozifanya ambazo zinatupa maisha ya siku hadi siku. Mimi niseme tu kwamba nataka kutoa historia kwa ufupi sana.

Mhe. Mwenyekiti, mara baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 Marehemu Mzee wetu Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wetu wa Kwanza, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema yeye na wenzake wote waliotangulia mbele ya haki ambao wametuwezesha kusimama mbele ya Baraza hili. Mhe. Mwenyekiti, Mzee Karume alisema mambo matatu muhimu, kwanza elimu bure, pili afya bure na tatu maji bure wananchi watumie wanavyotaka. Kwa bahati nzuri yameendelezwa na Mhe. Rais wetu wa Awamu ya Saba Dkt. Ali Mohamed Shein ameyakariri hayo na anaendelea kuyafanya kama yalivyotokea huko nyuma. Kwa mfano anaendeleza kwa juhudi zake zote mambo ya afya, mambo ya elimu bure, lakini na maji tumekubali matokeo kwa sababu wakati unabadilika.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 1964 wakati wa Mapinduzi Zanzibar kulikuwa na watu laki tatu kama na sitini au na sabini, sasa hivi 2018 tupo watu milioni moja laki tano na inaendelea. Kwa hivyo, tuseme kwamba harakati zimeendelea na maisha yameongezeka ya watu, mahitaji ya maji yanapungua. Mimi wazo langu liko hapa, kilio kikubwa kama alivyosema Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali nampongeza ingawa kaikopesha *ZAWA* shilingi milioni mia mbili, nasema si haba lakini hazikidhi haja. Mimi katika jimbo langu la Kijitoupele peke yangu nina visima

vyangu vinne na visima hivyo ili vikamilike nahitaji kama milioni mia sita na zaidi.

Nitatoa tathmini nina kisima cha *ZAWA* Magirisi kinataka shilingi milioni 47,600,000 nazitoa kichwani kwa mawazo yangu. Kuna kisima cha Kijitoupele Mashine ya Maji kipya hakijatumika kinahitaji shilingi milioni 63. Kuna kisima cha Ras al Khaimah ambacho kinaendelea Tomondo Maduka Saba kinataka shilingi milioni 57 na kuna kisima chengine cha Kwarara Kandahar katika taarifa iliyopita kinatakiwa shilingi milioni kama 56. Kwa hivyo, shilingi milioni 200 peke yangu hazinitoshi. Lakini najua kutoa alichonacho sio mbaya kutia changamoto katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema tu kwamba kwanza naipongeza Wizara hii lakini naanza na Wizara ya Maji, mimi sina chengine nitakachochangia isipokuwa maji. Maji ni uhai wa viumbe vyote, bila ya maji hatuna maisha. Kwa hivyo, adha hii imekuwa kubwa ya muda mrefu nampongeza Mhe. Waziri kwa juhudi yake lakini pia nitatoa taarifa hapa kidogo imenifurahisha.

Niliwahi kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa Maji tukaparurana siku za mwanzo lakini likatokea tukio nikenda tena kwa mtihani mwengine kanipokea mikono miwili hili nampongeza kwa dhati. Sina tabia ya kumdharau mtu kwa wema wake, lakini nina tabia ya kumchukia mtu kwa ubaya wake. Kanipokea vizuri, tumekwenda vizuri na zile changamoto nilizoziendea nashukuru wasaidizi wake tumekwenda hadi tumefanikiwa kwa asilimia kiasi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii kuna visima 150 vya Ras al Khaimah hili suala zito na linaturudisha nyuma hatujui tuanzie wapi. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri hebu tuvimalize visima hivi kwanza, vipatiwe *pump* vyote, vipatiwe umeme ili

tuhakikishe kwamba wapi tumemalizia na tumefanikiwa kiasi gani. Tukimaliza visima hivi tumefanikiwa vizuri tunaona mahitaji yake kwa wananchi hatukufanikiwa tutachimba visiwa vyengine, lakini mimi siridhiki hata siku moja kwamba kila siku kuchimba visima tu wakati hivi vya mwanzo umeviacha. Mheshimiwa mimi nina visima vipya vinne katika jimbo langu kama kisima cha Magirisi au Taveta kitapatiwa huduma yote umeme na mabomba leo basi nasema kwa maeneo makubwa katika jimbo langu Meli Nne Uzi huko Taveta wenyewe, Kwarara na kwengineko mpaka Kijitoupele tatizo la maji litaondoka na bei yake nilisema inatakiwa shilingi milioni 47 kama sikosei.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna kisima cha Tomondo Maduka Saba hili linanisikitisha sana Mamlaka ya Maji wanaendeleza kutelekeza kisima hicho ili watu wapate maji, lakini kuna kisima cha asili hapo hapo maji yake huko nyuma tunakotoka yalikuwa yanapelekwa mote kuanzia Kwarara Maduka Sita mpaka huko Kwarara Tomondo. Lakini kwa babati mbaya katika utekelezaji wake ulikuja yale maji yakabadilishwa yakaelekezwa Tomondo mpaka leo, lakini leo hicho kisima cha Ras al Khaimah Maduka Saba maji yake yameelekezwa Tomondo huko huko huku watu hawapati maji.

Namuomba sana Mhe. Waziri na Mkurugenzi yupo hapa na wasaidizi wake tukimaliza Baraza tufanye ziara mambo ya ofisini tuyaache kwa sababu maji ni huduma muhimu kwa wananchi wetu. Lakini iwe na muelekeo wa kupatikana kwa watu wote, wananchi wapo tayari igaiwe kwa zamu leo iwe siku mbili huku halafu ielekeze huku siku mbili watu watajaza katika madumu yao na mambo mengineyo. Namuomba Mhe. Waziri kisima hiki cha Tomondo Maduka Saba kwa kuwa tuna kisima cha asili kinaelekeza maji huko huko Tomondo kifanyiwe marekebisho yaelekezwe Maduka Saba na kuendelea wananchi wakapate maji na huko wastirike na Ramadhan kesho kutwa.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, napongeza kisima cha Kijitoupele ambacho tunaita Mashine ya Maji kisima kikuu kile kinasaidia sana jamii Pangawe, Kijitoupele na kwengineko. Lakini bahati mbaya tumekwenda katika jitihada yetu yote kubwa ya kufanya nampongeza Mkurugenzi, mpaka ndugu yangu Maulid nampongeza sana na wafanyakazi wake, maana la kweli mtu mpe wamejitahidi lakini hadi kufikia leo maji hayapatikani. Naomba kile kisima kipya ambacho kipo hapo hapo hakijatumika toka kimeanzishwa kisima kile mpaka leo kimekaa tu kiunganishwe mipira wapelekewe wananchi wetu wa Kijitoupele sehemu ya Mzee Takrima na kwengineko tutapata faida kubwa sana kwa wananchi wetu na hii sio kwamba kelele za maji zitapungua.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niseme tu visima vyetu vyote mpaka kule Kwarara Kandahar nako kuna kisima kimekaa tu visima vinne hivyo kama tutafanikiwa nasema tatizo la maji litaondoka. Nimuombe sana Mhe. Waziri, nampongeza kwa juhudi yake tunakwenda mbio pamoja wakati mwengine lakini wakurugenzi na watendaji wengine wapo bega kwa bega kutuunga mkono, tunapokwenda tufuatane kwa sababu sisi maeneo tunayajua na shida za watu wanajua sisi ndio wasemaji wao na wafuatiliaji wa kila siku katika shida zao hizo za maji.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba mimi kilio changu nasema maji, mambo ya ardhi, mambo ya nini wala sina habari nayo, wenye matatizo ya ardhi watasema wao mimi tatizo langu maji. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri maji.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti kwa kamati yake na rai aliyoitoa lakini visima vyetu vya maji vinahitaji huduma ya umeme na bila ya huduma ya umeme maji hayapatikani. Kwa hivyo, niwaombe sana *ZECO* kwanza nawapongeza kwa dhati kabisa kwa asilimia mia moja zaidi kwa kazi nzuri

wanazozifanya, ikitokea hitilafu ya umeme, pakikatika nguzo ukipiga simu hata saa saba za usiku *standby* wanakuja bila ya matatizo. Kweli tuwapongeze na tuwasaidie kwa hali na mali lakini wana mzigo mzito, mimi nimepiga hesabu hapa kwa ufupi tu wanadai taasisi mbali mbali, ukienda kwenye *ZAWA* shilingi bilioni 12 na taasisi nyengine hizo za serikali shilingi bilioni moja, taasisi za Serikali ya Muungano wa Tanzania shilingi bilioni moja na hapa pana shilingi bilioni 15 kwa Unguja.

Ukiunganisha na Pemba *ZAWA* wanadaiwa shilingi bilioni moja nukta saba, Wizara ya Afya shilingi milioni 73, ukienda taasisi nyenginezo za SMZ shilingi bilioni 2.6, jumla nimezichukua hapa wanadai shilingi bilioni kumi na tisa, mia nane kumi na nane milioni, arubaini na tano elfu, mia tatu arubaini na tano na senti sitini na tano. Narudia tena *ZAWA* ili waendelee vizuri ahlan hawa *ZECO* walipe pesa zao hizi bilioni kumi na tisa, mia nane kumi na nane milioni, arubaini na tano elfu, mia tatu arubaini na tano na senti sitini na tano. Mheshimiwa hii changamoto kubwa wenzetu wanafanya kazi nzito na wanakwenda mbio usiku na mchana hawalali *ZECO*. Nasema tu kwamba ili wapate fedha hizi walete huduma zaidi ma-*transformer* tunayo na mapya yanafungwa maeneo mbali mbali, ukiwapigia simu nguzo imekatika wameshafika. Kwa hivyo, ningeomba serikali kupitia taasisi hizi ifanyiwe mpango zipate pesa zao ili kuendeleza shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitalozungumza hapa kwa ufupi ni suala la Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji nawapongeza kwa dhati kabisa tena nawapongeza kwa kazi zao nao nzuri. Lakini kama watu walivyotangulia kusema mpaka taarifa ya kamati naipongeza kwa dhati kwamba wapatiwe nyenzo za kufanyia kazi. Nimetoa mfano Mhe. Mwenyekiti, walijenga barabara yetu ya Kwarara ingawa sasa naiomba tena wizara hapa na wananchi wangu wananisikia kwamba barabara ili idumu vile kuwekewa katika barabara zetu hujengwa kingo za kuzuia angalau

usalama zisivunjike. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili liangaliwe.

Barabara zimejengwa mabilioni kuta hazitofika hata milioni mia moja. Kwa hiyo, tutafute rai hiyo milioni mia mbili tunusuru barabara zetu siku ya mvua kwa sababu mara nyingi ikija mvua huwa zinachimbuka pembeni na zinakufa upesi. Ndio maana barabara zetu ukipita na gari yako utakuta pembeni kama kuna misumeno ile michubuko, lakini palipojengewa kingo barabara zipo salama.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, ili twende vizuri tuseme tu kwamba dunia leo imebadilika, dunia ndio hii hii wananchi wake wamebadilika kila mmoja ana tabia yake, kuna majambazi, kuna wahujumu wa uchumi wa nchi zetu na wengineo. Lakini niseme tu kwamba tunaposafiri kwenda Dar es Salaam na unapotokea Dar es Salaam kuja Zanzibar unasachiwa Bandarini na Uwanja wa Ndege, lakini unaposafiri kwenda Pemba kwa Uwanja wa Ndege unasachiwa kama kawaida unapotoka kule. Naunga mkono.

Narudia tena naiomba serikali kupitia Shirika la Bandari sasa hivi tubadilike lazima pawe na vyombo vya kuwapekua wananchi wanaotoka Pemba kuja Unguja na wanaotoka Unguja kwenda Pemba. Hizo bangi, madawa ya kulevya nasikia Pemba yamekamatwa tele yamepitia bandarini, kwa hivyo mimi ushauri wangu huo dunia ndio hii hii watu wake wamebadilika. Kwa hivyo, hii natoa ushauri kwa kamati hili pia mliangalie kwa sababu utasikia leo mtu anakamatwa Pemba ndani ya gunia mwanamke na yale mabaibui wanayaita ya bamita sijui nini, mashekhe wa uwongo, maana yake kaja kavaa baibui kumbe kajaza makete tele ndani ya mwili wake. Kwa hivyo ni hatari Mhe. Mwenyekiti, naomba hilo liangaliwe.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa una dakika moja, nakupa dakika moja umalizie.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Haya Mhe. Mwenyekiti, namalizia nasema jengine kwa ufupi dakika moja nisaidie Mheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti, *ZURA* ni chombo muhimu sana na wananchi wameshakizowea kusikiliza bei za mafuta. Lakini hii *ZURA* kwenye maji inatusaidia nini, maana hii imeambiwa *ZURA* ni sehemu ya kupatikana sijui mafuta leo bei fulani, sina tatizo ndio ulimwengu, lakini tuna shida za maji katika maeneo yetu wamefika lini katika maeneo kutusaidia kuwauliza wananchi wana shida za maji. Kwa hivyo, mimi kazi za *ZURA* sizifahamu wala hazina tija yoyote kwa wananchi wetu, kwa sababu kwenye mafuta najua tija ile ikipatikana na wao asilimia yao inapatikana, kwenye maji hawakemei wala hawafuatilii wala hawajui lolote.

Mimi naomba huu ushauri kama kweli *ZURA* inasimamia jamii kwenye maji na mafuta basi ije katika maeneo yetu ituangalie na iwaangalie wananchi wetu wanapata shida. Kwa hivyo, Mheshimiwa baada ya hayo ombi langu liko pale pale maji mengineyo yatakuja baadae.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naiunga mkono ripoti hii na nampongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Wajumbe wote pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara zetu mbili kwa kazi nzuri wanayofanya. Tushirikiane tupate maendeleo. Naunga mkono wa asilima mia moja ahsante mheshimiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, sasa namwita Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akifuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajitayarishe.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona naomba nichangie Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Kwanza, niipongeze kabisa kamati hii hasa kwa Mwenyekiti wake mzoefu Mhe. Hamza Hassan Juma kwa alivyoeleza changamoto zake vizuri na za uwazi katika kamati hizi. Lakini pia niwapongeze sana wote kwenye kamati hii ambao wanashirikiana kumsaidia Mhe. Hamza. Vile vile, niipongeze wizara kwa ujumla kwa jitihada zao wanazozifanya, lakini nitatoa michango yangu ambayo nahisi haya yanataka kutekelezwa au kutoa ushauri ili yakaangaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia wizara zote mbili lakini kwa pamoja kwa mambo tofauti nitakapoyataja nitaanza na suala la maji. Mhe. Mwenyekiti, hapa Zanzibar bado suala la maji halipo vizuri nikimaanisha Unguja na Pemba. Taarifa zinazotoka kwamba sijui maji labda Zanzibar tunapata asilimia themanini tumeshafika sijui ngapi. Kwa kweli, takwimu ile sio sahihi, ukiangalia Zanzibar nzima kila kona sio jimbo langu tu majimbo yote maji watu hawapati. Watu wenye uwezo wao wenye visima vyao na baadhi ya sehemu maji wanapata. Lakini ukichukulia sasa *population* yetu tunaofaidika na maji ni kidogo, lakini katika *percentage wise* wanazozitoa wao hazipo sahihi, sio za ukweli. Leo ukiangalia Unguja nzima na Pemba sio Michenzani, Malindi, wala Mji Mkongwe kama sio watu wenye visima binafsi wanaopeleka mabomba basi ingekuwa hatari.

Mhe. Mwenyekiti, jimboni kwangu halikadhalika Kikobweni hawajawahi kuona hata mabomba ya maji tokea wamezaliwa watu wazima mpaka wanatarajia kufa wengine. Halikadhalika sehemu tofauti za kwenye jimbo langu maji ni tatizo. Ningeomba wizara husika hebu wawe wakweli wasitoe tu takwimu za uwongo kubabaisha watu, maji hakuna Unguja, maji kidogo sana, *population* tunayopata maji ni watu kidogo. Mhe. Mwenyekiti, kwa *research* yangu mimi naweza kusema labda watu wanapata

asilimia thelathini na tano Unguja na Pemba mpaka arubaini lakini hatujafikia awamu ya kusema tumefikia asilimia sitini wasipotoshe viongozi wa kitaifa wanapokwenda kuwapa ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya maji Zanzibar haipo vizuri sio kweli watu hawapati maji maeneo yote na hapa kama kuna mwakilishi mmoja kama wenye majimbo hamsini na nne ya Unguja na Pemba atasema kwamba jimbo lake kila sehemu wanapata maji nitakubaliana nae, hakuna. Sehemu chache sana hata kwenye majimbo yao yanayotoka maji. Lakini nizungumzie suala hilo la maji ni muhimu wanaochimba visima *private* haina haja sasa ya kuwalipisha, ilitakiwa wizara wapeleke dawa kwa ajili ya kusaidia. Lakini sio tena masuala ya kulipia mtu kachimba mwenyewe, fedha zake mwenyewe halafu wanalipishwa hiki kitu hakiwezekani. Lazima tuangalie hali ya nchi iko vipi kuchimba kisima fedha nyingi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwenye suala la umeme, ukiangalia wizara husika na kazi yao kupeleka umeme vijijini kwa sababu wao ndio wanaopata zile pesa na kodi. Katika risiti ya umeme kuna mpaka *infra structure* ile *tax* kitu kama hiki ambayo unaponunua umeme mtu wa kawaida unachangia. Sasa leo wizara mtu anaenda kuomba anataka nguzo mbili au moja bili yake milioni tatu, nguzo moja kupeleka na waya bili yake milioni moja laki saba, lakini mwisho wa siku wao wao ndio wanaochukua fedha. Kwa nini kama wanataka wananchi walipie vile na umeme wasiwape bure, dunia nzima ni wajibu wao shirika kupeleka kwa pesa zao wenyewe na sio za wananchi.

Hivi mwananchi mnyonge hana hata kazi wapo vijijini nyumba hana ukamtoleshe milioni moja laki saba, milioni mbili mpaka milioni nne. Nina ushahidi, nina risiti karibu saba za jimboni wananchi maskini nguzo moja tu kuvuta pamoja na waya

wanaandikiwa bili milioni moja laki nne, nguzo mbili milioni tatu laki sita, huu ni wizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naongea hapa kwa niaba ya wananchi wote wa Unguja na Pemba, haiwezekani wananchi wadhalilishwe ni wajibu wao wizara wapeleke nguzo, wapeleke waya kuvuta umeme tutalipa sisi na umeme tunaotumia sio mpaka nguzo na waya tulipishwe sisi wakati shirika lipo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la ardhi Zanzibar tunayo nzuri. Lakini niombe wizara wanapotaka kuja kuwafutia watu ardhi, basi wahakikishe wanawafutia watu wote wanaohusika kufutiwa ardhi, wasije wakaja wakabagua wakawaachilia viongozi ambao wameweka maeneo hawajayafanyia *investment,* wakawaachia wakaenda kuwafutia watu binafsi wanawaonea. Sisi tunajua mmoja mmoja kiongozi gani na gani anamiliki ardhi kubwa ndani ya nchi hii ambayo haja-*invest.* Katika ufutaji wao wawe makini lazima watende haki, atakapofutiwa mtu wa *private* ambaye haja-*invest* basi afutiwe na yule ambaye kama yuko serikalini au mtu yeyote ana umarufu na hasa wenye maeneo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wamehodhi *square* metre elfu kumi, elfu themanini mpaka laki moja hawajafanya *investment* yoyote. Sasa naomba haki ije itendeke, lakini kwenye masuala ya waraka akahakikishe Mhe. Waziri atatoa *title deed* kuwapa wananchi. Wananchi hawawezi hivi sasa uwezo wa kwenda kuchukua mawaraka kwenda kulipia kwa mujibu wa nyumba, watoe serikali sasa hivi bure masuala ya waraka kwa sababu yale ni makaratasi tu na kusaini sio labda kwamba kuna masuala ya *payment.* Leo atakuja kuambiwa mtu maskini akalipe sijui *percent* ngapi apewe waraka.

Hapa Zanzibar asilimia tisini na tano watu hawana waraka wa nyumba wala viwanja Unguja, hakuna watu wenye *title deed* hapa na kama kuna mtu atanibishia mwache ainuke anibishie. Watu wenye vitu hivyo ni watu wenye uwezo wachache tu lakini maskini wote hawana *title deed* ya moja kwa moja, wana karatasi ya Sheha, karatasi ya Halmashauri, kikubwa nacho *certificate transfer*, *certificate* wizara. Ningeomba masuala haya yafanywe bure wasiwatie wananchi kwenye vikwazo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la sekta ya baharini. Sekta ya baharini najiuliza siku zote kuna watu binafsi wana meli kumi kumi akiwemo Bakhresa mbona haziharibiki, meli ya Zanzibar kwa nini imeharibika. Hebu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji watupe ukweli nini kumefanyika, kuna mtu anafanya makusudi kuiharibu ile meli au meli mbovu tuelezwe. Lakini meli za Bakhresa hapa zipo ndogo kuliko yetu sisi ghali zaidi na zake yeye zinafanya kazi kila siku anatengeneza pesa, kwa nini ya serikali ile hasara. Ukweli uko wapi wa meli hii hebu tuelezeni wananchi wanapata tabu kwa sababu ile meli ya serikali ni meli ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye suala la viwanja vya ndege, nimpongeze mkurugenzi wa masuala hayo, simjui lakini anakwenda vizuri. Ninachoomba kwamba pale aweke watu wa kuweza kuwasaidia wageni mizigo, kuna watu wagonjwa wa migongo, wagonjwa wa maradhi, watu wazima wanabebeshwa, wakati wa ku-*check in* wanafika anaambiwa abebe begi mwenyewe kilo 30 au 40 ataliweza wapi mtu mzima. Wawekwe watu wa kusaidia wageni wote pale walipwe na serikali. Zipo nchi ambazo zimeweka watu *private* unalipia unasaidiwa. Lakini je, kama mtu hana fedha za kulipa. Serikali iweke watu kwa kupitia Uwanja wa Ndege mambo yaendelee vizuri. Huo Uwanja wa Ndege mpya tunausubiri sitaki kuzungumzia nasikia mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye majenzi. Niliwahi kuzungumza siku za nyuma kwamba kuna watu wametapeliwa kwenye Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Katika masuala ya nyumba walizokuwa wakinunua kuna watendaji ndani ya wizara wamewatapeli watu. Kwa hivyo, naishauri wizara wawarejeshee nyumba zao wale waliotapeliwa na wanawajua wengine ni nani na nani. Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri ameshawahi kukiri kama kweli taarifa hizo wanazo sio tatu wala nne watu waliotapeliwa kwa njia ya uongo. Sasa ningeiomba wizara yako watu wale wawarejeshee wasidhulumiwe wameshatumia pesa zao.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye masuala ya barabara. Mimi nimpongeze Mhe. Rais kwa barabara yangu pamoja na watu wote wa jimboni mpaka Mkokotoni na majimbo mengine inajengwa. Lakini hali iliyokuwepo sasa hivi sio nzuri wafanye utaratibu wa kutia angalau rojo la lami ili njia zipitike, kwani mavumbi kwenye Jimbo langu la Chaani yameshauwa watu macho, kifua, pumu, wazee wanaumia wameshanituma mara nyingi kuja kuzungumza watilieni rojo msiwatilie kifusi tutawaumiza macho na vifua wanyonge wale hawana pesa za kwenda kutibiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda kwenye suala la daladala, ningeiomba wizara nimeshaishauri sana wawawekee *speed limit* wenye daladala wendawazimu wanauwa watu kwa shilingi mia tatu, wanashindana wanakwenda *speed* mia na arubaini, kwa nini msiwatilie mashine mwisho *speed* 60 kwenye daladala. Mhe. Mwenyekiti, nchi za wenzetu zipo *control* ambazo unatia kwenye gari inakuwa *speed* haiwezi kuvuka zaidi ya uliyopangiwa, na ukizidisha ukienda kuichomoa ina-*dictate* kwenye wizara, kwa nini wizara hii ishindwe hata iwalipishe wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali nimemsikia wakati nipo kwenye redio nakuja kwa kusaidia fedha kwa njia ya mkopo bila ya riba. Ni suala zuri japokuwa kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali ni kidogo, lakini si kidogo milioni mia mbili kujitolea mtu kwa miezi minne ange-*invest* kwenye biashara zake angepata mapato. Lakini inanisikitisha sana kusikia kwamba kaenda kulipia umeme kwa viongozi wa kitaifa kwa imani yake halafu anatokea kiongozi mwengine kwa njia ya maandishi anamjibu ujeuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Katibu Kiongozi simjui wala simfahamu, lakini kwa suala hili kama ni kweli kalifanya huyu Katibu Mkuu Kiongozi, basi hili suala la kulaaniwa. Haiwezekani tukaona viongozi ndani ya nchi hii wanajibu maneno ambayo ya kashfa kwenye barua tena *official* yule kama kafanya kwa imani yake na kama alivyotoa mifano huko nyuma kwenye serikali iliyopita viongozi wale walizimiwa umeme na ni kweli. Umeme alikatiwa Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma, leo kaingia imani kaona yasijekuwa yale yale watu wakaja wakajisahau lakini kwa serikali ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein nafahamu haiwezi kufanya hivyo, kwa imani yake akaona akalipie.

Leo anakuja kujibiwa ametaka sifa, amejifurahisha, amejifurahisha nani? Mimi ningeomba kwamba sisi sote viongozi hakuna kiongozi hata mmoja aliyekuwa juu isipokuwa Mwenyezi Mungu, hapa tutaheshimiana, tunamheshimu Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Rais waliobakia wote wafahamu *level* yetu ni moja na sisi wengine pia ni wakubwa, sisi tupo kwa niaba ya wananchi, wao wengine kama kuna mtu kateuliwa basi ajifahamu yeye kateuliwa. Sisi tumechaguliwa na wananchi hawezi mtu akatutambia tambia tu akaleta ubaguzi, akaleta maneno ya kashfa tena kwa kujiamini kupitia barua inayotoka Ikulu, hicho kitu hakipendezi.

Kwa hiyo, ningemuomba Mhe. Rais na busara zake awaambie viongozi kuna mambo mengine hayafai, angemjibu kwa hekima ingekuwa nini. Haya mambo kwa kweli hayapendezi, nasema tena sisi tunayemuabudu, tunayemuogopa ni Mwenyezi Mungu. Tunafahamu tuna viongozi wa nchi Mhe. Rais wetu tunampenda sana wa Zanzibar, Makamu wa Rais pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano na wengine wote, lakini kiongozi mwengine yeyote atakapokosea hapa tutakuja kuambizana *live and clear* hakuna kufichana, wakati wa kuogopana, wakati wa kusema mtu anyanyaswe atolewe maneno umekwisha. Viongozi wa kitaifa tuna hekima nao, tunawapenda wanafanya kazi vizuri lakini watendaji wao ndio tunazungumza mara nyingi baadhi yao wanaharibu na hali ndio tunaiona kama hii mfano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kuzungumza sana kwa sababu nimesema simjui wala sitaki kumjua. Nashukuru sana ripoti ya Mhe. Hamza Hassan Juma hii hapa nai-*support* asilimia mia moja. Nawataka mawaziri wote wa wizara mbili wafanye kazi zao vizuri mambo yaende vizuri, wananchi wafaidike waone matunda ya nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante na wewe nakushukuru pia, sasa namwita Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajitayarishe akifuatiwa na Mhe. Masoud Abrahman Masoud ajitayarishe.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, maana yake unapokuja baada ya Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf anakuwa ameshapiga vigongo vyake vikali halafu unafuata wewe sijui unaanzia wapi, lakini nimpongeze ndio katoa mawazo yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu. Lakini pia nichukue nafasi kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe.

Hamza Hassan Juma pamoja na wajumbe wake wote wa kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia sifa ziende kwa uongozi wote wa wizara zote mbili husika kwa jinsi gani wametoa mashirikiano mazuri, naona kila siku zikienda ripoti inayotoka nyengine, inakuja nyengine inakuwa bora zaidi. Jana ilikuwa ripoti ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame ilikuwa nzuri, sasa leo naona Mhe. Hamza ripoti yake imeifunika ile, kwa hiyo hongereni sana. Kesho inakuja ripoti ya Mhe. Miraji Khamis Mussa na wajumbe wake naamini itazidi kuwa nzuri zaidi, na naamini hivi ndio inavyotakiwa Baraza letu kuleta ripoti ambazo zitaweza kuishauri serikali kwa niaba ya wananchi ili tuweze kuleta tija kwa pamoja sote na katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tunguu nikiwa mtetezi na msemaji wao hapa, ili niweze kuchangia ripoti hii. Moja, nitajaribu kuchangia kwa mujibu wa kutoa mawazo kwa nchi na mimi pia nitagusia jimbo langu juu ya changamoto ambazo nilizokuwa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza na suala la umeme. Kwanza nataka nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hasa kwa maelekezo yake aliyoyatoa katika *ZECO* pamoja na wizara husika kuhakikisha kwamba deni ambalo tunadaiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano linaweza kukamilishwa au kulipwa, pia tuweze kwenda sambamba juu ya mahitaji yetu na kuweza kujipangia. Kwa hiyo, nampongeza sana Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba nawapongeza sana *ZECO* kwa kazi nzuri hasa kupeleka umeme katika visiwa kama cha Fundo, ni jambo zuri sana kwa sababu ukiangalia miaka nenda miaka rudi ndugu zetu kule walikuwa wanapata tabu, sasa naamini vijana wetu watakuwa wanapata nafasi ya kusoma, pia wananchi watatumia nishati hii ya umeme ili kujipatia kipato.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri nikiamini kwamba Mkurugenzi wa *ZECO* na watu wao husika wapo juu wananisikia. Napenda kukumbushia *issue* ya Kikungwi kule Uwandani Mhe. Waziri mwaka jana nilizungumza na watu wa *ZECO* waliniahidi kwamba watakwenda. Hivi karibuni nimechapwa kwenye Mawio nikaambiwa kwamba bado hii kazi haijakamilika. Kwa hiyo, nakuomba sana Mhe. Waziri suala la Kikungwi kama ndio ulivyonambia mwaka jana, basi mwaka huu angalau ile kazi ianze kwa kupelekewa zile nguzo na sisi pia tutachangia mawazo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nigusie juu ya masuala ya maji safi. Tulifanya ziara mwaka jana mwanzo mwanzo nafikiri na Naibu Waziri kwa niaba yako Mhe. Waziri tulizunguka katika Jimbo la Tunguu maeneo yote ambayo tuna visima tofauti. Nikushukuru sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira katika *issue* ya Kibele ulipeleka watu wako kunisaidia, lakini bado changamoto tunayo katika *tank* la maji la Unguja Ukuu linavuja vibaya mno, gharama zake ni kubwa zinahitaji nguvu ya serikali ili kuweza kulitatua tatizo lile ili maji yaweze kupata nguvu na kasi kufika mpaka katika kijiji cha Ng'ambwa kilichopo katika kisiwa cha Uzi. Kwa bahati mbaya au nzuri katika Jimbo langu la Tunguu eneo la Ng'ambwa halikulingana na kisiwa cha Uzi kila unapochimba kisima wanapata chumvi na katika watu ambao wapo katika hali duni sana na mazingira yao ni magumu, na kama nilivyosema mawaziri wengi bado hawajafika kule kwenda kujionea. Mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri uweze kwenda katika kijiji cha Ng'ambwa kwenye kisiwa cha Uzi ili ukajionee mwenyewe hali halisi ilivyo na tuweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwenye suala la maji katika eneo la Ubago tuna changamoto pia hasa kuhusiana na *pump*. Tunaiomba sana wizara yako kwa kushirikiana pamoja na wapiganaji wetu

tuangalie utaratibu ambao tutashirikiana pamoja na *ZAWA* kuhakikisha kwamba maji ambayo yanapatikana katika maeneo yale kwenye kambi zetu za jeshi tunaweza tukafanya mradi mdogo kwa kushirikiana na wananchi ili tuweze kuwasaidia.

Pia katika vile visima ambavyo vimechimbwa na Ras al Khaimah bado katika Jimbo la Tunguu hakuna hata kisima kimoja ambacho kimeacha kutumika pamoja na eneo la Mjonga na maeneo mengine tofauti. Kwa hiyo, ningeomba sana zile *pump* ambazo Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali amezizungumzia yupo tayari yeye kujitolea, na zile za Ras al Khaimah ambazo ziko zaidi ya mia zilitolewa katika msaada basi na mimi kwa Jimbo la Tunguu mtuonee jicho la huruma. Jimbo la Tunguu ni jimbo ambalo linakua kwa haraka, viwanja vingi vinatolewa, watu wanajenga lakini bado katika suala la miundo mbinu tuna changamoto. Kwa hiyo, katika suala la maji basi Mhe. Mwenyekiti kwa kupitia kwako Mhe. Waziri ajitahidi sana katika maeneo haya kuyatilia mkazo ili tuweze kuwasaidia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nitapenda nichangie kwa ujumla juu ya mambo tofauti, moja, nataka nizungumzie suala la meli ya mafuta. Tumepata fununu tunasikia kwamba kuna meli inataka kununuliwa ambayo meli hii itatumika kwa ajili ya mafuta na ni ya serikali. Lakini ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, mpango mkubwa wa serikali wao wanataka kujenga *depot* ya kwao kwa kupitia taasisi ya *ZURA* na eneo lipo Mangapwani. Sasa ukiangalia pale patakapokamilika ujenzi wa *depot* hii, hii meli ya mafuta ambayo itahitajika kwenda kuchukua mafuta katika maeneo tofauti itakuwa *redundant*, kwa sababu unaposema unataka kwenda katika mfumo ambao wa *BPS* (*Bio Procure System*) ina maana utakuwa na *single supplier* watu watakuwa na meli zao, meli zitakuja kufunga pale moja kwa moja katika eneo la Mangapwani watashusha mafuta. Sasa *unless* ile meli tutaanza kuikodisha,

lakini tutaikodisha kwa nani, kwa sababu bado sijapata uelewa mkubwa inawezekana.

Kwa hiyo, labda Mhe. Waziri atakapokuja katika mwezi wa tisa atatufahamisha zaidi, hii meli ya mafuta hasa kusudio lake ni lipi na ukiangalia katika mfumo huu wa *BPS* wanaotaka kwenda nao itatusaidia kitu gani. Ikiwa tunakwenda na mfumo huo huku unanunua meli mpya, sasa mimi nashauri fedha zile zichukuliwe twende tukajenge *depot* yetu moja kwa moja mpya wakati tayari wao wanafanya hii *study* ya *World Bank* tuangalie katika mfumo huo tutakwenda vipi. Sambamba na hilo nataka niunganishe katika mfumo mzima huu wa *BPS* ambao unahitaji *single supplier*.

Mhe. Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza sasa hivi leo asubuhi tumepokea taarifa ya Mhe. Waziri kwamba mafuta yalikuwa yameadimika kiasi hiki, yaliyopatikana yaliyokuwepo ni haya. Moja ya changamoto ambayo serikali iliyokuwa nayo ni kuwa na *strategic reserve* juu ya mafuta. Tunapata tabu kutokana na kwamba hatuna eneo la kutosha la kuweza ku-*cope* na *demand* ya mafuta yanayohitajika hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Kamati yetu ya Bajeti itakapokwenda kutembelea katika eneo la Mangapwani tumekuta ma-*tank* makubwa tayari yameshajengwa pale. Sasa nikiangalia kwa mawazo yangu kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kuishauri serikali, mawazo yangu yananipelekea maeneo matatu.

Suala la kwanza kuangalia ile sheria *Public Private Partnership* kuungana na hawa wawekezaji waliokuwepo ndani kutumia yale ma-*tank* ambayo yameshajengwa tayari kule Mangapwani. Eneo la pili ni kutumia ma-*tank* yaliyokuwepo Mtwara ili kuweka ile *reserve* ya mafuta kwa sababu *demand* ya Zanzibar kwa mwezi ni kati ya milioni kumi na mbili mpaka kumi na tano. Sehemu ya

tatu kuangalia ma-*tank* yaliyokuwepo kule Tanga, sasa tukisema tutegemee katika mfumo wa *BPS* ambao uzuri wanataka kurudisha kwenye mwezi wa nne na wa tano, ina maana kwa foleni ya Dar es Salaam meli kubwa zinapotaka kushusha mafuta na sisi tukitumia masuala ya *back road*, bado kutakuwa kuna uchelewaji wa vimeli vyetu kwenda kuchukua na kupiga hiyo *relay* kutoa mafuta Dar es Salaam kuyaleta hapa. Tukileta hapa pia kutakuwa kuna hasara ya masuala ya mafuta kupotea, pia usafiri tena. Sasa mimi nashauri *ZURA* waje na mkakati maalum kuangalia hizi *reserve* za sehemu tatu huku wakijipanga vizuri. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kila tukiangalia sasa hivi haipiti miezi miwili mafuta yanaadimika, sasa tujenge mawazo yenye ubunifu wa kutumia *reserve*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi natambua kwamba hawa taasisi yetu ya *ZURA* wana mkakati endelevu juu ya suala zima la Mangapwani wakisubiri *study* ya *World Bank*. Lakini naomba sana wakati wanapanga mikakati hiyo wananchi lazima wapate hii nishati ya mafuta na tusiwe tunaleta kero kwa wananchi katika kupata hii huduma, tunakera sana wananchi na wanashindwa kutuelewa, na tunaonekana hatuna mipango. Sasa mimi naomba sana serikali ijipange katika mpango endelevu na hili tatizo liondoke.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ni katika Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Nikisoma huu mstari wa kazi ya idara hii huwa najiuliza kwa mfano mchanga ni kama rasilimali unazidi kupotea kwa upande wa Zanzibar, baada ya hapo itakuwa *issue* ya mawe, baada ya hapo itakuwa *issue* ya maji. Kwa hiyo, naomba sana idara hii wakati inajipanga katika mipango miji na kusimamia suala zima la ardhi jinsi ya kujenga waanze kuangalia mfumo wa kujenga *low budget houses* kwa kutumia rasilimali gani ambayo itakuwa endelevu na itatumika pia kwa umakini kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wapo watu wanatumia hizi *prefabricated houses* najua zipo kampuni ziliwahi kuja katika miaka ya 1990, nafikiria huu mradi ambao unafanyika huku Fumba pia wana mpango kama huo, lakini wao wamekopa pengine mbadala wanaweza kutumia matofali na hizi *prefabricated*. Sasa tutumie njia ambayo suala la mchanga lisijekuwa baadae ni tatizo kubwa kuliko hivyo sisi tunaliona hivi sasa. Mimi naomba idara hii kwa kushirikiana na taasisi nyengine wapange mkakati kwa kuangalia wananchi wetu katika miaka ya mbele, kwa sababu kwa hali tunayokwenda nayo sasa hivi tupo wananchi milioni 1,450,000 kwa takwimu hii nilivyomsikia Mhe. Rais akiizungumza. Na ukiangalia kwa upande wa jinsi tunavyozaliana na uchumi wa Zanzibar unavyokua kila mmoja anataka kujenga, sasa lazima tuwe tunaangalia kwa kule mbali zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ni suala la *Airport*, nilizungumza leo asubuhi katika kipindi cha maswali na majibu kuhusu hii *airport service charge* unapata dola 40. Mimi naomba sana kwa sababu *Terminal II* itakapokamilika patatokea nafasi nyingi na fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Zanzibar na biashara tofauti. Lakini pia *Airport* hii itatakiwa ilindwe na iwe endelevu ya *Terminal II*. Kwa hiyo, mimi nashauri sana wizara husika ijipange kabisa kwenye masuala ya *training* kuanza kujua ni ajira ngapi zitatoka katika suala la *Airport*, lakini biashara gani ambazo zitahitajika na isiwe kama kufichwa na zisitolewe kwa upendeleo, zifanyiwe kwa *tender* wananchi wapewe elimu ya kutosha, watu wafaidike na wajengewe uelewa kama mtu anataka kufungua duka, ni duka la aina gani ataweza kufungua na biashara gani ambayo itakuwepo.

Pia na fedha ambazo zitakuwa zinapatikana waanze kuweka takwimu kuweza kujua kama wana-*anticipate* kupata kiasi gani cha fedha, na katika kuhakikisha kwamba ile *terminal* ikimalizika itakuwa ujenzi wake, *maintenance* yake, usafi wake sio tunakuja

kusikia kwenye *OC* hawajatiliwa. Sasa katika suala la *retain* watakayotiliwa hii dola 40 ya *airport tax* basi ianze kufanyiwa hesabu kabisa kama dola 15 wabakishiwe *Airport* ili kulinda ile *terminal* hasa na wageni. Ni aibu kuona kwamba ndani mara unasikia mafuta yamekwisha, sasa hivi angalau wamejitahidi sana lakini miaka ya nyuma kero zilikuwepo kama hizi, joto, *AC* mbovu. Kwa hiyo, mambo kama haya yanahitaji pesa.

Mhe. Mwenyekiti, utalii wa Zanzibar au wageni wanaokuja na suala la *Airport* ukiangalia haziendi sambamba. Suti anayovaaa Mhe. Waziri inaenda sambamba na utalii wa Zanzibar, lakini *Airport* yake sasa hivi haiendi sambamba. Kwa hiyo, lazima tuangalie mazingira yalivyo na kazi zetu zinavyokwenda pamoja na wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niunganishe hapa juu ya minara inayojengwa kwa ajili ya masuala ya huduma za simu na kwa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia minara yetu mjini sasa hivi kila pahala minara unaanza kuiona, na sisi kwetu ni kisiwa. Hivi najiuliza hakuna njia ya kuweka minara hapa Zanzibar lakini ule mnara ukawa kama mti umependeza, yaani ukatafutiwa njia ambazo ule mnara lisionekane chuma jekundu au rangi nyeusi lakini uwe unapendeza. Nafikiri ipo njia ya kuangalia kwa eneo letu kama visima vyetu tukaleta minara ambayo itakuwa na ubunifu yenye sifa nzuri kama utakuwa kama mti kama mvinje, lakini ukiangalia huujui kama ni mnara, lakini ni mnara kumbe ni mvinje. Naamini duniani tayari watu wameshafanya, sasa maeneo ambayo yanapendeza tutengeneze minara hii ambayo itakuwa inaleta sura nzuri na mtu akiangalia asijue pia kama ni mnara.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja suala la kampuni inayosimamia ujenzi wa barabara UUB. Mhe. Mwenyekiti, kila tukisoma na kila mwaka tukija tunaangalia kwenye bajeti kwamba sehemu fulani watu wanakosa mapungufu ya bajeti. Mimi nashauri kitu kimoja

ile sheria ya *Public Private Partnership* ambayo tumeshaipitisha na ipo. Mhe. Mwenyekiti, ile sheria kama inawezekana basi serikali ianze kuangalia kama ipo njia ya hili shirika letu pia, hii taasisi yetu kuingia katika mpango muhimu endelevu wakaungana na taasisi za kibinafsi na wakajipangia jinsi gani wao wataweza kufanya hizi kazi za huduma. Leo tukiangalia tunaambiwa *feeder roads*, *tanroads* watasimamia UUB lakini *feeder road* watasimamia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Lakini ukienda katika halmashauri zetu hawana vifaa watajenga vipi? Mimi Mhe. Mbunge wangu yeye ana vifaa anajenga kampuni, lakini ukiangalia UUB hiyo ni halmashauri yetu wanataka sijui sagamawe, watahitaji hili. Hebu tuangalie katika huo mji wa Tunguu ambao umekatwa viwanja zile barabara nikipita kote naambiwa mimi nikajenge, zitagharimu zaidi ya shilingi milioni mia sita. Shilingi milioni mia sita katika Wilaya ya Kati unazipatia wapi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa muda wako umemaliza, malizia dakika moja.

**Mhe. Simai Mohamed Said: N**aomba nimalizie dakika mbili. Ukienda katika maeneo yale ya viwanja vyote mpaka kule ukiangalia watu wakubwa wakubwa wanakaa, barabara zile zinatakiwa zijengwe njia zipendeze, huwezi ukasema Tunguu mji mpya lakini barabara ni mbovu tena ubovu wenyewe si mbovu tu ni mbovu sana. Sasa barabara zile ili tuzitengeneze tunahitaji fedha. Kwa hivyo, tuangalie hii taasisi ya *UUB* kama tutatumia ile sheria ya *Public Private Partnership* wakaungana na kampuni nyengine wakawa na vifaa vya kutosha. Leo kila eneo ukienda mtu anataka kujenga anahitaji kupita kwenye hizi *feeder road, feeder road* za Zanzibar kuwaachia Halmashauri haziwezi kubakia. Mimi naamini huku Mbweni, Chukwani, Mpendae mpaka tutakwenda pengine awamu ya tisa na ya kumi ya serikali nyengine *feeder road* zitabakia vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi naomba sana na baada ya hapo nashukuru sana, ilikuwa nimalizie hili suala la mafuta na gesi. Nashauri zile *data* Mhe. Mwenyekiti, namalizia. Zile *data* ambazo wamezipata katika kufanya kazi hii waliyofanya Seismic hii Kampuni iliyokuja waliyoingia pamoja na Ras al Khaimah hii taasisi waangalie sana zile *data* zetu watakuwa wanazi-*own*, wale watu wasije wakazitumia vibaya. Kwa sababu mtu ukishakuwa na *data* utakuwa na uwezo wa kwenda ku-*negotiate* mikataba tofauti ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia nakushukuru ahsante na nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Bahati Khamis Kombo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuchangia mchana huu. Kwanza kabisa niwapongeze sana mawaziri wote wawili, Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na Manaibu wao wote. Lakini pia niwapongeze sana Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano kwa juhudi zao kubwa ambazo wamezichukua kuona kwamba leo hii wametuletea changamoto mbali mbali mbele yetu tuweze kuzichangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja katika Mahakama ya Ardhi. Mahakama hii ina changamoto na kwa kweli changamoto hii ni kubwa na inafikia hadi kwamba wafanyakazi hawa wanakosa kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti iliyopelekea kupunguza ufanisi wa kazi za mahakama hiyo kwa upande wa Unguja na Pemba kwa kushindwa kupata vitendea kazi, kama vile vifaa vya

kuandikia, karatasi, kalamu, kompyuta, *printer*, mashine ya kutolea *copy* na mafaili ya kufungulia kesi. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana hapa kwamba wizara hii iwapelekee vifaa wafanyakazi hawa kwa sababu kutokupelekewa vifaa ni suala moja wapo linalosababisha kurundikana kwa kesi nyingi au kuweza kupoteza kumbukumbu za wananchi walio wengi. Tunajua kwamba wananchi wetu baadhi yao ni wakaazi wa shamba wanatoka na kwenda kusikiliza kesi zao, lakini wanapofika pale wakiambiwa kwamba kesi yenu leo haitoweza kusikilizwa hawajui ni sababu gani na kumbe ndani ya ofisi wameshajua kwamba kumbukumbu ile imepotea. Mheshimiwa niombe sana vitendea kazi vipelekwe ili wafanyakazi wetu hawa waweze kufanya kazi kwa ufanisi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika changamoto hiyo hiyo Nam. 6, Uchakavu wa Majengo ya Mahakama ya Ardhi Pemba yanayopelekea ofisi moja kutumiwa na watu zaidi ya mmoja. Mfano halisi Mahakama ya Ardhi ya Wete Pemba ambayo ofisi moja inatumiwa na hakimu, karani, wahudumu pamoja na matarishi wa mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, hili si jambo zuri kwa kweli, naiomba wizara inayohusika ifanye jitihada za makusudi kuona kwamba hakimu kapewa ofisi yake ili aweze kufanya kazi zake vizuri. Kuchanganya makarani, wahudumu pamoja na matarishi kwa kweli si jambo jema, kwa sababu hakimu anatakiwa afanye kazi zake kwa utulivu na awe na ufanisi mzuri. Lakini pia kuna wananchi ambao wanakwenda na kesi zao pale, inakuwa si jambo jema kama kwanza wanakwenda nazo kwa mara moja hazitakiwi kusikilizwa na watu wote, lakini ikiwa wamo hawa makarani, wahudumu pamoja na matarishi lazima kesi zile wataweza kuzijua mapema. Kwa hivyo, naiomba serikali ichukue jitihada za makusudi ili kuona hakimu kapewa chumba chake maalum cha kufanyia kazi zake.

Pia niwapongeze sana kamati kuona kwamba inaomba Mahakama ya Ardhi pamoja na Kamisheni ya Ardhi kufanya kazi kwa ukaribu ili kuweza kupunguza idadi ya migogoro ya ardhi inayozidi kuendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, migogoro ya ardhi imekuwa ni mingi sana. Kwa hivyo, tunaiomba mahakama ishirikiane na wenzao ili kuona kwamba kesi hizi zimeondoka kwa haraka ili kupunguza mrundikano wa kesi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika suala zima la maji safi na salama. Mheshimiwa nimeona hapa kwamba ziko changamoto nyingi lakini changamoto moja tu ambayo mimi nitaisemea ni kuchelewa kuunganishwa na mitandao ya maji kwa visima vya Ras al Khaimah.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la maji ni suala zito sana, naamini nikisimama tu basi watu wote husema he! Mhe. Bahati heshi kusemea maji, lakini hii ni changamoto na changamoto hii mimi imenitia hofu sana. Kwa sababu tuna visima ambavyo vimeshachimbwa muda mrefu baadhi ya vyengine tayari vimeanza kufanya kazi, lakini utaambiwa siku tatu tu visima vile tayari vimeshaharibika mashine. Je, Mhe. Mwenyekiti, ndani ya vile visima kuna nyoka anatambaa anatuhujumu lakini sisi wenyewe bado hatujamjua nyoka huyo. Naomba sana suala hili liangaliwe kwa kina kutokana na hali halisi tuliyonayo ya ukosefu wa maji ndani ya shehia zetu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni niliuliza swali katika Baraza letu hili kwamba kisima kilichopo Mgagadu kilichofadhiliwa na wenzetu Wachina hivi sasa kina tatizo la maji. Wananchi wa Mgagadu hawapati maji na tumeambiwa kwamba kisima kile huenda ikawa mashine imeharibika. Jambo la kusikitisha sana

kisima kile tumepewa karibuni tu haijatimia hata miaka minne kuambiwa kuwa tayari kisima kile hakifanyi kazi.

Jambo jengine la kusikitisha tunao wenzetu wa kijiji cha Ngomeni. Kijiji hiki kilikuwa ni sawasawa na kijiji cha Mgonjoni hawana maendeleo ya aina yoyote, lakini leo tunamshukuru Mwenyezi Mungu Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya juhudi kubwa sana kuona kwamba hivi sasa Ngomeni wanapata umeme, wanapata afya, wanapata elimu na maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kwamba pale vipo vijiji jirani ambavyo vilikuwa vikipata maji baada ya wenzetu wa Ngomeni kupata maji haya kikiwemo kijiji cha Kuyuni, Ngezi, lakini pia kuna kijiji kimoja ambacho kiko ndani Kaandani. Kijiji hiki hivi sasa hakipati maji baada ya kuuliza tumeambiwa kwamba wamekosa maji kutokana na masuala ya kiufundi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kama ni masuala ya kiufundi mimi nipo tayari saa yoyote tushirikiane na fundi huyu ili kuona wananchi wangu wa Kaandani wanapata maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia naomba sana kile kisima changu cha Ras al Khaimah kilichoko Ukutini, kilichoko Ngwachani. Namuomba sana Mhe. Waziri aniangalie tena kwa kina kuona kwamba visima vile vimepatiwa juhudi za makusudi ili wananchi wa Ngwachani na Ukutini waweze kutumia maji yale.

Vile vile niende tena katika maoni na maagizo ya kamati. Kamati inataka serikali kuharakisha ulipaji wa fidia za wananchi ambao aidha mazao au ardhi zao ziliathirika katika utekelezaji wa shughuli za uwekaji wa miundombinu ya maji. Mimi niseme tu Mheshimiwa, nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote baada ya kuleta suala langu hapa

la malalamiko la Mgagadu, Zawadini na Shumbageni watu wale wameanza kulipwa kwa hatua kubwa sana. Niseme tu kwamba hivi sasa tayari tumeshafikia asilimia 75 kwa waliolipwa. Kwa hivyo, hapa nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika tawi la Pemba changamoto nzima ya suala la umeme. Hapa nimeona kwamba ukosefu wa mita za TUKUZA imepelekea watu wengi kukosa huduma ya umeme kwa wakati. Mimi niseme kwamba ndani ya jimbo langu nashukuru sana, lakini jambo dogo ambalo naomba watendaji wetu wanapofika katika kupachika hizi mita za TUKUZA waweze kuelimisha wananchi. Kwa sababu imetokea changamoto moja ya kwamba wananchi wangu wa Kaalani, Zawadini pamoja na wananchi walioko Shumbageni wanapopachikiwa hizi mita wanapokwenda kuchukua umeme mtu anatoa shilingi 50,000 lakini anajikuta ana *unit* tano na baadae wao hawajui nini kilichotokea. Mimi nimechunguza vya kutosha nikaona kwamba hizi mita wao wanatakiwa watoe asilimia kidogo ndio waweze kuendelea baadae kupata umeme vizuri. Kwa hivyo, nawaomba sana wale watendaji wetu watakapokwenda kuwapachikia hizi mita wawape elimu ya kuwa hizi mita tunapachika lakini kuna asilimia fulani ambayo mnakatwa na baadae mkimaliza malipo hayo mtaweza kupata umeme vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Meneja wetu wa Shirika la Umeme wa Pemba kwa juhudi zake kubwa anazozichukua kuona kwamba wananchi hawapati matatizo ya mara kwa mara.

Sasa niende moja kwa moja katika mazingira. Kwa upande wa mazingira nimeona hapa kwamba uchimbaji ovyo wa mchanga kwenye maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Hali hii inasababisha athari kubwa za mmong'onyoko.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba sio Mjini Magharibi peke yake niseme hata na mimi sasa hivi katika jimbo langu la Chambani ile sehemu ambayo inachimbwa mchanga Giningi. Kuna haja Mheshimiwa pale ya watu kupewa elimu ya kupanda miti. Kwa sababu kama tunavyoona kwamba tumechimba mchanga kwa muda mwingi lakini mashimo yapo mengi hayana aina yoyote ya miti hivi sasa, ni hatari kwa jamii kwa sababu zitakapokuja mvua kubwa pale maji yanakaa. Naomba sana watu wanaohusika na mazingira basi na sehemu ile wale wananchi wanaomiliki wapewe taaluma ya kupanda miti.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia moja kwa moja katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Mimi bado naendelea kusema kwamba wizara hii inafanya kazi kubwa lakini bado wananchi wa vijiji vya ndani barabara zao zinahitaji matengenezo ya hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, ni karibuni tu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati anaifungua barabara ya Mgagadu-Kiwani aliwaahidi wananchi pale kwamba barabara ya Mgagadu kwa Mkoba itafanyiwa matengenezo. Tuliona kwamba barabara ile tayari ilitiwa doza lakini tuseme mpaka hii leo barabara ile haijaulizwa tena na huko mbele tukiangalia kuna mvua kubwa za masika. Niiombe sana wizara hata kama bado ule utengenezaji mkubwa haujafikia kiwango chake lakini naomba hata kile kifusi kidogo waweze kutiliwa, ili itakapofika wakati wa mvua kubwa basi wananchi wasiweze kupata kadhia kubwa kama waliyonayo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nakumbushia vile vile ahadi ya Rais ambayo aliiweka katika jimbo langu Ukutini kuelekea Matele Chwale. Namuomba Mhe. Waziri alikumbuke suala hili na ile barabara imekuwa kwa muda mrefu tokea mwaka 2010 muda

umeshakuwa mkubwa, naomba sana ifikiriwe ili iweze kufanyiwa matengenezo barabara ile tusimuweke Rais wetu vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nashukuru sana naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Bahati Khamis kwa mchango wako, sasa namwita Mhe. Masoud Abrahman Masoud akifuatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa na Mhe. Machano Othman Said ajitayarishe.

**Mhe. Masoud Abrahman Masoud:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia pumzi na uhai wa kuweza kusimama mbele ya Baraza hili tukufu. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza mawaziri wote wawili, Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na watendaji wao kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja niende kwenye ujenzi wa barabara za Kizimbani - Miwani. Niipongeze wizara kwa kufikiria kuwa barabara ile ni barabara ambayo muda mrefu ilikuwa na ahadi ya kujengwa. Bahati nzuri wizara imetia kifusi kuanzia Miwani mpaka Kiboje, ilipokuwa inatengenezwa barabara ile wananchi wote wa maeneo hayo tulikuwa tunafurahia, lakini sasa hivi barabara hiyo toka ilipotiwa kifusi vumbi ambalo linajitokeza ndani ya barabara ile ndani ya maeneo yale kuna skuli, kuna majumba ambayo yapo karibu na barabara ile. Sasa hivi ukienda hospitali ya Kizimbani kuna foleni kubwa ya wananchi wa maeneo yale ambao wanakohoa kweli kweli kwa mavumbi wanayoyapata.

Mhe. Mwenyekiti, katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017 kwenye suala la utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi barabara ile ilikuwa inatajwa, lakini kwa bahati mbaya bajeti ya mwaka 2017/2018 ikawa haionekani. Bado niiombe serikali kwa sababu imeshapoteza fedha nyingi na barabara ile tayari imeshatiwa kifusi, kama uwezo wa kuweka lami kwa sasa hivi haupo basi itiwe japo rojo ili wananchi wetu wasipate ule usumbufu wa kupata mavumbi mengi ambayo sasa hivi imekuwa hatari kwa maisha yao. Niombe sana Mhe. Mwenyekiti.

Sasa hivi watalii wanakuja katika maeneo ya Kizimbani lakini na wao wakiiona gari inakuja kwa *speed* basi vijana wa Kizimbani pale huwa wanawawekea vipolo ili wasipate vumbi. Kwa kweli watalii wale wanasumbuka sana. Niiombe serikali kwa kupitia Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake watafute namna angalau ya kwenda kutia lami ili watalii wetu pamoja na wananchi ambao wanapita kwenye barabara ile wapate kupungukiwa na hilo tatizo la vumbi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili hili suala la barabara ndani ya jimbo langu tulipata mtihani wa mvua kubwa ambayo ilijitokeza miezi mitatu iliyopita baadhi ya madaraja yalivunjika. Nipongeze sana wananchi na viongozi wetu wa jimbo Mbunge na Mwakilishi na watu wengine tumechangia kusaidia ujenzi au kukarabati madaraja yale. Lakini kwa sababu ujenzi wa daraja una gharama kubwa niiombe serikali, wanatusaidia kutupatia wataalam wapo tunasaidiana nao, lakini niiombe iingize nguvu zake ili ile miradi iliyokwishaanzishwa ya ujenzi wa yale madaraja iweze kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala kubwa ambalo wenzangu kila anayesimama alikuwa analizungumza, suala la maji safi na salama. Niipongeze serikali kwa kutafuta

mikopo mbali mbali na makusanyo yetu ambayo tunayakusanya ya ndani kwa kuamua kutatua tatizo hili la maji safi na salama kwenye visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali takwimu inayotoa na ukienda huko kwenye majimbo ukiangalia kiuhalisia bado tuko mbali kweli. Mimi kwenye jimbo langu Shehia ya Mbuzini tokea nianze kuwa diwani kule mwaka 2000 mpaka 2015 na mpaka nikapata nafasi hii ya uwakilishi maji kutoka *ZAWA* hayajawahi kufika, wanatusaidia matajiri, wenye viwanda na baadhi ya watu waliochimba visima vyao binafsi, ndio watu wanafaidika na maji, lakini maji ya *ZAWA* hayapo.

Niiombe serikali iandae utaratibu kwa sababu kisima kichimbwe katika eneo la Mbuzini angalau watutilie *pump* na mabomba, bomba lipo liliwekwa. Niiombe serikali watutilie *pump* ili wananchi wa eneo lile la Mbuzini na wao wapate kufaidika kwa maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili la maji linaikumba pia Shehia yangu ya Bububu chini ya mlima pale kutoka Kijichi ukienda pale utaona huruma jinsi mabomba yalivyopasuka na yanavyomwaga maji safi na salama. Niwaombe wizara Mamlaka ya Maji *ZAWA* waandae utaratibu wa kwenda kutizama eneo la Kijichi Bububu maji mengi sana yanapotea. Maji hayo kama ingekuwa yanakwenda moja moja kwa wananchi maeneo makubwa wangekuwa yanapata maji safi na salama. Lakini uchakavu wa mabomba sasa hivi umekuwa ndio wimbo wa taifa katika eneo letu lile, kila siku ukipita maji yanavuja. Kwa hiyo, niwaombe Mamlaka ya Maji *ZAWA* watafute namna ya kutusaidia katika maeneo hayo.

Lakini maeneo ambayo walizungumza wenzangu ya Ras al Khaimah. Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kalizungumzia

suala la visima vya Ras al Khaimah, ni kweli kama serikali wangeamua hizi fedha ambazo zinapatikana wakamalizia hivi visima vya Ras al Khaimah tatizo la maji baadhi ya maeneo lingepungua. Lakini kwa bahati mbaya tunakwenda kuchimba visima vyengine vile vya Ras al Khaimah vinabakia.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika eneo langu la Dole kisima kimechimbwa limejengwa na tangi moja kubwa sana na nimshukuru Mhe. Mkuu wa Wilaya akaliingiza kwenye Mbio za Mwenge wa Uhuru likaenda kuzinduliwa, lakini mpaka leo kisima kile bado hakifanyi kazi bajeti zote zilizopita. Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu Mhe. Waziri huyu ni mpiga kura wangu katika Jimbo langu la Bububu, halafu ni dada yangu nilimuomba sana kati ya visima ambavyo anatagemea kuviingiza kwenye mpango wa ujenzi viwe visima vya Ras al Khaimah na  hasa cha Dole. Kwa sababu tangi lipo na wananchi walio katika Shehia ya Dole, Shehia ya Kiwamba Ngoma, Mkanyageni, Kizimbani wana tatizo la maji safi na salama na tangi hili lingesaidia kwa wananchi hao kuwapatia maji. Kwa hiyo, nimuombe dada yangu Mhe. Salama Aboud Talib, Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira mara hii na mimi aniingize katika ratiba yeye na watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nimpongeze sana Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme kwa kazi nzuri ambazo anazifanya na hasa kwenye jimbo langu pamoja na wenzangu wanasaidiwa kwa kunisaidia mradi wangu mkubwa wa Kikaangoni, lakini pia mradi wa Mbuzini barabarani. Niwapongeze sana kwa hilo. Lakini bado tuna tatizo katika eneo la Mipopooni la Mbuzini kuna nyumba wananchi wengi wanahitaji umeme katika eneo hilo. Lakini kama walivyosema wenzangu sasa ukienda shirika lile eneo la nguzo tano bili yake ukiletewa kwa kweli inakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa wananchi. Lakini mzigo ule ukitoka kwa wananchi huwa unakuja kwa Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi. Kwa

hiyo, niiombe serikali kwa kupitia kikao hichi waangalie taratibu yale maeneo ambayo tayari sasa hivi yameshakuwa na wakaazi wengi basi tuandae utaratibu ili nguzo za umeme zisambazwe na wananchi hao wapate kuvuta umeme kwa urahisi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Shirika la Meli na hasa meli ya Mapinduzi II. Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii inaonesha kama hii meli tayari inaanza kutushinda na serikali imetoa fedha nyingi na ni muda mfupi sana toka meli hii iliponunuliwa. Niombe serikali iangalie kwa jicho la huruma na iangalie vizuri watendaji wa hii meli. Kwa kweli meli za matajiri siku zote unaziona zinafanyakazi lakini meli hii ilipoletwa sisi tulitegemea itakuwa ni ukombozi wa Wazanzibari. Lakini kwa bahati mbaya sana meli hii siku zote ina matatizo leo chombo fulani, kesho chombo fulani, kesho kutwa chombo fulani.

Niiombe serikali ikiwezekana iundiwe kamati hii meli ichunguzwe au ipelekwe kwa mganga wa kienyeji ikapigiwe pungwa kwanza. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hili limekuwa tatizo sugu meli tumenunua kwa mapesa mengi haijafanya kazi hata mwaka mmoja hakuna kinachoendelea. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala hili pia kuna tatizo hii meli inapopata angalau ile nafuu ya kutembea kutoka Unguja kwenda Pemba bei ya tiketi ni shilingi elfu kumi na nane, unaambiwa ukienda kukata tiketi lazima uwe na kitambulisho cha Mzanzibari. Lakini tiketi ya meli ya Mapinduzi II huipati kama huna shilingi elfu thalathini.

Serikali kila siku tunapiga kelele watu wauziwe tikeki kwa mujibu wa kitambulisho. Lakini kwa bahati mbaya sana ukienda pale walanguzi wapo na wanalangua tiketi kwa bei ya shilingi elfu thalathini. Niombe serikali iunde kamati angalau pale

wakikamatwa watu wawili, watatu wakitiwa ndani kazi ya ulanguzi wa tiketi utapungua.

Mhe. Mwenyekiti, utafiti wa mafuta na gesi. Niipongeze serikali na sasa hivi kwenye maeneo yetu kila siku utakuta watu wenye kampuni zile na magari yao wanazunguka zunguka na inaonekana utafiti huu Mwenyezi Mungu ajaalie tufanikiwe tuweze kuyavuna hayo mafuta na gesi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ambalo ni dogo tu lakini niiombe serikali zile shehia ambazo tunategemea kwenda kwa ile siku mbili kabla iwe inatoa taarifa kwa wananchi, kwa sababu wale katika utafiti wao wanapiga mabomu, sasa yale mabomu kuna watu wana *pressure* yanawashtua sana. Kwa hiyo, niiombe serikali siku mbili kabla ya kwenda kufanya utafiti maeneo yale watoe taarifa ili wananchi waweze kujua kama kuna kitu fulani eneo letu kitajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nimpongeze tu Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira lakini ombi langu la kisima cha Ras al Khaimah na Dole alitilie umuhimu sana. Lakini pia Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji aiangalie sana barabara yangu ya Miwani ambayo sasa imekuwa tatizo kwa watalii pamoja na wanafunzi ambao wapo katika Skuli ya Kizimbani. Baada ya kusema hayo niipongeze Ripoti ya kamati hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa na mimi ya kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mawaziri wawili wanaohusiana na kamati hii pamoja na Manaibu Mawaziri na watendaji wao wa Wizara hizi. Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa ripoti yao hii nzuri na yenye muelekeo mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi nianze kwa kuchangia Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze hii mamlaka kwa jitihada zake kubwa wanazozifanya katika kutupatia maji safi na salama. Mhe. Mwenyekiti, nadhani sote tunashuhudia na nikisema Zanzibar ni Unguja na Pemba kwamba visima vingi vya maji vimechimbwa lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa kuna maeneo bado maji hayajafika. Sasa tunaiomba mamlaka ifanye jitihada ili zile sehemu ambazo bado maji hayajafika basi tunawaomba sehemu hizo yafike.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika jimbo langu kwanza niipongeze serikali sehemu kubwa maji yamefika, lakini kuna sehemu bado hatujapata maji. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwamba tumekwenda pamoja katika jimbo langu kutembelea mpaka sehemu moja Kengeja Mjiweni pale pamechimbwa kisima. Nikamueleza kwamba kuna watu wa Shehia ya Chole bado maji hawapati na akanieleza kisima ndio hichi na kisima kina maji ya kutosha lakini bado *pump* hatujapata. Sasa namuomba Mhe. Waziri muda umekuwa mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali kwa kujitolea kukopesha pesa hapa kwa ajili ya hizo *pump*. Kwa hivyo, naomba na hapa watu wa Chole kisima kilichopo Mjiweni kitupiwe macho, ili watu wa Chole nao wafaidike kupata maji kabla ya mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nizungumzie kuhusu *ZAWA*, kuna malalamiko makubwa mara nyingi unapofungua redio kusikiliza Mawio utasikia kwamba kijiji fulani wamepigiwa *ZAWA* mabomba yamepasuka maji yanapotea lakini hawaendi hata wapigiwe simu. Kwa hivyo, tunakuombeni kwamba tabia hii sio nzuri, sio tabia ya uungawana, zile sehemu ambazo mnapata

taarifa kwamba maji yanapotea basi ni vyema mnapopata taarifa muende, mfanye uungawana hii ndio kazi yenu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nizungumzie *ZAWA* Pemba. *ZAWA* iliyoko Pemba inakusanya mapato lakini mapato yale baadae wanayapeleka Unguja yote, wakati huo huo inawezekana wakarejeshewa kidogo. Lakini mimi naiomba serikali kupitia wizara basi yale mapato yanayokusanywa kule Pemba yabakishwe kule kule ili waimarishe ile miundombinu ya maji iliyoko kule. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, suala hili naomba wizara ifanye hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nichangie Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO).* Kwanza nilipongeze shirika kwa jitihada yake kubwa zaidi kwa upande wetu Pemba kwa sababu visiwa vingi vilivyokuwepo Pemba vimeshapata umeme kikiwemo kisiwa changu cha Shamiani Muambe. Lakini mimi hapa Mhe. Mwenyekiti, kidogo nina masikitiko kwamba *ZECO* wanadai tena pesa nyingi na masikitiko yangu makubwa kwamba wanapodaiwa maskini wananchi watu wa chini wengine wanakatiwa umeme.

Lakini sasa hapa tumeambiwa kuna *ZAWA* wao wanadaiwa, Taasisi nyengine za SMZ zinadaiwa, Taasisi za SMT zinadaiwa pesa sio kidogo bilioni kumi na tano, milioni mia tatu arubaini na tatu, laki saba na ishirini, mia moja na tisa pointi saba si pesa kidogo. Sasa na wanaodaiwa mimi nathubutu kusema si maskini, kwa nini hawalipi? Aangalie maskini aliye chini zaidi ndie anayetiwa mkakati kwamba lazima alipe, lakini hawa kwa nini hawaambiwi wakalipa na pesa ni nyingi hizi.

Sasa nadhani Mhe. Mwenyekiti, kama hizi Taasisi za SMT ni vyema na wao wakalipa kwa sababu *ZECO* ilipokuwa inadaiwa deni kubwa na *TANESCO* hapa Zanzibar tulifika pahala tukataka

kukatiwa umeme. Lakini kumbe "Mkuki kwa nguruwe kwa mlimwengu unaumiza sana".

Sasa nadhani iko haja na sisi kutia changamoto kwamba hizi Taasisi zote za SMZ, SMT zilipe ili *ZECO* na wao wapate fursa ya kufanya mambo yao vizuri, ili zile sehemu ambazo tunapiga kelele majimbo yetu umeme haujafikishwa basi ufikishwe Pesa hizi tukizipata zote basi nadhani sehemu nyingi umeme utafika kwa sababu sio kidohgo. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwenye masuala hayo ya deni basi ni vyema zile taasisi zote zinazodaiwa zikalipa, ili *ZECO* wakaenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile niendelee kuchangia Shirika la Nyumba Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilipongeze hili shirika linafanya jitihada kubwa ingawaje kuna kasoro ndogo ndogo. Naiomba wizara izishughulikie hizo kasoro ili na wao waende vizuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa tumeambiwa kwamba kamati imetembelea sehemu mbali mbali kuangalia idadi ya nyumba zile za shirika. Lakini hapa mimi nataka niende sehemu ya huku Pemba na hasa nataka kuzungumzia katika nyumba iliyopo Kengeja.

Mhe. Mwenyekiti, hii nyumba imejengwa na nakumbuka kwamba imewekewa jiwe la msingi na Mhe. Mzee Abeid Amani Karume marehemu tokea tarehe 12 Januari, 1972. Hii nyumba ilitolewa fidia sehemu kubwa kupewa watu wa Kengeja waliokuwa wanaishi katika kijiji kimoja kinachoitwa Makomba, kwa sababu sehemu waliyokuwa wanaishi ilichukuliwa na serikali kwa kupewa Magereza. Sasa watu walihamishwa kijiji kizima wakenda kulipwa sehemu hiyo ya majenzi kwenye nyumba hii. Sasa hii nyumba Mhe. Mwenyekiti, iko katika hali mbaya. Juzi nimekwenda pale kutembea pana jamaa zangu basi kiukweli hali yake si nzuri ukiingia mle ndani unaweza ukasema hutoki.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii nyumba kwa kusema kwamba waliopewa ni wenyewe wamepewa fidia. Serikali ikisema kwamba hii nyumba waachiwe wale hii nyumba itaanguka. Kwanza namuomba Mhe. Waziri aende akaikague ile nyumba iliopo pale Kengeja aiangalie hali yake. Naiomba serikali ile nyumba basi waende kwanza wakakae na wananchi wanaoshi pale wabadilishane mawazo waone tupite njia ngani ili hii nyumba tuihifadhi isije ikaanguka. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, hapo nimeshafahamika.

Vile vile naomba nichangie Idara ya Utunzaji wa Barabara *UUB*. Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 45 hapa namba 7 unaosema ucheleweshaji wa ulipaji fidia kwa wananchi walioathirika katika ujenzi wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka niipongeze serikali kwa jitihada yake kubwa kwa ujenzi wa barabara zetu na nataka niseme kwamba serikali inajitahidi sana. Lakini mimi nina kilio kwa muda mkubwa kwa ujenzi wa barabara ya Mtambile-Mwambe. Hapa ujenzi huu wa barabara ilipojengwa na muda umeshakuwa mkubwa zaidi ya miaka kumi wananchi wa sehemu hizi waliharibiwa vipando vyao. Sasa mpaka hii leo wananchi wale bado hawajalipwa pesa zao. Je, lini wananchi watalipwa pesa zao.

Mhe. Rais wa Zanzibar suala hili ameshalitolea maelezo kwamba serikali ichukue jitihada mara moja ili kulipwa. Siku ile nadhani Mhe. Mwakilishi wa Gando alilizungumza suala hili mbele ya Rais na Mhe. Rais akasema kwamba ichukuliwe hatua mara moja kwamba hawa watu walipwe pesa zao, watu wa Gando, watu wa Muambe yaani barabara hii ya Mtambile-Muambe walipwe pesa zao muda umeshakuwa mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hiyo iliyojengwa hivi sasa haipitiki imeshamaliza. Lakini watu walioharibiwa vipando vyao mpaka hii

leo bado hawajalipwa. Sasa naiomba serikali hili suala basi ile kauli ya Mhe. Rais tuithamini kwamba sisi hutegemea Rais akishasema mambo yatakwenda vizuri. Sasa tena pasiwe na kusita sita kwa sababu wananchi watatoka imani na serikali yao. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naona nifikie hapo mimi naiunga mkono ripoti hii mia juu ya mia, ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mussa Foum Mussa kwa mchango wako, sasa namwita Mhe. Machano Othman Said nae aweze kutoa mchango wake kwa mchana huu.

**Mhe. Machano Othman Said:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo sana leo kwa sababu hali yangu ya afya kidogo sio nzuri, lakini imebidi nitoe mchango wangu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Siku ya Alkhamis iliyopita mimi na Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tulikwenda kutembelea baadhi ya sehemu ya jimbo letu kwa mambo mawili. Jambo la kwanza kuangalia sehemu ambazo zinavujisha maji na jambo la pili kuangalia hali halisi ya matenki ya maji katika Shehia ya Kama. Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda Shehia ya Chuini na Kama bahati nzuri Mhe. Naibu Waziri alifuatana na wataalam wake wa *ZAWA.* Hali ambayo tumeikuta kule Mhe. Mwenyekiti, ni ya kusikitisha kwanza mabomba mengi yamepasuka na yanamwaga maji yanatiririka tu bila ya mpangilio.

Kule kwetu tuna maji ya mgao sasa ukienda siku ya mgao ndio hatari zaidi. Katika baadhi ya maeneo migomba na miti mingine imenawirika na kuwa rangi ya kijani zaidi kutokana na umwagiliaji wa maji ovyo. Lakini baada ya kazi ile kuangalia sehemu ambazo zimeharibika mabomba tulipata fursa pia ya

kutembelea matenki mawili  ya maji Kama, ingawa moja tayari limeshaanguka na sasa hivi wanatoa vipuri kwa ajili ya kutengenezea sehemu nyengine. Lakini hilo ambalo halijaanguka halikai maji kwa sababu uwezo wa kukaa maji hamna sasa hivi limekuwa kama pakacha tu maji yanaingia lakini yanamwagika.

Kwa maelezo ya wataalam wa maji walisema wanaweza kujenga jingine pale jipya lakini baada ya kumaliza kujenga Mkwajuni na Paje kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub ndio waje kuangalia eneo lile. Kwa maelezo yao tenki lile lina uwezo wa kuwahudumia wananchi 30,000, kwa hivyo kama lingekuwa linafanyakazi vizuri maana yake wananchi wa Shehia ya Mfenesini, Shehia ya Kama na Shehia ya Chuini wasingelikuwa na tatizo la maji hata kidogo. Kwa hivyo, niombe serikali wafanye juhudi ili kutatua tatizo hili la maji katika shehia hii.

Mhe. Mwenyekiti, humu Barazani kama alivyozungumza mwenzangu tuna majimbo karibu hamsini na nne baadhi ya wenzetu ni mawaziri na sisi wengine *backbencher*, lakini hata mawaziri nina hakika na wao kwenye majimbo yao wana tatizo kubwa la maji, pamoja pengine na wewe Mwenyekiti na wengine maji ni tatizo. Ombi langu kwa serikali kwa sababu sasa hivi Mwenyekiti wa Kamati kasoma ripoti yake sisi wajumbe tunaichangia baadae tutakuwa na mrejesho wa serikali mwezi wa tisa. Niombe serikali kuna kipindi cha mpito hapa leo ni mwezi wa pili lakini kati ya mwezi wa tano na wa sita wizara hii itakuja Barazani kuomba bajeti kwa kupitia bajeti yetu ya 2018/2019, na baada ya miezi mitatu watakuja tena kuelezea mafanikio na utekelezaji wa ushauri wa kamati.

Mimi naomba na wenzangu nitawashawishi baadae, kwanza wizara hii katika kipindi hichi cha miezi sita cha mpito watayarishe *roadmap* ya kuonesha kila jimbo maeneo ambayo wanapata maji ya uhakika na salama ili tuje kujadili kwa kina. Na

ikiwezekana wizara hii kabla ya bajeti yao waandae semina kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuwaeleza nini changamoto ya maji katika nchi yetu ya Zanzibar. Maana yake kila mmoja anasema lake, wakija *ZAWA* wanatwambia maji tunapata kwa asilimia 75 - 80 lakini wenyewe wanakiri kwamba asilimia 30 yanamwagika njiani, kwa hivyo hata hiyo asilimia 50 haifiki. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, ukifika wakati wa kamati mwezi wa 9 bado hakuna mambo hayo mimi nitalishauri Baraza liunde Kamati Teule kwa ajili ya maji tu kuangalia nini tutafanya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, natoa tu kama indhari ikifika mwezi 9 bado suala la maji liko hivi hivi basi tutaomba serikali kupitia Spika aunde Kamati Teule. Kwa sababu kwa mujibu wa kifungu 111 cha kanuni zetu Mhe. Spika anaruhusiwa kupitia Baraza la Wawakilishi kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo maalum ambalo linahitajiwa kuzungumzwa kwa kina. (*Makofi*)

La pili umeme Mhe. Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila kama wenzangu Shirika la Umeme wamejitahidi sana kufanya kazi zao, ukiangalia miaka ya nyuma na sasa wamebadilika na wanafanya kazi vizuri. Tuombe tu Shirika la Umeme waendelee kuimarisha ule mradi wao wa kuhuisha umeme katika baadhi ya maeneo ambayo yanapata umeme mdogo yakiwemo maeneo ya jimbo la langu mimi kama Chuini, Kama na sehemu nyengine. Kwa hivyo, ni matarajio kwamba shirika hili litaendelea kutoa huduma nzuri kwa wananchi ili kusonga mbele na wananchi wapate huduma na waangalie sasa utaratibu. Kwa sababu mtu akiingiza umeme atanunua umeme kwanza waangalie utaratibu wa kuwakopesha watu katika kuunga umeme, ili hizi kelele za waheshimiwa kwamba gharama za kuunga umeme ni kubwa zitaweza kufidia kutokana na mkopo kwa wananchi. Lakini pia kwa Shirika la Umeme, wajitahidi kuondokana na hizi mita za kawaida, mradi ule wa mita za *TUKUZA* ufanye kazi kwa haraka

ili kusiwe na sababu kwamba sisi tunalipishwa hivi tunakatiwa umeme nafikiri hili linawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, nafikiri hapa sina mambo mengi nitazungumza kidogo sana. La kwanza, najua kama serikali wameliona hili na wanajua ni tatizo, lakini tunaomba tu serikali iharakishe kutafuta vifaa vya ujenzi na kuwakabidhi *UUB set* mpya za ujenzi. Hivi sasa ni tatizo hata kama tunapata pesa za maendeleo lakini utekelezaji wa miradi yetu kupitia idara hii unakawia sana kwa sababu inayoeleweka kwamba vifaa vyao ni vichache na vichakavu. Kwa hivyo, natarajia kwamba wizara hii itajitahidi kuwapatia *UUB* vifaa vya kutendea kazi ili na sisi tusiweze kugombana na serikali katika utekelezaji wa shughuli zetu za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, barabara tumemsikia Mhe. Simai Mohammed Said kwamba ukweli *feeder roads* ipo katika Tawala za Mikoa, lakini Tawala za Mikoa hawajawa na vifaa vya kufanyia kazi, lazima Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ndio watoe vifaa vya kufanyia kazi. Kwa hivyo, tunaomba sana wapatiwe vifaa hivyo waweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine la danadana ni kati ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuhusu kukabidhiana barabara za *MIVARF*. Tunaomba hadithi hii nayo ifike mwisho, kama kuna tatizo la kiserikali lipatiwe ufumbuzi ili barabara hizi zikabidhiwe ujenzi ziweze kufanyiwa ukarabati, barabara zimejengwa na sasa hivi zishaanza kuharibika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira narejea tena kuhusu Idara ya Mipango Miji. Mhe. Mwenyekiti, naomba watu wa mipango miji pamoja na majukumu

yao mengi lakini waharakishe kwenda kupima eneo la Chuini pale Kwanyanya kwa ajili ya mji mdogo kama serikali ilivyokubali ili manispaa ya Magharibi 'A' waweze kupaendeleza. Hivi sasa ni hatari sana daladala zinakaa njiani, magari ya mawe yanakaa njiani, watu wanakaa njiani, kwa hivyo matatizo ni makubwa. Lakini pale kama tunajenga soko, kituo cha daladala na mambo mengine patakuwa pazuri. Kwa hivyo, tunaiomba Idara ya Mipango Miji waweze kukamilisha zoezi la eneo lile ili wananchi nao wajue kutakuwaje.

Mwisho Mhe.Mwenyekiti, kwa Wizara zote mbili, wizara hizi ndio wizara ambazo zina mamlaka na mashirika mengi kuliko wizara zote kwa Zanzibar, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Tumesikia kwamba serikali kwa kupitia Tume ya Utumishi inataka kuweka usawa katika mishahara na maposho kati ya wafanyakazi wa mashirika na serikali, hili jambo halikubaliki sana katika utumishi wa umma kwa sababu hata wenzetu huwezi kulinganisha mfanyakazi wa shirika na mfanyakazi wa serikali. Wafanyakazi wa mashirika wanafanya kazi kwa malengo maalum na wanapangiwa na mashirika yao, wanafikia lengo la kuzalisha wanajitahidi sana kufanya kazi. Kwa hivyo, mimi nashauri tusije tukafanya kwamba mfanyakazi wa shirika mshahara wake uwe sawa au maslahi yake na wa serikali. Mashirika yana taratibu zao wapange walete serikalini lakini lazima wao wenyewe madam wanapata faida basi waachiwe waangalie nini wanafanya katika suala hili. Tukiharakisha tunaweza kuyavuruga lakini pia tunaweza kurejesha nyuma mchango wao katika shughuli za uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi naunga mkono ripoti hii ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano na naomba waheshimiwa wenzangu wapate nafasi ya kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe dakika kumi zilizobakia nampa Mhe. Jaku Hashim Ayoub amalizie.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unaosema unapokuta maji yakoge hujui kama mbele utayakuta tena. Nichukue fursa hii kwanza kuzipongeza wizara zote mbili. Mhe. Mwenyekiti, nishukuru leo watendaji karibu wizara zote mbili wapo juu, tofauti na jana Wizara ya Afya tulipokuwa tukichangia watendaji walikuwa hawapo baada ya Katibu Mkuu na nani, leo juu kunaridhisha kiasi fulani. Namuona Mhe. Waziri kama anaumwa umwa kidogo, leo Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira hali yake sio nzuri, pengine nimpe pole namuona kama mnyonge mnyonge kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na kitengo cha *ZMA* cha usajili wa meli. Juzi nilipiga kelele kidogo kwa kitengo hichi na nikasema kuhusu usajili wa meli, kuna meli zinaanza kuondoka kwenda kusajiliwa nchi nyengine. Amri iliyotoka kwa ndugu zetu wa damu kuwa meli yenye usajili wa nje ya nchi kama Iran, Dubai Muscat na nchi nyengine sio meli zilizokuwa za ndani, meli za ndani zimo katika mzunguko huo wa ndani chochote kinaweza kikazuiwa. Naomba kidogo waziri hapa afuatilie na tulikuona kwenye vyombo vya habari kwa mbele meli za ndani hakuna sababu za msingi na sisi tunahitaji mapato.

Ikiwa meli inaenda kusajiliwa Japan, Iran, Dubai pale kidogo mtihani, lakini meli inatoka nje ya nchi inakuja hapa mpya inataka kufanya kazi hapa mnazuia aa! sio halali. Mhe. Waziri utakapokuja hebu tueleze hii meli mpya iliyonunuliwa kwa pesa chungu nzima karibuni dola milioni 30 ni tatizo. Nilisema mimi meli hii kabla hajaongeza *Azam Marine* boti nyengine mpya, boti zake tatu au nne hazifiki gharama ya  meli hii. Ni pesa nyingi

zilizotumiwa na leo meli yetu nimeshuhudia ikienda ikishusha inasuasua.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la barabara nimpongeze sana mkurugenzi aliyepo na nimpongeze kuongezwa muda wake Bw. Ali Tahir, kazi aliyoifanya tumeiona ni kubwa pamoja na vitendea kazi kuwa havipo. Nimuombe tu kuna mashimo kule njia ya Paje bado hayajakaa sawa ni hatari na watalii wengi wanatumia njia ile kidogo inaweza kusababisha ajali Mwenyezi Mungu asije akajaalia kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la maji ambacho ni kilio cha karibu wawakilishi wote, suala la maji limekuwa tatizo sugu, hichi ni kilio cha watu wote na kama tunavyojua maji ni uhai wa kila kitu. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa nia yake ya kutumikia wananchi, ikiwemo harufu niliyoipata niwaambie watu wa Michamvi, kuna harufu nzuri sasa inaanza kuelekea kwa muelekeo. Nategemea bajeti inayokuja huenda Mwenyezi Mungu akajaalia ikaingizwa fedha ile kupata maji yaliyokuwa safi na salama. Kwa hivyo, niwaambie wananchi wa Michamvi kwa harufu niliyoipata wakae mkao wa kula panapo majaaliwa chini ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kupitia mwakilishi wao kwa kelele alizopiga ndani ya chombo hichi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mtumishi wao lakini tumeshuhudia kuna eneo la Kibondemaji karibu kila mwaka kunatokea ajali au wakati mwengine watu kupoteza maisha. Tulishuhudia pale alikwenda Katibu Mkuu kuhusu ujenzi wa daraja je, umefikia wapi. Kuna msemo unaosema "Usipoziba ufa utajenga ukuta". Tulishuhudia pale walikwenda wakandarasi lakini naona kimya mpaka leo na nilimuona Katibu Mkuu mwenyewe yupo juu sasa atueleze.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwenye ripoti hii kama sikumshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa ripoti yake sijamtendea haki kwa umakini wa hali ya juu hakuficha kitu kaeleza mengi. Katika Mahakama ya Ardhi kweli kulikuwa kuna kilio kikubwa sana cha muda mrefu kuna watu wanakuja pale *Majestic* kutafuta haki zao lakini pa kujificha mvua hapana baadae wanaroa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye tatizo la mafuta *formula* iliyotumika pale bado haijakaa sawa, lakini kwa harufu niliyoipata kwa *formula* ile nafikiri imevunjwa kwa muagiziaji mmoja, sasa hivi mwenye mafuta ni *GAPCO* na *Zanzibar Petroleum* kidogo. Niwatoe wasi wasi wananchi kuna meli kubwa ya *UP* huenda ikaingia lakini nafikiri jioni hii au kesho pengine. Kwa hivyo, tatizo la mafuta huenda likapungua kwa data nilizokuwa nazo au harufu niliyoipata.

Mhe. Mwenyekiti bado dakika moja iliyobaki hii niendelee kukushukuru na mimi muda umekaribia kufika. *(Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Nashukuru sana kwa kujali huo muda saa zetu zina matatizo hazilingani wajumbe samahanini sana pale inapotokezea kasoro fulani fulani. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa muda huu tuliokuwa tumeutumia kuweza kujadili vizuri ripoti hii na hatimae tukafikia muda huu kwa salama niwapongeze sana. Naakhirisha kikao hichi cha Baraza hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa tunaendelea na kuchangia ripoti iliyo mbele yetu na mchangiaji wetu wa mwanzo, sasa hivi atakuwa Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali.

**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Kwanza kabisa napenda kuipongeza hii kamati kwa ripoti yao hii ambayo inafahamika vizuri. *(Makofi)*

Pili nakupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa busara zako ambazo unazichukua katika kutupa nafasi sisi Wawakilishi kuchangia, ahsante sana. Mimi mchango wangu utakwenda moja kwa moja. Kwanza nianze na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, nikianza tu nitaanza na sekta ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyoelewa kwamba ardhi ni raslimali ambayo kwa kweli tunaitegemea kwa kila hali, tunaishi juu ya ardhi, tunajenga juu ya ardhi, tunatembea juu ya ardhi na tunajenga majumba, barabara, viwanda na kadhalika na zaidi ya yote tunazikana kwenye ardhi, ni muhimu sana. Lakini sasa ukiangalia ardhi yetu ni ndogo, idadi ya watu inaongezeka kila uchao, wanaozaliwa na wanaoingia. Mhe. Mwenyekiti, tunakumbuka sote hapa mwaka 1994/1995 tulikuwa watu 300,000 na sasa hivi tuko watu milioni moja na nusu, na pengine ikifanywa sensa leo inawezekana tukawa milioni mbili na zaidi. Hii inatulazimisha tuitunze tena tuitunze sana ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia tena mwaka 1984 nadhani lilitokea joto kali sana hapa Zanzibar, kiasi kwamba mikarafuu ilianza kunyauka, migomba ikakauka, wale wanaokumbuka watakumbuka. Matokeo yake maji yalipanda kwa *centimetre* kama hivi, wataalamu wa mambo ya mazingira wanafahamu, maji yalipanda juu na lingeendelea joto lile kuna hatari ya baadhi ya

sehemu tungezikosa. Sasa hayo ni mambo ya maumbile *climate change*, yaani mabadiliko ya tabia nchi yanatudhuru. Mhe. Mwenyekiti, mbali na hayo wenyewe sasa tunakata miti, tunachimba ardhi isivyotakiwa, tunachimba mawe visivyotakiwa. Tumeona kule Pemba watu wanachimba mawe mpaka maji yanatoka. Huko chini kuna milizamu ya maji chumvi na maji baridi. Hapa Zanzibar pia kuna sehemu kunachimbwa mchanga, basi unapakiwa mchanga unachuruzika maji mpaka unakwenda unakofika yanabadilika yanakuwa mabwawa. Kwa bahati nzuri tukichimba hatujakutana na mlizamu wa maji ya chumvi, basi tukikutana nao sehemu ile itapotea na sehemu nyengine zitapotea.

Mhe. Mwenyekiti, jengine wenzetu wanafukia bahari ili wapate ardhi kubwa zaidi kwa sababu ya *population* za watu zinaongezeka na mahitaji yanaongezeka ya ardhi, sisi hatujafanya hivyo. Sasa matokeo yake wale wanaofukia ardhi maji yale yanakimbia sasa yanakuja kwetu. Sawa sawa na ukawa na bakuli ukalitia jiwe maji yataporomoka, yatatafuta pahala pepesi ambapo hapahifadhiwi yanakwenda kubomoa, hatari inatukabili visiwa. Kuna visiwa huko vya Kiribati vimeshazama na kama vimebaki basi ni kidogo sana na wito wa *UN* ilikuwa ni kuwaondoa watu kule wasiishi tena kwa sababu saa yoyote kinaweza kuzama kabisa. Mwenyezi Mungu atupishe mbali na majanga haya.

Kwa hivyo mimi ninachoshauri ni kwamba tujitahidi jamani ardhi tuilinde na tuzuwie sana. Hata yale mashimo yaliyochimbwa tuyafukie, lakini zaidi ya yote tuilinde ardhi na sisi kwa kuifukia tuna-*reclaim*. Sasa hivi sisi ukichukua idadi ya *square meter* au *square kilometre* ya miaka ya nyuma iliyopita huko na ukachukua sasa hivi sidhani kama *research* hiyo imefanywa, utakuta ardhi imepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hivyo ni lazima tuirudishe. Naomba mikakati maalum na nashauri mikakati maalum ipangwe ili tufukie baadhi ya zile sehemu so zilizokwishavamiwa na maji na tufukie sehemu nyengine ili tupate ardhi tujenge, tulime na

kadhalika. Hapa ni kwenye ardhi sitaki kuendelea sana maana masuala ya ardhi kwa kweli ni makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, niingie moja kwa moja kwenye maji. Mhe. Mwenyekiti, nasema siku zote maji ni uhai, kila kitu ni kipaumbele lakini maji ni uhai. Hata Dini zetu zinasema hata ukimnyima kuku maji basi wewe una dhambi. Maji tuliyokuwanayo Zanzibar tumeanza kuyatumia tangu miaka ya nyuma huko, tumechimba visima, tumefanya nini, maji yakitumika na hata mafuta yakichimbwa, visima vyengine vinakauka maana yake maji yanapungua.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja tulitembelea kule Mtopepo chini kule mtoni, kina cha maji sijui kilikuwa sijui *centimetre* ngapi juu, sasa hivi kiko chini. Maana yake yanatuta au yanakauka, kwa Kiswahili cha kishamba huko yanatuta, yanakauka. Sasa kama yanakauka maana yake nini, yatakwisha. Kwa hivyo nashauri sana Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wafanye utafiti wa makusudi ili kujua matumizi gani, ni kiasi gani tunatumia na kwa miaka mingapi tunatumia kiasi hicho, na kiasi gani kinapatikana kinazalishwa ili tuweze kutafuta mbinu mbadala za kupata maji. Maji baharini yapo, mkondo huo hapo wa kuelekea Dar es Salaam, tunaambiwa kuna *billions* za lita za maji ziko ndani ya bahari, zinataka zitumiwe tu. Kwa hivyo, nawashauri wayatumie maji haya. Huu upungufu wa kila siku unakujaje na wakati tunazungukwa na bahari, tunaweza tukaichuja tukapata maji, tuna maji ndani ya bahari huko tunayakama haya haya yaliopo huku nchi kavu yanazidikwisha. Nadhani sasa hivi tuandae mikakati ya makusudi ili kulitatua hili tatizo la maji.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu sasa nagusia kuna kadhia ya maji. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni mwenzangu sana, nilionana naye siku moja nikamwambia kuna watu wamechimba visima au Mwakilishi aliyekuwa pale

alichimba visima wakati ule kwa msaada wa Ali Yussuf, visima vile hajaja kuniambia mimi lakini nadhani anasema ni vyake, kapewa msaada na Ali Yussuf rafiki yake. Matokeo yake, hayo sio neno, lakini ule ubaguzi wa maji wanaoupata watu wetu, baadhi ya watu wetu wanakosa maji hawayapati. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aziangalie zile barua nilizompa kutoka kwa hawa wahusika wanao-*claim* kwamba yale maji ni yao binafsi kwa sababu wamesaidiwa, azitizame halafu hatua za kisheria zichukuliwe. Visima vyote ninavyojua mimi, ikiwa vya binafsi au vikiwa vimechimbwa na serikali vyote ni mali ya wizara hii. Sasa waende kwa makusudi wakavichukuwe visima viwe chini ya *ZAWA*, tuone kutakuwa na malalamiko. Nashauri sana hatua hii ichukuliwe haraka sana ili kuepusha malalamiko kule, kuna malalamiko. Kuna baadhi ya sehemu kwa kipindi cha miaka ya nyuma hazikufika *pipes* za maji kuna hivyo visima, tunajitahidi kulaza mabomba lakini ni maeneo makubwa hatuwezi kuyakamilisha kwa milioni 20 tunazopewa uzigae kwa barabara, uzigawe kwa maji na uzigawe kwa mambo mengine hazitoshi. Kwa hivyo tunashauri sana visima vile vitumike vizuri na vitumiwe na jimbo watu wote wapate, kusiwe na siasa ndani ya maji, maji hayana siasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naondoka kwenye maji, kadhia ya maji bwana ni kubwa. Lakini kabla sijaondoka kwenye maji nasema tuna visima viwili Mtopepo. Visima hivi vimechimbwa na Ras el Khaimah, kimoja tumeshamaliza kufanya kila kitu, tumeshaweka umeme kila kitu tunasubiri *pump* ili watu tuwape maji, *pump* hiyo hatujaipata. Tuliambiwa mwanzo kabisa siku hizo tayarisheni *pump* yenu ipo, lakini mpaka leo *pump* ile hatujaipata. Mhe. Waziri, nakuomba sana kama mwenzio, nakuomba tuipate ile *pump*. *(Makofi)*

Lakini jengine kuna kisima cha pili Ras el Khaimah kiko kule Welezi juu kwa ajili ya Mtopepo. Mhe. Mwenyekiti, tumetoa pesa

kijengwe kibanda, kibanda kile hakikujengwa. Tafadhali Mhe. Waziri fuatilia kibanda chetu kijengwe kwa pesa zetu zile zile, wakisema kuna zaidi basi tutaongeza, lakini kibanda kijengwe mtuletee na *pump* kule ili tuondowe matatizo ya maji Mtopepo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii sipendi niiseme sana maana yake nitakuwa najisema mwenyewe, nimekuambieni Waziri ni mwenzangu sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja kwenye umeme. Siku zote kuna lile bango lao linasema tuna ng'arisha eeh, silikumbuki lakini bango lile linasema tunang'arisha, huduma za kung'arisha, kwa hivyo jiunge na umeme ili upate kung'arisha maeneo yako. Ni kweli kabisa umeme tunautumia hata kwa biashara, wanaotengeneza malai, wanatumia umeme, wanaotengenza juisi wanatumia umeme, anayehifadhi aliyenunua kisamaki chake ili asikitumie chote anahitaji umeme akihifadhi ili kesho aweze kukitumia. Sasa kuna kuzimika mara kwa mara kwa umeme. Mimi sizungumzii madeni, madeni yameshazungumzwa sana walipwe madeni yao. Lakini nasema wazidishe bidii kwa watu kupata umeme, umeme unaweza kuzimika leo hapa jambo dogo sana basi ukakaa siku tatu hujaupata. Kwa hivyo wajitahidi sana ili umeme upatikane kwa wakati, huku kuzimika kwa mara kwa mara kunasababisha kuharibika kwa vyombo vingi vya umeme na hakuna malipo yanayopatikana kutokana na maharibiko yanayotokea kwa shughuli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nawashauri kwamba matatizo yanayotokea mara kwa mara huko unakotokea umeme. Sasa nawashauri kwamba hebu wafanye kama Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kuna ma- *Extension Officer* mabwana shamba huko vijijini, hebu na huku kunakotumiwa umeme tuwaweke hawa *Electricity Officer,* nafikiri wataitwa *Electricity*

*Officer* au mtawaita vyovyote vile, lakini wawekwe huko vijijini ili wahudumie, pakitokea tatizo litatuliwe kabla halijaleta athari, hiyo itapunguza kuchelewa kuzimika kwa umeme.

Sasa naondoka kwenye wizara hii kwa kusema kwamba changamoto zote zilizoainishwa....

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, muda wako unamalizika.

**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi:** Hata sijaingia wizara nyengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ndio, muda haukusubiri.

**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Changamoto zilizoainishwa naomba sana zitatuliwe. Halafu kwenye usafiri. Daa! kuna usafiri wa nchi kavu sikupata kuzungumzia, kuna baharini, kuna angani yote hayo nilitaka kuzungumzia, halafu pia kuna majenzi na nyumba pia nilitaka kuzungumzia. Lakini nikiyataja haya nafikiri mmeshafahamu nafikiria kusema nini juu ya haya wenzangu wapo, kwa hivyo sitoyasema muda umekuwa mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, nawashauri sana Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Balozi Ali Abeid Karume nakuomba sana tuwekeeni mabango kwenye barabara zetu, bango la njia hii inaitwa nini, halafu kilomita ngapi inakwenda, hata kwa watalii itasaidia kwa sababu kama hujui njia hii inakwenda Pwanimchangani, ukiona bango hii Pwanimchangani basi utajua hii inakwenda Pwanimchangani utaifuata uwende Pwanimchangani. Halafu *speed limit*, hizi *speed* zinazokwendwa wakati mwengine zinakwenda *speed* kubwa, tuweke *speed limit*, ikiwa ni kilomita 20 kwa saa basi iende kilomita 20, kwenye 60 ende kilomita 60 akifanya kosa basi ahukumiwe.

Michango ni mingi Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa imani yako ya kunipa nafasi hii ya kuchangia. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa anafuata Mhe. Suleiman Makame Ali na baadae atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Shaib Said Ali ajitayarishe.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia ripoti hii ya kamati ya Ardhi na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia kwanza niwapongeze Mawaziri wa wizara zote mbili, ikiwemo Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji chini ya Mhe. Waziri Balozi Ali Karume. Vile vile niwapongeze watendaji wa wizara zote hizi mbili. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze pia Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wake, akiwemo Mhe. Khadija Omar Kibano wa Jimbo la Mtambwe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hii Kamati kusema kweli imekwenda kuona mambo mengi na hawakuyaficha, wametuletea ili kuweza kuyafanyia kazi. Tutaweza kuyachangia na mengine nina imani kwamba yote yatafanyiwa kazi na wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 11 kwenye Mahakama ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi wanakabiliwa na changamoto nyingi. Ni kweli hata mimi nimeshawahi kwenda kule Pemba ofisini kwao pale Machomanne, nikawakuta hata ile kompyuta ni tabu kusema kweli. Kompyuta moja hiyo hiyo inatumika na ofisi nzima. Kwa hivyo inakuwa wanasubiriana, sijui niseme kwa lugha gani hata iweze kufahamika, yaani wamepanga foleni

wasubiri kwamba aondoke yule akae mwengine aweze kutekeleza shughuli za kazi pale.

Pia Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasemea hawa Mahakama ya Ardhi, pia niende kwenye masuala mazima ya utoaji haki. Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ndio ndio kila kitu, ikiwa Mahakama ya Ardhi au Mahakama yoyote, ni lazima tujitahidi kuwa wakweli hasa katika roho, nafsi ili kutenda haki kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi nasema kwa Pemba lakini sio Pemba tu nina imani hata hapa Unguja yapo. Mhe. Mwenyekiti, wanajitahidi sana lakini wana mambo wakati mwengine ya kusikitisha. Wale wanaostahiki kupewa zile haki zao kwenye masuala ya ardhi hufika mpaka wengine wakanyimwa, pengine mayatima wanakoseshwa haki zao. Kwa kuwa kuna mtu ana pesa, anatoa pesa tena inakuwa wale wengine wanasahauliwa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine masuala haya ya ardhi yanakwenda mpaka maeneo ya serikali, linajulikana kwamba hili ni eneo la serikali, lakini sasa Mahakama ya Ardhi hawafanyi utafiti ili kwenda kupeleleza wao wanatoa hukumu tu. Pengine lile eneo ni la serikali wanasababisha migogoro mikubwa sana katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, haya yapo kwa Unguja na Pemba, nina imani kati ya Wajumbe wote waliomo humu katika Baraza lako tukufu wa majimbo, sifikirii kama kutakuwa kuna Mwakilishi aliyekuwa hajaguswa na tatizo hilo kwa njia moja ama nyengine. Kwa hivyo nawaomba sana Mahakama ya Ardhi watowe haki kuhakikisha kwamba wananchi wanawapatia haki pale panapostahiki. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niliishauri Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira juzi hapa ili kuhakikisha kwamba yale maeneo

yaliyowazi ili kuondoa hii migogoro ya ardhi, basi ni kupimwa hususan yale ya serikali, yapimwe ili yajulikane yatambulike, hii migogoro ndio itapungua.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, licha ya hivyo nathubutu kusema kwamba hii migogoro ndio itapungua lakini Mhe. Mwenyekiti, licha ya hivyo nathubutu kusema kwamba watu wataendelea kugombana mwishowe watafika kuuwana, kwa sababu haya tunashuhudia. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Mahakama ya Ardhi Unguja na Pemba, kwa kila Mkoa basi kuhakikisha kwamba wanatoa haki kwa pale inapostahiki na pia vile vile kuwapa haki zao wale wanaodai. Mhe. Mwenyekiti, watende haki hiyo na wasiwe wabadhirifu kusema la ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Idara ya Mipango miji na vijiji. Hii Idara ya Mipango Miji mara nyingi nithubutu kusema kwamba inafanyika kwenye Wilaya za mjini mjini, huko vijijini watu wanajijengea wanavyotaka wenyiwao, ardhi Zanzibar hatuna ardhi ya kutosha hata hivyo. Lakini kama hii mipango miji na vijiji iko vizuri basi tuna uwezo wa kujenga nyumba vijijini kwa mipango mizuri na tukapata maeneo mengine yakawa ya ufugaji na kilimo. Kwa hivyo naiomba sana kwenye Idara hii ya Mipango Miji wahakikishe kwamba wanashuka mpaka huko vijijini, kuhakikisha kwamba wanatoa taaluma na wanapanga vizuri ili kuhakikisha kwamba maeneo haya mengine yanabakia kwa shughuli za kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakupa mfano ninaowajua kwa Mhe. Makame Kojani ikiwaka nyumba moja moja pale hazibakii, lakini sio Kojani tu hata jimboni kwangu Ziwani watu wanajenga visivyo utaratibu. Kwa hivyo naiomba sana sana Idara hii kuhakikisha kwamba pale wanapotoa vibali vya ujenzi na hata walipokuwa hawajatoa vibali vya ujenzi wafuatilie kuhakikisha

kwamba watu wanapanga vizuri, wanajenga vizuri na sio kujijengea wanavyotaka wao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa kumi na tisa Mamlaka ya Maji Zawa. Hapa ndio penye hicho kishindo, wengi wanailalamikia Mamlaka ya Maji lakini pia tunaipongeza Mamlaka ya maji. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji ukiangalia kiundani wana madeni wanayaleta sehemu za Serikali na taasisi binafsi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapo tunapokwisha kuwatetea Mamlaka ya Maji, hebu mimi nataka nijue kuna taratibu gani zile za miradi ya maji kama mfano miradi kutoka kwa Wachina wale na sehemu nyengine, kama miradi iliyokuja kutoka Oman ya Ras El Khaimah. Pemba kuna miradi ya maji iliyofadhiliwa na Wachina kwangu mie Ziwani ambapo ninapatikana jimbo lile la Ziwani Shehia ya Ndagoni na Shehia ya Wesha na vitongoji vyake. Mhe. Mwenyekiti, tangi lile limegharimu mamilioni ya mapesa lakini maji hayatoki mpaka ikabidi mimi Mwakilishi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji nawashukuru sana, nilisimamia mpaka kuhakikisha kwamba Ndagoni wananchi wanapata maji, kwa sababu bila ya maji Mhe. Mwenyekiti, hata humu Barazani sifikirii kama tungekuja.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya maji hata mtoto anakushinda maji ni muhimu sana. Kwa hivyo nawaomba sana Mamlaka ya Maji hususan kwanza wanapopata miradi wasiripue ripue, ilikuwa tumetoka kwenye miradi ile ya visima kimoja kimoja kila Shehia tumekwenda miradi ya kijumla ya matangi ya maji. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nithubutu kusema yamerudi pale pale. Mhe. Mussa Foum alisema kwa upande wake wa Kiwani, lakini na mimi nasema kwa upande wangu wa Ziwani. Nilimsikia Mhe. Raza hapa akisema kwamba kila mmoja akitaja lake itakuwa hatwishi, lakini bila ya kutaja langu na Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo akataja lake, Mhe. Jaku akataja lake, Mhe. Mussa Foum akataja

lake kwenye jimbo lake, hizo changamoto zitajulikana hazijulikani.

Kwa hivyo naomba sana kwamba hizi changamoto tuziseme kila anayekabiliwa na changamoto aseme lakini pia naiomba sana Mamlaka ya Maji kuhakikisha kwamba zile sehemu zote zinazomwagika maji basi waende, kuzizuie sehemu zile tuzidhibiti na kama kutakuwa kuna watu wanafanya makusudi wachukuliwe hatua yoyote wanayoijua wao. Kwa sababu yawezekana maji yanafika sehemu moja sehemu nyengine hayafiki kwa mabomba kupasuliwa. Kwa hivyo naiomba sana Serikali kupitia Mamlaka ya Maji hili suala walisimamie na pia nawaomba wananchi kwamba wasifiche ushahidi kwenye hili, kwa sababu wanaoathirika ni wao. Kwa hivyo naishauri sana Mamlaka ya Maji kuhakikisha kujitahidi kuhakikisha wanawapatia wananchi maji, maji ni muhimu sana katika maisha ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Shirika la Umeme kwenye ukurasa wa 22. Nawapongeza sana Shirika la Umeme kwa kutugharishia lakini Shirika la Umeme baada ya kuwapongeza na wao niwape changamoto zao kidogo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nadir alizungumzia hapa kwamba unataka ile nguzo mpaka utoe milioni mbili. Hilo ni kweli na mimi mwenyewe yameshanifika haya. Kuna tatizo gani kwamba mwananchi yule anataka kulipia umeme mwezi hadi mwezi au siku hadi siku, lakini gharama inakuwa kubwa, mpaka inafika kwamba anashindwa kuungiwa umeme. Siku nyengine anatoa laki tano, siku nyengine laki sita, laki nne hamsini, ni gharama kubwa sana. Kwa sababu kutia umeme ninaweza kusema sio shida lakini shida ni hiyo kulipia sasa, ukifanya hesabu kwamba miaka yote utakayoishi duniani yeye anatumia umeme analipia, kwa hivyo ile gharama ile inarudi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naomba sana kuhakikisha kwamba wawapunguzie wananchi wawapunguzie kwenye hili suala la kuunga umeme kwa sababu wananunua umeme kila siku, naomba sana sana kuhakikisha kwamba Shirika la umeme linawapunguzia lakini vile vile wasiwasumbue inafika siku nyengine mwananchi anaunga umeme anakwenda miezi minne au mwaka mzima umeme haupati mpaka atoe chochote, tutafika wapi Mhe. Mwenyekiti, hatufiki. Kwa hivyo naomba sana na watu wa Shirika la umeme nao wawe waadilifu kwenye hili mtu analipia umeme pesa walizotaka wenyewe halafu inakwenda tena mtu anahangaika mpaka anamtafuta Mwakilishi kwenda kumsaidia. Naomba sana kuhakikisha kwamba Shirika la umeme watimize wajibu wao.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 30 kuhusu sekta ya mazingira. Mazingira nayo ni muhimu. Niwaombe sana kwanza niwashukuru sana watu wa Mamlaka ya Mazingira wanavyosimamia vizuri na walivyodhibiti misumeno ya moto. Kama sio juhidi zao na juhudi za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, nawashukuru nao pia nadhani ingelikuwa miti yote imeshalala. Maana Mhe. Mwenyekiti, mnazi ilikuwa ikiuona msumeno wa moto unalala wenyewe bila ya kufikwa. Kwa hivyo ingelikuwa sasa hivi tunaendea kwenye jangwa, kwa hivyo nawashukuru sana kwa jitihada hizo.(*Makofi*).

Lakini niwaombe sana watu wa mazingira kwamba pale ampapo kwamba panatakikana kufanyiwa jambo kama kufukia bahari kama pale Tibirinzi. Mhe. Mwenyekiti, bahari ina sifa moja, ukiifukia hapa basi inatoboa kwengine, wewe ulikuwa shahidi. Tibirizi pale mpunga ulikuwa humu, sijui niseme humu kwa nani kupita kwa kimo humu Barazani labda Mwalimu Haruna, mpunga pale ilikuwa Mwalimu Haruna hawezi kuukamata lakini sasa hivi Tibirinzi yote watu hawalimi tena waliohamia ni kaa dondo kama unawajua Mhe. Mwenyekiti, na nina imani unawajua kaa dongo,

eneo lile la Tibirinzi wakulima wangapi wakifaidika. Sasa hivi hakuna mkulima hata mmoja Tibirinzi anayefaidika na sio Tibirinzi tu na hata sehemu nyengine tu kama katika jimbo langu kule Ndagoni Kambanga na sehemu nyengine kule Michngwani na sehemu nyengine kama Wesha. Watu tayari suala hili la chumvi linawaathiri kwa sababu tatizo ni hilo kwamba chumvi inazuiwa huku inakwenda sehemu nyengine. Kwa hivyo niwaombe sana watu wa mazingira wanapodhibiti masuala hayo na wanaposimamia haya wawe makini sana ili kuhakikisha kwamba mazingira hayaathiriki na zile sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Shirika la Nyumba Zanzibar ukurasa wa 36, kuzienzi nyumba za maendeleo ni kuenzi juhudi na jitihada na hekma za Mzee wetu Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, kuzienzi nyumba zile. Mhe. Mwenyekiti, pale Madungu nyumba zilikuwa zipo hali mbaya lakini sijui niseme mradi niseme, sijui pesa zimetoka Serikalini zimefanyiwa marekebisho kama nyumba mbili moja haikwisha, lakini zile nyumba kwa anayetoka Dar es Salaam akienda sasa hivi pale atajiuliza hii nyumba imejengwa kipande hapa, ile nyumba nzuri. Kwanza nimshukuru sana kwamba aliyesimamia suala lile lakini mimi nikitaka kujua kwamba hizi pesa zilikuwa zimeshakwisha, maana mpaka leo hakuendelei chochote. Kwa hivyo naomba sana ili kuzienzi juhudi na jitihada za Mzee wetu, Muasisi wa Mapinduzi basi na zile nyumba zienziwe, ziimarishwe na kila wakati ziweze kung'ara ili vizazi vyetu na vitukuu na vinying'inya waje kuona nyumba zile na kuhakikisha kwamba kweli Mapinduzi ya Zanzibar yaliasisiwa na mtu mashuhuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwen Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye …

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**Mhe. Makame Suleiman Ali:** Aaka! Mhe. Mwenyekiti, samahani nigaie dakika moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakupa dakika moja umalizie.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ninakupa dakika moja umalizie.

**Mhe. Makame Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, itakuwa sijawafanyia haki wananchi wa Pemba hususan wanaofanya kazi katika utunzaji wa uendelezaji wa barabara, ni shahidi wewe mwenyewe Pemba kulitokea maafa ya barabara ilikuwa kama wewe uko Konde huwezi kufika Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwezi wa tano wa sita wa saba wa nane watu wale wako kazini usiku na mchana wakifika majumbani kwao watoto hawawajui walivyolala, wanaingia ndani saa saba za usiku wanatoka saa kumi za usiku. Lakini cha kushangaza kulipelekwa pesa pale kwa ajili ya kulipwa wale *over time* yao, mpaka leo hii nikikwambia Mhe. Mwenyekiti pesa ile hawajaipata. Afisa Mdhamini yupo hapa ananisikia, akiulizwa anasema mimi ninagrisi, hata mkisema nyinyi ni kazi bure. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kwenda hivyo, lazima tuwasemee watu, tuwatetee na Mhe. Mohammed Ahmada anakiri hilo. Mimi nataka nijue, hii pesa imekwenda wapi, tunaopitisha pesa ni sisi, wale wafanyakazi wapewe haki yao, zile pesa wapewe ni pesa zao. Juzi alisema kama wanataka kuziba viraka. Eeh! Mhe. Mwenyekiti, hicho kiraka na njaa kitazibika, si watatuondosha njiani tu wale, kesho barabara inachimbuka vile vile.(*Makofi*).

Naomba sana kama pesa ile ilitoka basi ni kwamba pesa ile wapewe wahusika Mhe. Mwenyekiti naunga mkono ripoti hii asilimia kwa mia, na mimi naomba sana na kusisitiza hayo tuliyosema tunashauri yafanyiwe kazi ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe sasa ninamuita Mhe. Asha Abdalla Mussa, akifuatiwa na Mhe. Shaibu Said Ali na Mhe. Ali Khamis Bakar ajitayarishe.

**Mhe. Asha Abdalla Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii niweze kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wajumbe wengi wamechangia ripoti hii na kila Mjumbe anayesimama hapa tatizo ni maji, barabara na umeme. Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba kamati hii ya Mawasiliano ambayo imekwenda kufanya kazi katika maeneo husika na ikagundua changamoto mbali mbali na hatimae kutuletea wajumbe hapa, naamini kwamba Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wa Wizara hizi watayachukua na mwezi wa tisa watakuja kutupa majibu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi lakini ninachotaka kuzungumziani changamoto ya Shirika la Umeme (*ZECO).* Mhe. Mwenyekiti, wananchi wana malalamiko mengi wanapokwenda kutaka huduma ya umeme ambayo wanataka kuungiwa umeme wanafanya malipo pale na baadae wanakaa muda mwingi yaani muda mrefu, lakini huduma ile wanashindwa kupewa kwa muda muafaka. Naomba sana Wizara husika isimamie na kuhakikisha kwamba wananchi wanapopeleka mahitaji yao basi waweze kufanyiwa kwa haraka.

Lakini pia hapo mwanzo kulikuwa na mita zile za mwanzo kwa sasa kuna mita za *TUKUZA*, kwa kweli kuna changamoto kubwa katika mita hizi, wananchi wanalalamika sana kwamba wanaambiwa watoe mita za zamani lakini wanapokwenda kuungiwa mita za *TUKUZA* basi wanakuta wamewekewa na deni juu yake. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba Wizara husika

wakiletewa basi matatizo kama haya au malalamiko haya wafuatilie, malalamiko haya ni mengi na madeni wanayoyakuta katika mita hizo ni pesa nyingi sana, naomba sana Wizara husika ifuatilie changamoto hizi, naamini hapa katika majimbo mengi yapo malalamiko haya kwa hivyo naomba sana wafuatilie kwa karibu.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Wizara ya Ujenzi. Tatizo la barabara ni tatizo sugu katika maeneo yetu yote zikiwemo barabara za ndani ambazo zipo katika serikali za mitaa, lakini barabara zile ambazo zipo barabara kuu, naomba sana Wizara husika, changamoto zilizotajwa humu na nyengine ambazo hazijawekwa kwenye ripoti hii. Naomba sana musikilize vilio vya wananchi ambavyo na sisi tunaweza kusimama hapa na tukawatetea na tuwakesea, naomba Wizara husika iyafanyie kazi na baadae wananchi waweze kufaidika na matunda haya.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Mamlaka ya Maji (*ZAWA),* kwa kweli mpaka sasa sisi viongozi tunajiuliza na tunasikitika hizi pampu zinazowekwa katika vituo vyetu vya maji zinafika pahala hatupati jibu, pampu inaweza kuwekwa mwezi huu wa Febuari ikifika mwezi wa Machi pampu haifanyi kazi au imeungua tatizo ni nini. Tunaomba sana Wizara husika ifuatilie na tuone kwamba haya matatizo au changamoto zinaondoka kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja nikushukuru.(*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakupongeza sana. Sasa namuita Mhe. Shaib Said Ali akifuatiwa na Mhe. Ali Khamis Bakar na Mhe. Omar Seif Abeid ajitayarishe.

**Mhe. Shaib Said Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kukutana hapa jioni hii, tukiwa wazima na kuendeleza majukumu yetu kama tulivyopangiwa. Awali ya yote niwapongeze Mawaziri wetu wa Wizara hizi jinsi wanavyofanya kazi zao na leo hii tumepata changamoto kidogo katika Wizara zao baada ya Mhe. Hamza Hassan Juma hapa na kamati yake kutembelea na kuzama kabisa na kuibuka na haya ambayo wametuletea hapa nashukuru sana.

Baada ya hayo ili mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nianza katika ukurasa wa 15 suala la Msajili uhaba wa wafanyakazi. Tunajua kwamba ardhi ndio mali ya wananchi wetu wa Zanzibar na ardhi Mwenyezi Mungu katujaalia kwamba haikui kama yanavyokuwa maji ndani ya chombo, kama anavyokua binadamu, ardhi iliyopo ndio iliyopo lakini watumiaji wake wanakua na hususan Wazanzibari, kwa sababu Mwenyezi Mungu katujaalia kwamba hatuna miiko ya uzazi. Kwa maana hiyo ardhi inabakia lakini watu wanaongezeka. Sasa kuhusiana na masuala ya kwamba ardhi hii haitasajiliwa kutakuwa na uhaba wa wafanyakazi ambao watashindwa kuisajili ardhi hii, sijui vizazi vyetu baadae vitaelekea wapi. Kwa hivyo mimi namuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuongeza ajira na wataalam katika Wizara hii ili ardhi yetu isajiliwe na iweze kupangwa vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo katika kifungu hicho hicho nije katika uelewa mdogo wa mirathi. Mhe. Hamza Hassa Juma hapa sijui alikwenda kwendaje mpaka hichi kipengele akakiingiza huku, lakini na sisi kule kwetu kuna msemo kwamba ”ibwavo ndio ichinjwavyo”. **K**wa maana hiyo madam kakiingiza hichi na sisi, itabidi tuchangie. Mheshimiwa ni kweli kwamba kuna uhaba mdogo wa suala la mirathi katika vijiji vyetu hususan vijijini. Vijijini wengi wanarithisha, Madiwani wanarithisha, Masheha wanarithisha, wataalam wanarithisha, watu maarufu wanarithisha,

masuala haya yatapelekea vurugu kweli kweli katika wakati wa mirathi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, suala la mirathi tunasema kwamba wanawake tunawazalilisha katika masuala ya ndoa hususan tunavyowaacha, tunawaachia mzigo mzito. Lakini na moja katika suala ambalo linawadhalilisha wanawake wa vijijini ni suala la mirathi. Mhe. Mwenyekiti, vijiji ardhi inarithiwa bila ya wao kushirikishwa wanawake, anaambiwa tu anapokuja akadai ardhi yake watu baada ya kurithi, anauliza yangu iko wapi, anaambiwa yako wewe imekatwa na mama yako sehemu fulani lakini haonyeshwi, wala hapewi wapi watu wamerithi. Kwa hivyo kipengele hichi Mheshimiwa namuomba Waziri kwamba alete utaalamu, apeleke utaalamu vijijini kuhusu masuala ya mirathi hususan vipande vya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika ukurasa wa 17 kifungu cha (2) uhaba wa wataalamu katika Idara ya Mipango Miji. Haya ni masikitiko makubwa, tunaona watu jinsi wanavyojenga mpaka kwenye makuburi watu wanajenga, vianzio vya maji watu wanajenga, kwenye misitu yetu ya kitalii watu wanajenga. Kama mpaka leo kutakuwa bado kuna uhaba wa wataalamu kuhusu mipango miji sijui tunakwenda wapi. Namuomba Mhe. Waziri masuala haya ni changamoto ambazo zinataka ufumbuzi wa haraka sana kwani ardhi ndiyo raslimali yetu na hatuna pengine pa kwendea.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kwenye ukurasa wa 19 Mamlaka ya Maji, naamini kila Mwakilishi atakayesimama hapa naamini hichi ndio kilio chake kikubwa sana. Kama kuna nyimbo ya kuimbwa basi wananchi wa hapa wangeimba maji! Maji! Maji! Hakuna Mwakilishi atakayesimama hapa akasema kwamba mimi jimbo langu linaunafuu wa maji. Ikiwa kazi hizi tutapewa sisi

Wawakilishi tuangalie mpaka leo hii fedha ambazo tunasaidia majimboni hatujapewa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, licha ya uhaba huu wa maji uliomo katika vijiji vyetu, lakini pia sijui niseme nini, wala sijui nitumie neno gani, nikisema uzembe itakuwa siyo vizuri, nikisema kuna watu maalum ambayo wanataka haya masuala yasiendelee itakuwa siyo vizuri. Sijui nitumie lugha gani mpaka niseme hivyo. Mimi niseme katika jimbo langu moja pale Pujini, kuna tenki moja kubwa sana tumejengewa na Machina. Tenki hii tulikuwa tukipata maji eneo lote la Pujini, tukiwapa wenzetu kuna kijiji kinaitwa Matale, kuna kijiji kinaitwa Mwine, Chanjamjawiri, wote walikuwa wanatumia maji hayo kutoka na tenki hiyo moja kwa ukubwa wake walikuwa wakipata maji. Tenki hiyo hivi sasa niseme sijui imeachiwa au sijui imefanywa vipi, imekufa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, masuala kama haya ya ufatiliaji na kuona kwamba wapi ingekuwa maji sehemu nyengine tunapata bila ya wasi wasi. Kutokana na hayo hususan maji watu wa eneo hilo wanapata kwa mgao na siku nyengine hawapati kabisa. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri kwamba lile tenki la maji la pale Pujini/Tondooni alifanyie ukarabati angalau watu wa maeneo yale wapate maji.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika ukurasa wa 22 katika sekta ya umeme. Nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi alivyotuletea maendeleo katika vijiji vyetu. Hivi karibuni nimshukuru kwa dhati kabisa Balozi Ali Karume alipokwenda kunifungulia umeme katika Kijiji changu cha Pujini kinaitwa Mtimbu. Nimshukuru kwa dhati kabisa na wananchi wanakupa salamu zao sana za dhati kabisa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata hivyo bado suala la umeme wanaposambaza umeme kuna manung'uniko makubwa sana kwamba nguzo zinapowekwa wananchi bado huwa hazijawafikia. Kwa hivyo mimi naomba suala la kusambaza umeme basi na zile nguzo wasogezewe wananchi karibu, kwa sababu zinawekewa tu pahala lakini bado kuna nyumba fulani mpaka wavute umeme ule. Namuomba Mhe. Waziri kwa dhati kabisa kuna kijiji changu kimoja kinaitwa Limani. Kijiji hichi kina ahadi ya Mhe. Rais kwamba kitapelekewa umeme, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri akiangalie kijiji hichi na hii ahadi aweze kuitimiza. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika Wizara ya Mawasiliano ukurasa 35 kifungu cha 4, hapa pana ushauri wa Kamati inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, ushauri wa kuuzwa kwa meli ya MV. Mapinduzi II. Meli hii ikiuzwa sijui tutakwenda wapi na sijui tutasema nini. Ninaloliomba mimi kwa Waziri achunguze Mheshimiwa ile meli ina matatizo gani, imeingia nini, kuna kidudu gani kinachosababisha mpaka meli ile siku ipo Pemba, siku ipo gatini inasubiri matengenezo. Tunaizungumza meli hii kwa sababu ndiyo meli ambayo inayowasaidia wananchi wetu wa Zanzibar hususan kisiwa cha Pemba na ndiyo meli ambayo tunaiamini kabisa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikuthibitishie kwamba hii meli hizi meli nyengine zilizobakia wananchi wanapanda tu, kwa sababu hawana vyombo vyengine vya kupanda, lakini kama meli ile itafanya kazi hususan basi naamini kwamba vyombo vyengine vyote vitalala. Nimuombe Mhe. Waziri ile meli isiuzwe, kama kuna utaratibu wa kufanyiwa meli ile mpaka ikawa nzima ikaendelea na shughuli zake basi ifanyiwe. Hili nilisema hapa kwamba Mkoa wa Kaskazini kama kuna matibabu yafanywe kule na hii nayo itiwe kwenye suala hili, ipungwe kidogo na ile meli. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ni aibu kabisa kwa serikali yetu kwamba meli ile ni mpya na kuna meli hapa zaidi ya miaka 20 zinafanya kazi, lakini meli ile leo hata miaka mitano haijafika, leo meli inaharibika kila wakati, ni aibu sana. Kuna wenzetu hawa waliojificha, wao hutafuta sababu ndogo tu ikawa ndiyo kampeni yao kubwa sana. Mimi nakuhakikishia mwaka 2020 suala kubwa ni meli na maji, hakuna jengine. Tukiyaweza masuala haya mawili basi tumefunga midomo yao, lakini kama meli yetu ya MV. Mapinduzi II itapita leo, kesho ikifika ipo Mombasa, itakuwa ni sababu kubwa sana. Ile midogo tuliyoambiwa kwamba wamenunua meli mbovu isiyokuwa na maana, pesa zimeliwa yatatokezea hayo. Mhe. Waziri ajitahidi sana ili masuala haya yasitokezee.(*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa muda umemalizika, muda wako umemalizika,

**Mhe. Shaib Said Ali:** Mheshimiwa nikitoka hapo nije katika utunzaji wa barabara, kuna hizi barabara za ndani.

**Mhe. Mwenyekiti:** Muda umemaliza malizia kwa kufunga mchangio wako.

**Mhe. Shaib Said Ali:** Ahsante Mheshimiwa baada ya hayo naunga mkono hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Sasa namwita Mhe. Omar Seif Abeid akifuatiwa na Mhe. Ali Khamis Bakar.

**Mhe. Ali Khamis Bakar:** Naona umenitaja mimi mwanzo ndio Mhe. Omar Seif Abeid, lakini naona ukisha umegeuza vipi tena.*(Kicheko*/*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe kutokana kwamba wewe ulikuwepo mwanzo katika orodha lakini kwa sababu hukuwepo ndio nikakuweka nyuma, ndio nikafuata utaratibu ambao waliokuwepo katika Baraza.

Mhe. Omar Seif Abeid endelea na Mhe. Ali Khamis Bakar atafuatia.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya upendeleo ahsante sana. Mhe. Ali Khamis Bakar samahani ndugu yangu sote tuko kwenye jahazi moja hakuna tatizo, lengo letu moja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote mimi nachukua fursa hii kumshukuru Allah (SW) aliyetujaalia kukutana tena jioni hii kwa nia moja, kwa lengo la kuichangia hotuba hii adhimu iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Wenyeviti, kamati muhimu, kamati ambayo ni muhimili mkubwa wa nchi yetu ni kamati inayogusa uhai. Mhe. Mwenyekiti, sote tumo katika ardhi, sote tumo katika mawasiliano bila ya mawasiliano hatuwezi kufanya kazi zetu zikanyooka, bila ya ardhi hatuwezi kuishi, huo ni ukweli usiofichika. Katika hotuba hii iliyojaa mambo mengi mimi nataka niende kifungu kwa kifungu kama muda wangu ulivyo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naanza ukurasa wa 8 katika changamoto ambazo wenzangu wameanza kuzizungumza za upungufu wa utaalamu wa usimamizi na uthamini wa ardhi, mipango miji, uchoraji pamoja na ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi. Jambo hili ni tatizo kama kamati ilivyoliona. Mimi huwa nalizungumza mara nyingi wakati nikitoa maswali yangu, hata juzi pia nililizungumza suala hili juu ya upangaji miji na maendeleo ya vijiji. Jambo hili ni chukizo, jambo hili sasa ipo haja ya kulifanyia kazi tukaiondoa kabisa kadhia hii.

Leo ujenzi holela wa maeneo yetu umekithiri. Mhe. Shaibu kaizungumza, wengi waliotangulia wamezungumza lakini kama tunautizama upande mmoja tu. Hatuna wafanyakazi wa kutosha nani ataweza kumudu kufanya kazi hizo. Ushauri wangu na wito wangu kwamba suala la uwepo wa wafanyakazi wa kutosha ni la umuhimu, lipewe umuhimu wa aina yake, tuhakikishe kuwa wafanyakazi wanatosheleza katika Idara hii na wanapewa vitendea kazi vya kisasa ili likitokea tatizo tuweze kuwalaumu kisawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo jengine ambalo amelizungumza nalo ni kilio kikubwa, kuwepo kwa kwa mamlaka mbili tofauti za usimamizi wa ardhi za eka tatu. Jamani serikali moja, nchi moja, Idara inayosimamia ziwe mbili kwa kitu kimoja, tunakwenda wapi. Mimi nashauri ikiwa serikali imeamua kuyahamisha mashamba ya eka tatu kuyapeleka Wizara ya Kilimo wayahamishe yote wayapeleke Wizara ya Kilimo, ikiwa imeamua kuyabakisha Idara ya Ardhi iwape watu wa Idara ya Ardhi mashamba yote yabakie Idara ya Ardhi, isiwe nusu iko huku na nusu iko huku, jambo hili halitaleta taaswira nzuri. Hili litaweza kuleta hitilafu huko mbele kwa sababu wananchi wataweza kuhoji, wananchi tutawapa nafasi ya kutuhoji inakuwaje leo kwamba Unguja shamba za eka tatu wawe nazo Idara hii na jengine wawe nayo hawa. Nadhani hili Kamati wamelikuta na limeibuliwa katika ziara zao na ndipo wakalizungumza.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimelizungumza zamani hili, kwamba jamani ni vyema suala hili likaachiwa Idara moja, nikaambiwa kwamba Wizara ya Kilimo ndiko kwenye wataalamu. Sasa ikiwa Wizara ya Kilimo kwenye wataalamu hawa wataalamu wapo Pemba tu, Unguja hawapo wa Wizara ya Kilimo. Kama wataalamu wa Wizara ya Kilimo wapo basi mashamba yote yarudishwe Wizara ya Kilimo wapewe wataalamu wayafanyia kazi. La inaonekama kuwepo Idara ya Ardhi wataweza

kuyashughulikia vizuri mashamba wakaweza kuyatambua na kuyaendeleza kuyafanyia kazi, ni vyema yarudishwe Idara ya Ardhi na Mazingira Wizara ile yaweze kuyasimamia wakayapima, wakayajua uhalisia wake, wakayatengenezea hati, wakawakabidhi wanaohusika.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 9 na10, miongoni mwa changamoto ya Afisa Mtambuzi wa Ardhi aliyeteuliwa na Waziri kwa mujibu wa Sheria iliyoundwa na Kamisheni ya Ardhi kwamba hadi leo hajalipwa stahiki zake. Vipi mtu ataweza kufanya kazi kama hajalipwa pesa, vipi anaweza kuwa na ari ya kufanya kazi akiamini kwamba kazi ninayoifanya malipo yake ni hewa, hayapatikani. Si yeye, wala mimi, wala sote tuliokuwemo humu ndani, hakuna mtu anayekubali kufanya kazi isiyokuwa na malipo. Nasema haina malipo kwa sababu kumcheleweshea sio lengo, lengo ni kwamba anafanyakazi, analipwa kwa muda, hata sheria inatueleza sisi ya Dini kwamba mtu analipwa ujira wake kabla jasho halijakauka, analipwa kazi kwa ajili ya jasho lake alilolitoa analipwa kwa kazi yake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naishauri sana serikali, naishauri wizara, Waziri dada afanye bidii ahakikishe kwamba huyu mtu ambaye tumemteuwa kama Afisa Mtambusi anapewa haki yake kwa wakati, jambo ambalo litampa moyo wa utendaji kazi ambao utendaji wake kazi tunautegemea kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu, kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi, ushauri wake ni muhimu.

Mhe. Spika, lakini pia katika ukurasa wa 10 kuna kitu ambacho mimi nimeshawahi kukizungumza tena na leo kimejirejea cha minara ya simu kutolipa kodi. Kwa nini makampuni ya simu yanayofanya kazi kibiashara yanayopata faida kwa kila nyenzo yakawa hayalipi kodi. Mimi napendekeza lilokuwa kampuni iliyokuwa hailipi kodi ifungiwe, izuiliwe leseni ya kufanya

biashara. Sisi tunahitaji kodi, tunahitaji tupate pesa ziweze kuendesha serikali. Serikali haiwezi kuendeshwa bila ya kodi. Leo wao ukipiga simu unaambiwa kuna nyimbo huko, ukitaka kujiunga na wimbo huu bonyeza moja upate huduma ya nyimbo, unalipa au wanatoa bure, walipe kodi kwa nini wawe hawalipi kodi. Mhe. Waziri katika majumuisho ukija mwezi wa tisa utwambie ni muda gani hawajalipa na kiasi gani cha fedha wanachodaiwa ili Makampuni haya yawajibike kulipa kodi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika 12 ninakwenda kwenye Idara ya Mahakama. Idara ya Mahakama ni Idara ambayo tunaitegemea na leo ukitizama mrundikano wa kesi umeanza kupungua kwa kazi kubwa zinazofanywa na Idara hii ya Mahakama. Mahakama zetu za Ardhi zinafanya kazi kubwa. Mimi nakumbuka kipindi cha nyuma wakati inaanzishwa Mahakama ya Ardhi Pemba tulikwenda pale kukawa kuna kesi zaidi ya 700 za ardhi, lakini ndani ya kipindi cha miaka miwili kesi zile zikapungua mpaka zikaja 150 sijui 200. Nasema hivi kwa sababu nnajuwa kuna mzee wangu mmoja alikuwa ni *assessor* pale, alikuwa akiniambia mimi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa leo moja kati ya kazi zao ni kufanya *site visit* kama ilivyoonekana, lakini vipi wataweza kufanya *site visit* ikiwa hawana vyombo vya usafiri. Mhe. Waziri nakuomba sana kwamba tumeamua kuingia katika mpango huu wa kuanzisha Mahakama za Ardhi ambazo ni Mahakama zenye ngazi ya Mahakama ya Mkoa, ngazi kubwa za Kimahakama zenye maamuzi, lazima na ni wajibu kwetu siye kuwapatia usafiri, lazima tuhakikishe kwamba kwenye bajeti inayokuja tunaingiza kifungu cha kuwapatia hawa vitendea kazi vikiwemo vya usafiri. Mheshimiwa *page* ya kumi na saba, kumi na nane inazungumzia uhaba wa wataalamu. Idara hii inayosababisha kuzorota uhaba wa wataalamu kwa upangaji wa mji na vijiji. Lakini pamoja na uhaba

wao kama nilivyosema lakini wanatakiwa wawajibike uwajibikaji ni muhimu sana kwa watalamu wetu.

Ni muhimu nasema hivi kwa sababu gani, leo ukienda katika maeneo kama Konde ule mji una *master plan* toka miaka ya 1960, ukitafuta utaiona lakini maeneo yote ya mji wa Konde leo yamezibwa yale maeneo ya wazi kwa nini, na nilishawahi kwenda kuripoti kwamba jamani hebu fanyeni kazi mji hii sasa itapotea hadhi zake. Baada ya muda vizazi vyetu vitakuja kutusukubu sisi, tutaulizwa je, wazee wetu walikuwa hawaoni kwamba hali hii inaharibiwa na wao wakanyamaza wakawa wananyamaza.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi bado natoa ushauri kwamba suala la ujenzi katika miji yetu yote ya Unguja na Pemba, ni suala la lazima kulifuatia na kuhakikisha kwamba mtu yeyote anajenga kutokana na ramani ya eneo linalohusika na kama amefanya makosa basi apewe adhabu kwa ajili ya makosa aliyofanya. Leo kuna watu wanajenga majumba yao ndani ya *line* kubwa za umeme, lakini hakuna mtu wa kuwakemea. Athari ikitokea mwananchi yule atakufa, familia inapotoa, watu wanangamia. Sasa tusisubiri yakatokea majanga kama hayo. Sheria ya ujenzi wa kwenye *high tension* za umeme imeelezwa wazi maeneo yameainishwa lakini watu wanajenga ndani ya maeneo ya umeme mkubwa na watu bado wanaachiwa.(*Makofi*).

Mheshimiwa najua muda si rafiki lakini nataka niende kwanza kwenye Idara ya Mazingira. Mheshimiwa mimi nimezungumza sana suala la mazingira limenikumba mimi katika jimbo langu la Konde, eneo la bandari ya Msuka ni tishio watu wanalia. Mhe. Mwenyekiti, wewe ni shahidi ushawahi kutembelea au kama bado nakualika uwende ukatembee na uongozi wa serikali nawaomba waende, nishamuomba sana Waziri wa Tawala za Mikoa kuna kambi yetu pale ya KMKM, leo inaning'inia kwa maji ya chumvi, ilikuwa mita 300 au mita 400 bahari, leo zimebakia mita 20, bila

ya hatua za dharura kuchukuliwa suala lile baada ya miaka mitano itakuwa hadithi. Kwa hivyo naomba watu wa mazingira wende watumie wataalamu wao wakaliangalie eneo lile jinsi gani lilivyoathirika, wapate maoni ya wananchi wawaeleze kwa sababu ule ni mkanda mkubwa sana ulioathirika, kutoka maeneo karibu na Vumawimbi hadi Msuka ndani.

Mwisho nataka kuzungumzia suala la bandari na meli Shirika la Meli kwamba meli yetu Mhe. Shaibu kaizungumza na sisi sote tunaizungumza, tuiombe tu serikali kupitia wizara na Shirika la Meli wafanye uchunguzi wa kina ili kuweza kubaini tatizo hasa la meli kama alivyosema Mhe. Shaib. Suala la meli ile imekuwa ni gumzo kubwa sana mitaani, limekuwa ni gumzo ambalo halimalizi. Hebu tujitahidini kulifunga lile suala la gumzo la meli na tupate kuzungumzia jambo jengine kwamba sasa meli yetu imetulia ili watu wetu nao wapate kupumzika.

Mwisho kwa upande wa mawasiliano Mheshimiwa napenda kuizungumzia sana Shirika la Simu la *ZANTEL* kwamba huduma wanazozitoa haziridhishi. Mhe. Waziri tunataka tujuwe siye serikali ina *share* Shirika lile la simu la *ZANTEL*, lakini kwanini shirika lile halitowi huduma kama ilivyo. Leo unaweza ukapiga simu ukasikia kuna ngoma za Msewe, kesho ukasikia kuna mawimbi, keshokutwa ukasikia kuna jengine. Mheshimiwa kulikoni. Sisi tunakuomba wewe utupe jibu katika mwezi wa tisa, mwaka jana ulinambia kwamba wameamua watafunga mitambo mipya, lakini badala ya kufunga mitambo mipya ndio wameongeza kufunga mitambo mibovu. Mimi nasema hivyo hivyo kwa sababu hakuna yeyote atakayesimama hapa leo akaisifu *ZANTEL* kwa huduma. Kwa sababu huduma yetu siye ni kupata mawasiliano yalio bora na ndio ilikuwa tegemeo letu kwa Zanzibar Shirika la *ZANTEL*...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa malizia

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Leo limepoteza mwelekeo wake. Kwa hivyo baada ya haya Mheshimiwa sitaki kumega muda, naunga mkono hotuba hii ya kamati kwa asilimia mia na Inshaallah ni matumaini yangu kwamba mwezi wa tisa itakapofika, wizara itatupa majibu yenye mwelekeo ambao wenye mafanikio kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu tunao waongoza.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi.(Makofi).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa, anayefuata ni Mhe. Ali Khamis Bakar na akifuatiwa na Mhe. Said Omar Said na Mhe. Musa Ali Musa ajitayarishe.

**Mhe. Ali Khamis Bakar:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena kunipa nafasi kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati kaka yangu Mhe. Hamza, kwa kazi kubwa aliyoifanya na leo hii kukileta kitabu hichi kilicho mbele yetu na tukaweza kuchangia kwa yake ambayo alifanyia kazi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikiendelea nimpongeze Afisa Mdhamini Pemba (JB) kwa kazi kubwa anayoifanya na niseme tu kwamba Afisa Mdhamini Pemba ni hodari sana kwa kazi zake nzuri, anafanya kazi usiku na mchana. Lakini vile vile niwapongeza Mawaziri wangu wawili; Waziri wa Ardhi lakini vile vile na kaka yangu Komredi kwa kazi kubwa anazozifanya kuona kwamba wanasimamia vizuri wizara hizi ili kutatua matatizo ya wananchi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa Shirika la Nyumba ambalo wenzangu wengi wamegusia juu ya changamoto ambazo zipo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianza kwa nyumba za vijiji. Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashuhuda kwamba Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa awamu ya mwanzo alianzisha suala hili la nyumba za vijiji ili kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha, lakini vile vile kupata makaazi mazuri na bora kuweza kukaa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Micheweni nyumba hizi zipo kwa muda mrefu lakini sasa hivi zimechakaa mapaa yake yanavuja nyumba ni mbovu hazikaliki hata ile azma ya serikali kwamba kuna mapato yanapatikana pale lakini hayapatikani kutokana na nyumba hizi ni mbovu. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri kwamba angalie suala hili la nyumba zile kama kuna uwezekano awauzie yaani wananchi ambao wana uwezo wa kuzinunua nyumba hizi, ili kuweza kuzikarabati ukilinganisha nyumba hizi mfumo wake wa zamani wa ujenzi ni wa kizamani yaani hata nafasi hazina. Hivyo namuomba sana kama kuna uwezekano nyumba hizi wauziwe wananchi walio na uwezo kuweza kuziimarisha ili waweze kupata makaazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwa Mamlaka ya Maji (ZAWA), kwanza niwapongeze kwa kazi kubwa wanazozifanya lakini vile vile mimi kwa upande wangu wa jimbo langu la Tumbe nawashukuru sana asilimia iliopo mia moja, nimefikia asilimia themanini ya kuweza kupata maji. Kwa hivyo lazima niwapongeze kuona kwamba ni asilimia ishirini tu ya kadhia hii ya maji katika wananchi wangu wa Tumbe ndio iliyokuwa haipo nahisi kwamba kiupande wangu mimi wamenitendea haki. Hivyo nawaomba tu juu ya zile changamoto baadhi yake zilizopo katika jimbo langu waweze kuzitatua kuna baadhi ya vijiji vidogo tu ambavyo havijafikiwa na maji Insha'allah nina imani kwa mwaka huu 2018 na Afisa Mdhamini wangu mzuri JB, nina imani

kwamba katika jimbo langu la Tumbe kwa vile vijiji ambavyo havijafikiwa na maji vinaweza vikafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoa hapo niende kwa Shirika la Umeme wenzangu wengi wanechangia juu ya changamoto zilizotajwa katika kamati hii kwenye kitabu hichi, miongoni mwa changamoto hizo hapa wamesema ukosefu wa huduma ya umeme, katika baadhi ya vijiji katika Kisiwa cha Unguja na Pemba lakini mfano wametolea Shehia ya Sizini. Hili ni kweli lakini tu niseme si Shehia ya Sizini tu hata mimi katika jimbo langu la Tumbe kuna sehemu ya Uwaani baadhi ya nyengine Shumbaviamboni na kule Chimba baadhi ya sehemu nyengine umeme vile vile haujafika. Nimuombe tu Mhe. Waziri aangalie hali halisi ya mambo haya ili aweze kututalia na wananchi wetu waweze kupata mazingira mazuri.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hapa nimuuluize Mhe. Waziri kuna minong'ono isiyo ya uhakika ambayo nimeisikia kutoka juzi eti kuwa umeme umepandishwa bei. Kwa hivyo mimi nataka kujua atakapokuja anijibu kwamba kuna minong'ono hiyo imeelezwa kwamba kuna upandishaji wa umeme bei, hivyo atapokuja anijibu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwa Mamlaka ya Barabara, Shirika la Ujenzi wa Barabara. Mhe. Mwenyekiti hapa wenzangu wengi wamechangia juu ya hali halisi nzima ya maeneo yao lakini hata yale ya kawaida ambayo barabara zetu kubwa ambazo tunazitumia siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nimekuta baadhi ya changamoto ambazo zimetajwa lakini tu mimi nataka nikumbushie. Mhe. Waziri barabara inayotoka Fuoni kuelekea Tunguu sote ni mashuhuda humu katika kipindi cha mvua kuna sehemu inaitwa Kibondemzungu, pale sehemu ile ikifika kipindi cha mvua watu

wengi hutokezewa na maafa. Je, Mhe. Waziri, una mikakati gani ya eneo lile kwa kipindi hiki ambacho ni cha Kaskazi tunachoendelea nacho ukaweza ukajenga daraja ili kuwanusuru wananchi ambao wanapitia wananchi katika eneo lile na barabara uke wanaitumia ili kuweza kunusuru maafa haya yasiweze kutokea. Kwa hiyo ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana wizara waliangalie hilo pale katika eneo la Kibondemzungu kufanywe utaratibu wa kuweze kujengwa daraja.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze kwa kazi kubwa wanayoifanya lakini hapa nina maoni mawili. Kwanza nakumbuka kwamba kuna taarifa ya kuwa kuna wananchi ambao walishalipwa fidia katika sehemu ile ya uwanja wa ndege kama wahame, ili kuweza kupisha ujenzi wa uwanja wa eneo lake ambalo limekusudiwa katika masuala ya uwanja wa ndege liweze kubakia tupu. Lakini bado wananchi hawa siku hadi siku wanaendelea kujenga pale. Sasa nimuombe tu Mhe. Waziri hili kama halijui aliangalie kwa macho mawili kama kuna baadhi ya wananchi afanye ziara kila baada ya wiki kuangalia ni nani na nani ambaye alisogea na akigundua tu kama kuna wananchi labda wamesogea katika eneo basi achukuwe hatua za kisheria.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa nataka niengezee kitu ambacho nimekiona kwa uoni wangu. Mhe. Mwenyekiti, nimeshuhudi kwamba kuna daladala lakini vile vile na hata zile gari aambazo zinaenda pale kusubiri wageni zimewekewa *parking* kwa ajili ya usalama wao na wale watu wanaotaka kuchukua gari zile au kuingia wanapata hali nzuri. Lakini cha kusikitisha wale madereva wameshindwa kujengewa eneo maalum kwa ajili ya kukaa, kumejengwa vibaraza ambavyo hata kuezekwa havikuezekwa. Ina maana wale watu wanasimama tu pale hakuna hata labda sehemu ambayo imewezekwa kuweza

kuwanusuru ima kwa jua au kwa mvua. Kwa hivyo wanakaa tu, mimi namuomba Mhe. Waziri aliangalie na hili.

Lakini vile vile kuna wananchi ambao wanaenda pale kuwasubiri wageni wao nao hawana eneo zuri la kukaa. Kwa mfano uwanja wa ndege wa kule Chake Chake mimi nimeshuhudia kuna banda dogo ambalo limejengwa kando ya ule uwanja, wananchi wanapokuja pale kama kuna mtu anasubiri mgeni wake basi anaweza kukaa nje na akapata katika mazingira mazuri huku akimsubiri mgeni wake ateremke ndege, lakini baada ya kwisha teremka na yeye anapata kuungana naye. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri na kwa upande wa Unguja aliangalie hilo wananchi awajengee eneo rasmi la kukaa. Lakini vile vile kuna watu ambao ni wageni, lakini hata wale wanyeji ambao wanavuta sigara ovyo ovyo katika eneo lile jambo ambalo halipendezi na hawa angefanyia utaribu wa kuweze kujenga eneo maalum kwa wale wanaotaka kuvuta sigara wakaa kando, wakavuta sigara zao na baadaye mtu akaja zake katika mazingira ambayo wenzake wanakaa kuweza kuzungumza.

Lakini vile vile katika eneo hili hili la uwanja wa ndege kuna kile kituo cha daladala ambacho kipo pale. Mhe. Mwenyekiti, mimi vile vile na hapa naomba nichangie kwamba kuna ile barabara imewekwa maalum kwa kuweza kuingia gari pale kwenye uwanja wa ndege, lakini kuna wananchi ambao wanapita kwa miguu hususan walemavu hakuna eneo ambalo limetengwa la barabara kuweza kupita wao kama ni kipindi cha jua ama kuna mvua wakaweza kufika katika pale katika *airport* bila kurowa. Kwa hivyo hili namuomba Mhe. Waziri atakapokuja alione kuiona kamba ni jambo zuri, afanye maarifa mazuri ya kuweza kujenga ile barabara kwa ajili ya wanaokwenda kwa miguu, hususan walemavu wawe kipindi wanachopita wao sehemu yao lakini na vile vile zinazopita gari sehemu yake.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Shirika la Meli la Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hapa kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa inayoifanya lakini mimi michangio yangu itakwenda *against* kidogo na wenzangu. Mimi hapa kwanza nataka nizungumze kuhusiana na habari ya gati ya Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana serikali imefanya kazi kubwa sana kutujengea gati ile lakini nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba gati yetu inapofika kipindi cha mvua inakusanya maji utafikiria ni mtaro, panakaa maji mengi, wananchi wanaoteremka pale kwenye meli katika bandari ya Mkoani hata kama wana mizigo yako ambayo labda pengine mtu anasubiri gari yake au mtu wake aje ampokee au anasubiri lile toroli limchukulie mizigo. Mizigo inarowa hawana pa kuweka, mizigo ukiweka chini yote inarowa. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri na hili alichuwe alifanyie kazi kwenye gari ile pale ya bandari ya Pemba ya Mkoani.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi naomba nimwambie Mhe. Waziri wengi wamegusia suala la meli, mimi nataka kuligusia kwa upande mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kwamba kuna meli ya *SEALINK* kulikuwa na *SEALINK* mbili hiyo moja nasikia nayo vile vile imeharibika, lakini hata hii moja ambayo inafanya kazi, mimi nilikuwa naomba ifanye safari zake kwa mchana tu iondoke kila siku Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, Jumanne, wiki nzima lakini ifanye safari zake mchana, usiku kule kwetu tanasema hauna soko, likitokezea tatizo usiku ndio usiku na tayari huku nyuma limeshatokezea. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri wafanye wanavyofanya katika wizara yao wawapangie meli hii kwenda kule Pemba asubuhi ikifika Pemba kule kama imefika saa 8:00 iondoke siku ya pili, sio ifanye safari tena usiku. Hii kadhia

hii imekuwa kubwa na hata wananchi wanahangaika, wengine wanaondoka toka asubuhi makwao wanakwenda kukaa pale anasubiri mtu usiku anafika siku ya pili asubuhi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi mchangio wangu ulikuwa ni huo naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe kulingana na orodha bado ni kubwa, niwaomba sana tupunguze muda wetu dakika kumi na tano, tugawane kumi kumi ili tuweze kuchangia sote kulingana na muda uliopo na wengine hata kumi tunaweza tukavuta kulingana na kumi tunaweza tukavuta. Kwa hivyo sasa atakayechangia kuanzia dakika kumi na kushuka chini. Sasa namwita Mhe. Said Omar Said na akifuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

**Mhe. Said Omar Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Jaala Subuhana Wataala kwa kuniwezesha tena kuhudhuria tena katika kikao hiki jioni hii. Lakini pia nichukuwe nafasi hii ya kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano.

Nianze basi kwanza kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu wake, nimpongeze Mhe. Waziri wa Mawasiliano pamoja na Naibu wake. Niwapongeze kutokana na kazi ngumu na nzito wanayoifanya siku hadi siku lakini pia kwa uvumilivu wao wa muda mrefu humu katika Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano Mhe. Hamza Hassan Juma, jina linasibu. Hamza alikuwa ni mpiganaji mkuu katika vita vya Badri *(Makofi).*

Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma ni mpiganaji katika Baraza la Wawakilishi, nimpongeze sana kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kushirikiana na Wajumbe wake wa Kamati hiyo. Nimpongeze kwa kuwaridhia maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yake na hatimae mawazo yao ndio yote yaliyohudhurishwa hapa mbele yetu, nimpongeze sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 8 hapa nataka niungane na Mhe. Omar Seif Abeid katika changamoto za Kamisheni ya Ardhi. Hapa zimeorodheshwa changamoto nane lakini mimi nataka nigusie hii hii ya tano, inasema hivi nanukuu. Moja ya miongoni mwa changamoto ya Kamisheni ya Ardhi ni.

> "Kuwepo kwa mamlaka mbili tofauti katika usimamizi wa ardhi za eka tatu kwa Unguja na Pemba".

Maana yake hii ni kwamba mashamba ya serikali yaliyopo Pemba yako chini ya Wizara ya Kilimo, wakati mashamba kama hayo yaliyoko Unguja yapo chini ya Wizara ya Ardhi, hili ni tatizo. Mheshimiwa hili ni tatizo kama si tatizo leo hii kesho itakuwa mgogoro mkubwa huu. Nichukue mfano wangu mimi, mimi nina watoto wawili wanawake, mimi ninaishi huku Unguja lakini nina watoto wawili, mmoja Maryam na mmoja Asha, lakini Maryam naishi naye huku Unguja, Asha yuko Pemba. Maryam anaitwa Maryam Said watoto hao mama yao anaitwa Fatma. Maryam anayekaa na baba yake anaitwa Maryam Said, lakini Asha aliyeko Pemba anaitwa Asha Fatma. Huo si mgogoro nani walii hapo?

Mhe. Mwenyekiti, nadhani fikra hizi walizileta hao waliokuja na waliopita na kazi ya Baraza la Wawakilishi ni kurekebisha mawazo ya wale waliopita. Leo mawazo yetu yatakuja badilishwa kwa hao wanaokuja. Kwa hivyo mimi nashauri kwamba bado Wizara ya Ardhi ibebe mzigo wake kama ilivyo kisheria, Wizara ya Ardhi iwe ndio yenye mamlaka ya maeneo yote yaliyoko

Unguja na Pemba. Nashauri sana hilo kwamba hili halitoishia hapa keshokutwa tutakuja kuambiwa ile skuli ya Ng'ambwa kwa sababu iko karibu ya *studio* pale iko chini ya usimamizi wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, tutakuja kuambiwa hivyo hivyo keshokutwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa tulione hili na tulifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Ardhi ina jukumu zito na ina kazi muhimu mno tuliyowapa na ina watendaji mahiri na muhimu mno kwetu sisi, lakini mzigo tuliowapa hauna nyenzo. Mheshimiwa mimi kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi ni mtu makini sana. Lakini kwa mfano tuseme mimi nna mtoto hodari lakini nikasema hivi aah! mtoto wangu hodari huyo, anaweza akenda Nungwi kwa miguu akarudi hapa yuko makini. Sasa ikawa mimi namtuma kwenda Nungwi kwa miguu akanichukulie mizigo yangu akaja nayo hapa, siku mbili tatu vipi mtoto huyo si itakuwa nishamuangamiza. Kwa hivyo Mheshimiwa kwa umahiri walionao watendaji wa Kamisheni ya Ardhi, mimi nashauri wapewe *vote* yao hasa kutokana na kazi kubwa na majukumu makubwa yanayowalazimu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Mahakama ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, tunaposema hakimu huwa ni Hakimu wa Mkoa wa kawaida, huyu ni Hakimu wa Mkoa wa Mahakama ya Ardhi, Hakimu si Hakimu tu. Hakimu wa kawaida anahukumu yaani anachunga haki za watu, Hakimu wa Mahakama ya Ardhi anachunga haki za watu, Hakimu wa kawaida anaangalia haki za watu lakini bado yumo ndani ya ardhi. Kwa hivyo, naweza nikasema mwenye kazi ngumu ni huyu Hakimu wa Mahakama ya Ardhi. Kama hivyo ndivyo wanastahiki kupewa stahiki zote zinazowahusu Mahakimu wa kawaida, Hakimu wa kawaida anacholipwe, alipwe kama hicho Hakimu wa Mahakama ya

Ardhi. Wafanyakazi wa Mahakama ya kawaida pia stahiki zao ziende sambamba na wafanyakazi wa Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, nikotoka hapo niende kwenye Mrajis wa Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, nasema Kamisheni ya Ardhi ina jukumu kubwa, lakini Ofisi ya Mrajis wa Ardhi ina kazi kubwa zaidi, kwa sababu gani? Kamisheni ya Ardhi inatoa hatimiliki lakini Mrajis wa Ardhi yeye anasajili ardhi. Sasa ili aweze kusajili lazima kwanza aitambue na vipi kuitambua. Inawezekana sehemu moja wakapewa hatimiliki watu wawili, inawezekana eneo moja akapewa huyu hatimiliki, eneo hilo hilo nikapewa na mimi hatimiliki. Lakini je, tuiangalie ile Ofisi ya Usajili itatuandika sote.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa una dakika moja.

**Mhe. Said Omar Said:** Ahsante mheshimiwa. Haitotuandika sote. Sasa ili ipate uhakika lazima ifanye ufatiliaji nani anayehusu hapa na nani mwenyewe. Sasa kazi hiyo inataka ujasiri mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa Mhe. Waziri wa Ardhi namuomba sana Mhe. Waziri aniangalie kwa jicho la huruma katika eneo langu la kituo cha Elimu Mbadala. Kama jana nilivyoanza kusimulia hapa kidogo lilipowekwa jiwe la msingi kituo kile viongozi waliokuwepo hapo waliahidi kuchimba kisima hapo, lakini mpaka leo hakijachimbwa kisima. Kwa hivyo pale hapana umeme wala hapana maji. Mhe. Waziri nakuomba sana kwa bajeti hii utupe macho yako pale kwa masuala mawili, umeme na masuala ya maji.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na niseme tu nimekubali ripoti hii kwa asilimia mia. Nakushukuru sana.(*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sasa namwita Mhe. Hussein Ibrahim Makungu akifatiwa na Mhe. Mussa Ali Mussa na Mhe. Ame Haji Ali ajitayarishe.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi lakini awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kufika hapa salama katika Baraza letu tukufu, lakini niipongeze sana ripoti ya Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano kwa kazi yao nzuri na mambo mengi wametuandikia humu, nawapongeza sana mawaziri wote wawili wa ardhi na Waziri wa Mawasiliano. Pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kazi yake nzuri kutuletea ripoti hii ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie kwenye ukurasa wa 25 katika ripoti hii ya Mhe. Mwenyekiti wetu aliyotuletea Mamlaka ya Utafiti wa Mafuta, Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Zanzibar (*ZPRA*). Mheshimiwa mimi nisikitike sana hapa kwenye ripoti hii kidogo kwa sababu kunaonekana uchimbaji wa mafuta ni mambo muhimu sana katika nchi yetu na ukitizama tatizo kubwa katika ripoti hii tatizo ni kuchelewa kwa kuundwa Kampuni ya *Petrol Zanzibar* (*ZPBC*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba tatizo lake nini kampuni hii inachelewa kuundwa hata inakuwa hii sheria inashindwa kufanya kazi. Ukiangalia pia na Bodi ya Mamlaka ya Utafiti, Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar kama sheria inavyoelekeza. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba unielekeze tatizo ni nini kwa sababu hapa tukiangalia wananchi wengi wanavyoona kama Muungano wetu umetuzuia kutia mafuta wakati jambo haliko hivyo, huu Muungano wetu ni mzuri, Muungano wetu wa kidumu na hili suala la raslimali ya gesi na mafuta ni jambo wananchi wengi sana wanalisubiri kwa sababu ni ajira kubwa itasaidia nchi katika kusukuma ajira kwenye sekta hii ya mafuta.

Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri unambie tatizo ni nini tunashindwa kuendeleza sekta hii ya mafuta mpaka leo tunaambiwa hapa haijaundwa hii kampuni, Bodi haijakaa ikaundwa. Kwa hivyo naomba tatizo ni nini na kwa nini inachelewa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 56 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mheshimiwa kwanza mimi nipongeze sana sana Viwanja vya Mamlaka ya Ndege, nimpongeze Mkurugenzi kwa kazi yake nzuri sana anayofanya. Kama ninavyoona sasa hivi uwanja wetu unabadilika siku baada ya siku unabadilika lakini una changamoto nyingi sana mheshimiwa, ambapo ukiangalia *terminal* hii tunayotumia sasa hivi kwa *International Flight* kwa kweli changamoto ziko nyingi sana ndogo ndogo lakini zinaweza kutatuka. Tuangalie kwa sababu sasa hivi uwanja huo ndio tunautumia kwa wageni wetu wanaokuja Zanzibar kutoka nchi mbali mbali wa kitalii na wageni wengine wote wanaotumia. Kwa hivyo tuangalie lile jengo la abiria lilokuwepo sasa hivi la kuondokea haliridhishi ukiangalia kule juu hata *ceiling* halina lile jengo. Sasa namuomba Mhe. Mkurugenzi kwa kipindi hiki kama tunaendelea na ile *Airport* kuitumia basi hata ile *ceiling* iwekwe sawa kwa sababu mgeni akija akiangalia juu utaona yale mawaya yanaonekana ni aibu kwa wageni wanaotoka katika nchi iliyoendelea *Airport* kuiona vile. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia ukiangalia baadhi ya mashine hatuna hapa, kuwepo kwa X-*ray machine* hizi za mizigo mikubwa, kuna ndege nyengine zinashindwa kutua mheshimiwa kwa ajili ya mashine hizi. Ukiangalia kama kuna ndege nyengine *Emirates* haiwezi kutua kwa sababu ya viwango hatuna vya uwanja wetu haujakamilika. Mhe. Mwenyekiti, juzi juzi ilianguka ndege moja *charter*, mimi niko Dar es Salaam na bahati mbaya Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema kuna watu wawili alikuwa *engineer* na *pilot* wake wamefariki wote. Mimi najiuliza suala lile ile ndege

imeanguka jioni tumeshindwa kui-*save* iliwaka moto pale, lakini sijaona kwa nini tumeshindwa kui-*save* tusiwaokoe wale watu ili wasifariki, ndege imeungua na imewaka moto watu wamefariki. Sasa sisi tuna magari ya *fire* pale, sijui zile *fire* zimekaa ziko sawa au zinafanyiwa majaribio.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababau kuna ndege nyengine *international* haziwezi kutua kama ule uwanja haujakuwa wa kimataifa kweli kweli, kwa sababu hizi ndege zinazokuja hapa ukiangalia pale wakati wa kuruka mfano imewaka moto ile ndege pale, mna abiria karibu mia tatu mle ndani. Je, tunaweza kui-*save* ile ndege sisi. Kwa hivyo nawaomba sana mamlaka iangalie sana kwa sababu mashirika yanataka kuja kutua hapa kwetu lakini wanaangalia vigezo, hata haya mambo ya *handling* iangaliwe vigezo vipo vya kutosha, tukikaa inakwenda siku baada ya siku nchi zinaendelea sisi tuko hapa hapa bado hatujaendelea. Kwa hiyo, naomba sana Mkurugenzi wa Mamlaka uangalie vile vitu muhimu sana tuweke ili tuweze kuongeza hizi idadi ya ndege.

Mhe. Mwenyekiti, pia niishukuru sana serikali huu ujenzi wa *Terminal II* na sasa hivi unaendelea na ile *Airport* sio muda mrefu tutaitumia. Mimi nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi yake kubwa sana aliyoifanya kwa kuhakikisha uwanja ule unamalizika na fedha zilizotumika hazijapotea, kwa sababu kuna Baraza lilokwisha mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati. Katika kamati hiyo kulikuwa kuna Wajumbe walikuwa wanataka *Airport* ivunje ile, lakini kwa umakini wake Mhe. Makamu wa Pili nampongeza alisema *Airport* hiyo itajengwa na itakuwa na wamekuja wakandarasi wameibadilisha sasa hivi ujenzi karibu unakamilika. Kwa hivyo mimi nimpongeze sana kwa juhudi zake na serikali kwa ujumla kwa kazi zake nzuri alizozifanya. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Mheshimiwa Uwanja wa Ndege unakua siku baada ya siku kwa vile tunauongeza, na pia ulivyofika pale na baadae tukaongeza tena zaidi. Mimi nikiangalia tukitoka Dar es Salaam kwa ndege ukitizama chini unakuta uwanja umekaa ramani yake kama kashata mheshimiwa. Ukitizama hapa kuna nyumba wanaishi wananchi, hapa uwanja umeingia ndani, ukitoka mbele umekwenda tena sawa, umekwenda hapa kuna nyumba. Sasa hii *reserve* Wajumbe wamesema hapa, inatakiwa mita 60 *reserve* mtu yeyote asiwe kwenye uwanja ili ndege ikitokea bahati mbaya imeshindwa kutua au imeshindwa kuruka itakwenda kuvamia nyumba za watu. Kwa hivyo, wale jirani wanaokaa pembeni ya uwanja wale wahame, kama fidia walipwe na kama itakavyokuwa ule uwanja ukae sawa usikae kama kashata ramani yake mheshimiwa hauridhishi na unaibisha kwa wageni wanaokuja katika visiwa vyetu hivi.

Mhe. Mwenyekiti, niende haraka haraka kwenye ukurasa wa 48 kwenye Shirika la Bandari. Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana bandari yetu wanafanya kazi vizuri, wanajitahidi sana, meli zinakuja zinafunga mizigo pale usiku na mchana wanafanya kazi. Mimi nimpongeze Mkurugenzi wa Bandari kwa kazi yake nzuri sana. Kwa sababu ukiangalia pato letu la taifa sisi tunapata karibu asilimia 30 kwenye mizigo au mpaka 40 kwa wafanyabiashara walipa kodi pale. Kwa hiyo mimi niwapongeze na wafanyabiashara tukiwasilikiliza kwa kweli kiundani wanaridhika kwa huduma ya bandari kwa sasa hivi, mpaka usiku wanafanya kazi hawa ndugu zetu, niwape pongezi kwa kazi yao nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme hawa wenye makampuni makubwa, ukiangalia sasa hivi meli yetu imeharibika lakini kuna meli za *Azam Marine* zinafanya kazi masaa 24 zinakwenda Bara mpaka tiketi hupati. Inafika wakati tiketi pia hupati unanunua ulanguzi, tiketi elfu 60,000 watu wanataka kusafiri boti hamna. Lakini

ukiangalia changamoto kubwa Mheshimiwa mwenyekiti wetu ameandika hapa kuchelewa kwa malipo ya huduma zinazotolewa na baadhi ya makampuni na mashirika yakiwemo *Azam Marine*. Mheshimiwa hili ni jambo la kusikitisha sana, hii bandari inataka fedha ya kujiendeleza. Sasa bila ya fedha hawa ndugu zetu watafanya kazi zao vipi. Kwa hivyo, naomba sana hii kampuni iandikiwe barua ilipe kwa sababu wao wanafanya biashara nzuri, wananchi wanatumia meli zao sana. Sasa hivi meli yetu wenyewe sasa hivi inasikitisha imelala nangani pale. Lakini meli inayotumiwa ni *Azam Marine* peke yake ikienda Pemba imejaa, ikienda Dar es Salaam imejaa, magari yamejaa kwenye meli. Kwa hivyo, *alhamdulillah* biashara inafanyika kwa nini kodi hii isilipwe kupitia bandari wakapata kujiendeleza.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende haraka haraka kidogo kwenye Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, nimuombe sana Mhe. Balozi kule jimboni kwangu kuna njia moja ile ya Mwanyanya ndani, tangu mimi naingia kwenye Baraza hili njia ile inatiwa kifusi hivi sasa imekufa yote ile njia haifai. Kwa hivyo naomba sana miaka minne mpaka mitano sasa hivi ile njia haijatiwa lami. Sasa naomba kama kupitia halmashauri, kupitia wizara nisaidiwe mheshimiwa naomba kilio hiki, kwa sababu wananchi wangu wanasikitika sana njia ile haipitiki jeshini sasa hivi, kukiwa na maziko, ukiwa na mgonjwa inakuwa ni shida imetiwa kifusi mara ya tatu, naishukuru serikali lakini kifusi kinaharibika. Kwa hivyo naomba sana hata kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi njia ile ilikuwa itiwe lami mwaka jana. Kwa hiyo nakuomba Mhe. Waziri nisaidie sana ile njia ya Mwanyanya inayoanzia kwa Kisasi inatokea mpaka kwa Handhari huku.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye huu ukurasa wa 55 katika meli yetu ya Mapinduzi II. Mimi nisikitike sana meli ile, kwa sababu iliponunuliwa meli ile Mheshimiwa mimi nilikuwa Mjumbe wa

kamati na ilikuwa mimi niende Korea kwa bahati mbaya mimi sikwenda Korea, lakini ilikuwa nichukuliwe kwenda Korea kuangalia ule mkuku unavyowekwa. Leo ukitizama hii meli kila sifa, unaambiwa hii meli siyo, meli mlango hamna, meli mbovu. Sasa hatujui kilichofanyika nini. Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye Baraza hili watu wote walikatwa pesa maskini ya Mungu wakawa watu mishahara wengine hawapati, sisi wenyewe Baraza tulikatwa pesa humu. Sasa nashangaa meli hii imekufa kwa muda mchache imechukua abiria karibu 49,000 tu meli imekufa. Sasa kwa nini ife meli hii na meli nzuri. Lakini hapa kwenye changamoto tumeambiwa kukosekana kwa wataalamu wazalendo wa kudumu wa kushughulikia meli hiyo. Sasa wazalendo hamna kwenye hii Mheshimiwa tumeshaambiwa, kwa sababu hapa kuna wananchi wameshafanya kazi hawana nia njema na nchi hii ndio wanaoishughulikia meli hii. Mimi nimeuliza kwa nini hii meli imeharibika. Nimeambiwa imetiwa mafuta machafu. Mafuta hayo kwani hayapimwi, kwa nini imetokezea hivyo.

Mhe. Mwenyekikti, mimi gari yangu natia mafuta siku zote yanakuwa masafi, kwa nini meli hii itiwe mafuta machafu, itakuwa imefanyiwa *sabotage* makusudi meli kuharibika. Sasa hili suala kamati yetu imeleta ripoti kabisa katuandikia kwenye kifungu nambari 2 ukurasa wa 55, kukosa kwa wataalamu wazalendo. Sasa hili tuangalie sasa hivi tutizameni waletwe wale wazalendo wanaoipenda nchi hii na hasa tuwapeleke wananchi wetu wa Chama cha Mapinduzi waendeshe meli ile. Sasa leo wanakuwa wanakwenda watu hawana imani wanaiharibu meli mabilioni ya pesa yamepotea kwenye meli ile na wananchi wa Pemba inawasaidia na wanaokwenda Bara, leo hatuna usafiri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisikitike sana meli hii kukaa pale nangani inaharibika. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hebu atwambie tatizo lake nini meli hii, kama inatengenezeka...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa una dakika moja malizia.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Ahsante Mheshimiwa namalizia dakika tatu naomba. Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Sekta ya Nishati katika ukurasa wa 22.

Kwanza niwapongeze sana hawa Shirika la Umeme ndugu zetu, kuanzia meneja na mtandao wake wote. Niwapongeze kwa sababu hawa wafanyakazi nasema hapa ni wazalendo, kwa sababu kama hawa wanataka kufanya *sabotage* kama hii meli basi hawa ndio walikuwa wafanye *sabotage,* kwa sababu umeme hauchezewi na mtu asiyeujua, lakini ndugu zetu hawa wa Shirika la Umeme muda wote wanafanya kazi vizuri na umeme unawaka na sasa hivi umeme nasema asilimia karibu 80 hauzimiki ovyo ovyo. Mimi nawapongeza sana Shirika la Umeme kwa kazi yao nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakin niseme hawa Shirika la Umeme wenzetu wana madeni, ukiangalia kwenye ukurasa huu wa 22 haya madeni yao yalipwe, kwa sababu hawa watashindwa kuendesha hili shirika mwisho watakuwa wanakwama.

Mheshimiwa nimalizie kwenye Mamlaka ya Maji (*ZAWA*). Mimi nilikuwa mjumbe wa kamati miaka mitatu iliyopita kwenye masuala haya ya maji, Ras al-Khaimah walichimba visimba 150 na wametimiza visima 49 ambavyo katika Mkoa wa Mjini/Magharibi tu. Mimi shahidi nilikuwepo, lakini mpaka leo la kusikitisha visima hivyo katika Mkoa wa Mjini/Magharibi vinafanya kazi visima vinne tu, mimi mwenyewe kwenye jimbo langu maji sipati.

Mwisho nasikitika, natoa salamu zangu hizi ile *ambulance* ya kupakia wagonjwa leo inapakiwa maji kwenye jimbo langu. Wananchi hawana maji wanakwenda kuchukua *ambulance*

wanapakilia maji. Juzi mgonjwa anataka kupakiwa nikapigiwa simu mimi, nauliza *ambulance,* naambiwa inapakiliwa maji. Sasa naomba tuangalie hasa suala la maji tunafanya nini. Ndio hapa kuna watu wengine si wazalendo na hawana imani na nchi hii, wako hapa *ZAWA*. Haiwezekani Ras El-Khaimah watusaidie visima 150 visima vinne tu ndio vinafanya kazi mpaka leo, haiwezekani Mheshimiwa Zanzibar maji yapo mengi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nishukuru sana na niipongeze ripoti ya kamati, nimpongeze mwenyekiti kwa kazi yao na wajumbe wa kamati wote akiwemo na Mhe. Nassor Salim Ali akisaidiwa na Mhe. Mwenyekiti. Niwapongeze kwa kazi yao nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante kwa mchango wako Mheshimiwa. Sasa anafuata Mhe. Mussa Ali Mussa ametoka. Kwa hivyo anayefuata ni Mhe. Ame Haji Ali.

**Mhe. Mussa Ali Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ndogo ili nichangie Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano inayoongozwa na mwenyekiti kipenzi cha wawakilishi Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na wajumbe wake, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niende kwenye ukurasa wa 7, Kamisheni ya Ardhi. Nasema Kamisheni hii tuliitegemea kuwa itakuwa na mambo matatu, manne, mpaka matano. Kwanza kutambua ekari tatu, pili kutambua ujenzi wa miji pamoja na vijiji. Hii yote ilikuwa ni kazi yake Kamisheni ya Ardhi, kutambua ekari tatu zile alizoziweka Mheshimiwa kipenzi chetu cha mwanzo Mzee Abeid Amani Karume. Pili kupanga mji, vijiji na mambo mengine pamoja na kupima viwanja vya miji. Lakini mpaka leo hakuna kinachofanyika ni ubabaishaji tu. Kwa hivyo, nashauri kwamba Kamisheni hii ivunjwe kabisa haifai badala

yake iundwe Bodi ya mpito kushughulikia jambo hili. Hili jambo hii Kamisheni kwetu haikuleta maslahi yoyote, sioni kama ina maslahi na kama kuna mwenzangu anaona ina maslahi asimame aijengee hoja maslahi yaliopo.

Hili nilisema hapa Baraza lililopita kwamba ukienda kuhamia katika mji, kama ukihama hapa kwenda kutafuta mji wa kuhamia, ukikuta hakuna mtu mzima wala hakuna tajiri katika mji huo usihamie huo mji haufai. Kabla sijalichambua neno lile nikapata kibonge cha Kanuni nikakaa kitako. Sasa leo je, Wawakilishi wenzangu, wapiganiaji haki za wananchi wa Pemba na Unguja au wa Zanzibar wameyaona? Yale waliyonipigia Kanuni nataka kuyaeleza wameyaona leo? Kila Mwakilishi anayesimama anataka maelezo kuhusu meli ya M.V. Mapinduzi II, maelezo hayapo ni kiunga uzi tu, jamati limeingia golo, meli leo iko Bububu, Bububu ndio Pemba? *(Makofi)*

Jana nimesimama pale kuiangalia meli hiyo machozi yamenitoka, nilikuwa nimepakiwa na mheshimiwa mwenzangu nikamwambia simama meli yetu ile pale. Jamani tunakwenda wapi, kwa nini hatutumbuani, tutafika wapi kwa mpango huu. Mwaka 2020 ni keshokutwa leo unanunua pasi kwa shilingi 150,000 mwenye duka anakupa siku 30 kama pasi haifanyi kazi irejeshe uchukue pesa zako, leo meli ya shilingi bilioni mia tatu tumeshindwa kupewa *warrant* wa miaka miwili kama meli ikiharibika turejeshe au tuje tutengezewe. Tunaharibu pesa za serikali kutengeneza jambo ambalo halitengezeki. Kwa nini Waheshimiwa wenzangu hatukai pamoja tukamuomba mwenyekiti akatupa nafasi tukaunda Tume na mimi mwenyewe nikiwemo, tukachunguza wenzetu waliokwenda kutununulia meli ile. Haidhuru iwe ni mpya, sasa upya niliouzungumzia mimi ni upya wa meli, kamba, nanga, viti. Ule ndio upya wa meli? ile ndio meli ya kisasa? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema kwamba, "*Allah, Allah,* ujiti na macho na ncha ina hoho". Sasa hivi tunataka kujitia hoho kama hatukulishughulikia jambo hili. Hili ni jambo zito, kubwa na lenye dhara sana, pesa nyingi za wananchi tumezitumia kwenye meli hii. Leo tunataka na nimeona mapendekezo ya kamati hapa kwamba meli inaendeshwa kwa hasara iuzwe. Jamani meli mpya inaendeshwa kwa hasara. Kuna meli la Said Salum Bakhresa limekuja lile *Sealink* mwaka 1959 mwaka niliozaliwa miaka 62 ipo pale inafanya kazi, inakwenda Unguja na Pemba ikirudi, inakwenda kila siku usiku na mchana. Mhe. Mwenyekiti, imeundwa mwaka 1959 mwaka niliozaliwa ina miaka 62 meli ile ipo. Leo Meli ya M. V. Mapinduzi II imekuja miaka mitatu jamani inakwenda kuwekwa uchochoroni Bububu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena nakuomba kwa heshima yako na mapenzi yako Baraza mara moja liunde tume kuchunguza wenzetu waliokwenda kununua meli ile na tukigundua kuna mmoja kafanya uhiana, basi huyo tumtumbue tenzi hana jipu ana tenzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tumalizie hapo niende kwenye barabara. Nashukuru sihaba natakiwa kama binadamu ukipata ushukuru hata kama ni kidogo. Barabara ya Ole-Kengeja nimepata sihaba, nimepata kilomita tatu zile kutoka Ole mpaka Vitongoji panapitika na bahati nzuri ndio jimbo langu na wananchi wanajua kwamba hii ni juhudi ya Mwakilisha. Kwa sababu wananisikia nikipiga kelele, nikienda kule wananambia tumekusikia bwana, sasa nimepata. Lakini nasema tena kwamba pale tulipopata tupahifadhini vizuri. Hili namuomba Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, ile barabara pale palipopatikana akaipigie misingi, mvua za masika zinakuja itakuja kukatika barabara ile, itakuwa kazi na pesa za serikali bure. Sasa ingekuwa ni bora sana hivi sasa angewatuma wafanyakazi wake ile barabara

wakaipigia misingi ili isikae maji, pale tulipopata iwe tumeshapadhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niiombe serikali bajeti inayokuja tuisaidie Wizara hii ya Mawasiliano ipate vyombo vya kisasa, ma-*bulldozers* yenye nguvu ya uhakika ili waimalizie barabara ile kutoka Vitongoji kwenda Kengeja. Kwa vyombo vile ambavyo wanavyo kwa sasa tutawalaumu bure haviwezi, havipandi vilima vya Pujini na Chambani, nimekwisha kuangalia nawafuatilia vizuri, ingawa kuna maagizo wamepewa. Baadhi ya watendaji wake Mhe. Waziri wana maagizo wamepewa na nimesikia wakiyazungumza maagizo hayo, lakini nawaambia tena maagizo hayo yatawaletea madhara maana Baraza la Wawakilishi halitakubali. Mhe. Mwenyekiti, waliambiwa kwamba kuidhoofisha serikali ni kuharibu vyombo, wasikae makazini, wapoteze muda tu ili Serikali ya Mapinduzi iingie dosari. Mapinduzi hayaingii dosari bwana, Mapinduzi Daima, wakorofi waliotumwa kudhoofisha wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tutapambana nao na vijana wanaotaka kazi tunao, kwa nini tuwapembejee watu, wakati vijana wa Mapinduzi tunao wanataka kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo tusimpembejee mtu, kama mtu ana maagizo aliyopewa basi mtu huyu tumuweke upande ili tuwaweke vijana wakafanye kazi pale. Kiongozi wetu mkuu amesema sasa kazi, kwa hivyo tufanyeni kazi. Wawakilishi wote tushirikianeni pamoja kwa nguvu zote wakorofi tuwatoe na mule ndani ya meli ya Mapinduzi kama *Allah* ataijaalia ifanikiwe, sasa tunataka mchujo, tunakujua mwana Mapinduzi nenda kafanye kazi, kwani kuna kazi gani mule, kazi mule ina *captain,* waliobakia ni kurusha kamba, kufyagia, kuokota *pampas*, ndio wana Mapinduzi hawawezi, mbona wamekwenda kupiga kura, washindwe kwenda kuokota *pampas* mule na kuzitupa nje.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, leo nimeingia kwa mara ya mwisho juzi natoka kwenye Sherehe za Mapinduzi nakwenda Pemba, eti vyoo vyote vimejaa, tena kule *VIP* wanakokaa Waheshimiwa ndiko vyoo vilikoziba, kinyesi kiko juu. Huku kwa mama ntilie kupo safi kabisa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa una dakika moja malizia.

**Mhe. Mussa Ali Mussa:** Hata nusu dakika. Mhe. Mwenyekiti, hiyo dakika moja uliyonipa nataka kidogo nizielezee barabara za *airport.*

Barabara ya *airport* kutoka *Abeid Amani Karume Airport* kwenda Darajani na kutoka *Karume Airport* kwenda Chake Chake. Jamani mgeni yoyote anayekuja kutoka Ulaya, Oman, Marekani na kwengineko anafikia *airport,* keshokutwa mvua zinakuja paangaliwe pale panapoitwa Mkunazi wa Pili kwenye Msikiti. Wizara ya Mawasiliano haraka ichukue hatua kabla mvua hazijanyesha. Mhe. Waziri namuomba sana tena sana kabla mvua hazijanyesha barabara kutoka *airport* mpaka mjini Darajani itengenezwe, itanuliwe, itiwe mitaro tusije tukapata aibu mvua kubwa zinakuja. Kioo cha nchi yetu ni kutoka *airport* kuja mjini, namuomba sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ulinitaka nitume dakika moja na mimi nimetumia hiyo dakika moja, lakini nataka niunge mkono kamati hii inayoongozwa na mtaalamu Mhe. Hamza Hassan Juma na namwambia ahsante sana pamoja na kamati yake nawapongeza sana.

Ahsante naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, Mheshimiwa anayefuata ni Mhe. Ame Haji Ali akifuatiwa na Mhe. Yussuf Hassan Iddi ajitayarishe.

**Mhe. Ame Haji Ali:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nami nianze kwa kumshukuru Muumba wetu kutuwezesha jioni hii kuwepo hapa kufanya kazi tuliyotumwa na wananchi wetu huko majimboni.

Mheshimiwa mimi sina mchango mkubwa sana lakini ni wajibu kwa sababu wananchi wa Jimbo la Nungwi wamenituma nije hapa, kuna baadhi ya mambo tu kidogo naomba niwasemee.

La kwanza, niende katika ukurasa wa 13 wa kitabu hiki. Wenzetu wana kamati wameitaka Mahakama ya Ardhi kujitahidi katika utatuzi wa migogoro. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo ambalo limechukua sura kubwa sasa hivi katika nchi yetu ni eneo la ardhi hasa kwenye migogoro. Kule kwetu Kaskazini sasa hivi huna mahali utakapopita, huna sehemu utakayokaa usikutane na migogoro ya ardhi. Mimi ninaiomba sana wizara, naiomba sana serikali katika eneo hili tujitahidini kadri tuwezavyo tupunguze migogoro katika ardhi zetu, ardhi ndio raslimali kila kitu na wananchi wetu wanaitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, hata pale serikali inapofanya maamuzi ya kutumia ardhi kwa maendeleo ya wananchi hawa basi wananchi hawa wapewe maelekezo yanayofaa. Ardhi tunakubali ni mali ya serikali ndio utaratibu, lakini kuna wananchi wetu wanatumia toka asili na wazazi wao wamewakuta wanatumia, pale serikali inapopata jambo sasa la kwenda kutumia ardhi ile wananchi wetu hawa tuwaelekeze vizuri, ili sasa tusiingizwe mahali sisi viongozi wa chini tukapata masuala ambayo hatuna majibu nayo. Ninaiomba sana serikali katika eneo hili tulichukulie kwa nafasi hiyo tujaribu kadri iwezekanavyo tunapotaka kwenda kutumia ardhi zilizopo katika maeneo tuwaelekeze wananchi ili tusiingie katika mgogoro. Sasa jambo langu la kwanza nilitaka niliseme hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo langu la pili nataka nizungumze hii kadhia iliyopo katika nchi yetu ya uhaba wa maji safi na salama. Mimi naamini katika Zanzibar nzima jimbo linaloongoza kwa uhaba wa maji ni jimbo langu, naamini hivi.

Kwanza niishukuru serikali jitihada kubwa zimefanyika katika kutatua tatizo hili. Lakini nataka niiambie kwamba bado Jimbo la Nungwi linakabiliwa na uhaba wa maji uliokithiri. Licha ya jitihada zote hizi zilizofanyika lakini bado kuna uhaba wa maji uliokithiri. Leo mwananchi wa Jimbo la Nungwi analazimika akiamka kwanza aamke na shilingi elfu tatu za kuweka ndoa sita za maji kwa ajili ya matumizi nyumbani kwake. Na mwananchi huyu huyu analazimika aamke na elfu mbili za kuweka ukuni wa kupikia mapembe akiyapata, hajapata hayo mapembe, tufikirie mwananchi huyu wa kawaida ana gharama hizi za lazima za zaidi ya shilingi elfu tisa kabla ya kupata chakula hazimudu.

Kwa hivyo naiomba sana serikali katika eneo hili licha ya jitihada ambazo tumejitahidi, bado katika Jimbo la Nungwi kuna tatizo kubwa la maji. Vyanzo tunavyovitumia vya maji ni kupitia chemuchemu zetu za Kiashangwe. Mhe. Waziri zile chemuchemu zina maji ya kutosha, bado tukubaliane kwamba chemuchemu za Kiashangwe zima mati ya kutosha. Tatizo utendaji mbaya, nitoe mfano ulio hai. Tangi letu la Mwanguo, vikitumika visima viwili lina uwezo wa kujazwa maji kwa masaa ishirini na nne, lile tangi likijazwa kwa masaa ishirini na nne uwezekano wa kutumia maji Jimbo la Nungwi ni asilimia thamanini na watu wote watapata maji.

Kuna kisima mwaka kasoro siku moja umekatika waya wa mita moja kinashindwa hadi leo kushughulikia kisima kile. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanaendelea kudhalilika, wananchi wanaendelea kukosa maji, serikali tupo, viongozi sote kwa

pamoja tushakwenda kwenye pale kwenye eneo tushaliona jambo lile tumeliripoti si mara moja, nadhani Wawakilishi sote wa Kaskazini tumeenda eneo lile. Sote kwa pamoja tumeliona eneo lile. Lakini hadi leo kadhia ile ipo kipande kile cha waya hakizidi mita mbili na kama mita niliyokuwa pale haipo haya mita inapatikana Shirika la Umeme ndio ya serikali hii hii. Lakini hadi leo kisima kinashindwa kwenda kuweka huduma ile wananchi wakaendelea kupata maji. Jamani lazima tufike mahala tuwaonee huruma wananchi hawa ambao sisi ndio wametuleta hapa kwa ajili ya kuwatumikia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili zipo njia mbadala, maana mimi nimesema mwanzo kwamba jimbo hili linaongoza kwa uhaba wa maji kwa sababu hata ukichimba kisima cha kawaida upata chumvi, huwezi kupata maji mazuri. Kwa hivyo lazima utafute vyanzo viliiopo vyengine ili usaidie jambo hili, vyanzo pekee ni kwamba vipo visima ambavyo tushachimba kwa nguvu za wananchi. Tushakwenda mamlaka inayohusika si mara moja si mara mbili si mara tatu, lakini tunashindwa kupata majibu kwa nini visima vile vinashindwa kushughulikiwa vikafanyakazi. Tunacho kisima pale Mvuleni Mhe. Waziri kama hujafika, kile kisima kina maji ya kutosha ambayo mimi naamini kama tutaweza kukishughukilia kisima kile, wananchi wote wa eneo la Fukuchani na eneo jirani wako salama. Kisima kimeshindwa kupata umeme kimetiwa *pump* tumejaribu angalau tutie *solar* pale maji yapo pale yanashindwa kufikishwa sehemu huzika.

Lakini kisima cha pili kipo Kidoti kwa Marehemu Mzee Mcha kipo kisima Mhe. Naibu Waziri nimekwenda na wewe na Kurugenzi zako zote nimekupelekeni. Kile kisima Kurugenzi zilituhakikishia kina maji ya kutosha. Sasa kama kisima kile tungekuwa tumekimaliza tutakiunganisha kisima kile maana yake ni kwamba wananchi wa Kidoti wangekuwa salama, wananchi wa Bwereo wangekuwa salama, wananchi wa Kilimani wangekuwa

salama, maana yake sasa tumepunguza Shehia nne, zimebakia Shehia tano. Tangi linalotoa maji Mwanguo likapeleka Kaskazini hawa wangekuwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, sijui kilichoshinda kitu gani hadi leo ukenda huku unarejeshwa, ukenda kule hupati jibu. Tena kisima kile Mhe. Waziri kwa taaarifa yako wananchi wale wa eneo lile pale la Kidoti walitumia nguvu zao na Mhe. Ayoub Mahamoud Mkuu wa Mkoa wa sasa akawasaidia na Mhe. Ayoub Mahmoud mbele ya kikao akawaambia jamani nawachieni kisima hichi sasa *ZAWA* kilimalizeni, hakuna majibu. Kibaya zaidi kilicho hicho ni kwamba wananchi wale na kwa bahati wengine sasa wameshakuwa marehemu walitoa pesa zao kupitia Afisa wa Maji wa Wilaya hadi leo hawajalipwa. Mimi ni shahidi nimeshakwenda nao si mara moja si mara mbili kwenda kutoa maelezo hayo na kwa taarifa yako Mhe. Waziri watu wale wanadai shilingi milioni moja, laki moja na elfu kumi, zimekwama wapi sijui. Sasa mambo haya wakati mwengine tunawafanya wananchi wetu tuwavunje moyo na hakika serikali inao uwezo wa kupata mashine ya kisimani kile, nina hakika serikali inao uwezo wa kupata mabomba ya kusambaza kutoka pale ikawa salama.

Leo hii mimi nataka mtu yoyote atoke hapa kesho asubuhi aanze Fukuchani aangalie msururu wa mapira yaliko barabarani yanasubiri magari yatoke Chaani wauziwe maji. Jamani mpaka lini, hebu tuwaonee huruma watu mambo mengine haya yanawezekana. Sisi tumefanya jitihada kama viongozi. Mimi nilipokuja katika jimbo hili nilikuta hali hii mbaya zaidi kuliko hivi ilivyo sasa, nimefanya jitihada kupitia mfuko ule tulioipata sisi tumetoa *line* la maji kutoka Mwanguo mpaka Fukuchani wananchi wale wamepata afueni kidogo. Tumetoa line kutoka Bwereo mpaka Mwanguo wananchi wale wamepeta kidogo, lakini maji bado hayatoshi kwa sababu chanzo tunachotumia ni kimoja. Tunahitaji sasa *line* hizi tuzitoe katika chanzo kile tukielekeze

katika vyanzo vyengine ili hichi chanzo kimoja kilichobaki, hawa walioko huku Kaskazini wangepata maji. Maana hatuwezi kwenda kuchimba kisima Nungwi hata tukichimba kisima watapata chumvi. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa malizia muda wako.

**Mhe. Ame Haji Ali:** Heee! Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina mambo mengi ya kusema lakini naheshimu sana kiti chako. Baada ya kusema hayo naomba sana niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyowaambia wachangiaji ni wengi niwaombe tena sasa dakika tuzipunguze dakika kumi. Tutafanya dakika tano kwa wachangiaji waliobaki. Muda wetu uliobakia na hoja iliyoko inatakiwa imalize tuangalie na muda wetu. Kwa hivyo, kila mchangiaji atachangia kwa dakika tano.

Sasa anayefuatia ni Mhe. Yussuf Hassan Idd na akifuatiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla.

**Mhe. Yussuf Hassan Idd:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, japo naona dakika zimekuwa chache lakini nitakwenda maneno ya vijana *faster*, *faster*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa wote mawaziri Mhe. Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Balozi Karume na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Mhe. Salama Aboud Talib. Pia nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano kwa kuwasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum Mhe. Haji Omar Kheir kwa juhudi zake ambazo amezifanya kuhakikisha kwamba barabara ya Kijitoupele hadi Fuoni Mambo Sasa basi inapatiwa fedha na ikajengwa na hii ni ahadi imo katika Ilani yetu ya Chama Chama Mapinduzi. Kwa hivyo tunakupongeza Mhe. Waziri ukiangalia Ilani yetu ukurasa wa 150 hiyo barabara ya Kijitoupele hadi Fuoni Mambo Sasa utaiona.

Lakini kuna wananchi wa Fuoni bado wanaomba kwa sababu kuna mradi mkubwa tu kule wa Skuli ya Ghorofa Mambo Sasa, lakini njia yake kutoka Maharibiko hadi katika skuli ile si nzuri. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum Mhe. Haji Omar Kheir katika bajeti inayokuja ya 2018-2019 basi barabara hii ingizwe katika mpango wa lami ili iwe rahisi kutoka barabara kuu hadi kuweza kufikia eneo la mradi wa skuli hiyo.

Vile vile tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga barabara ya Mwanakwerekwe, Fuoni hadi Tunguu. Lakini barabara ile imekwama tunaomba tuiulize serikali je, tatizo gani limetokezea mpaka ile barabara imeishia Fuoni Polisi, lakini haijamaliza eneo la Tunguu na lini barabara hiyo itakamilika ili wananchi wapate kuitumia kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikumbushie ahadi mbili za viongozi wetu wakuu ya kwanza kabisa ni ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kujenga barabara kutoka Fuoni Mtundani hadi katika Skuli ya Kitongani. Juhudi za awali zimeshaanza lakini bado ahadi hii haijatekelezwa ipasavyo. Kuna wananchi wa Fuoni Kitongani, Fuoni Kipungani, Fuoni Mikarafuuni, Fuoni Migombani wana hamu kubwa ya kutumia barabara hii. Kwa

hivyo, tuombe Wizara ya Mawasiliano washirikiane na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kwamba ahadi hii ya Mhe. Rais Mstafu Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete inatekelezwa na wananchi wanapata kuitumia barabara ile.

Lakini vile vile katika barabara ya meli saba Birikani kweda Mwera Polisi. Barabara ile imejengwa kwa mradi wa *MIVAP* lakini barabara zile nilikuwa naona hazina viwango, barabara ile haipitiki lakini Mhe. Rais wa Zanzibar ameiona barabara ile na amehadi sasa tunakumbushia tu kwamba kabla 2020 basi basi barabara ile iwe katika kiwango cha lami, ili wananchi waweze kuitimua. Barabara ile ilikuwa kiungo kikubwa sana ilipotokea mafuriko kipindi kile cha mvua watu wa Kusini walikuwa wanaitumia barabara ile kwa ajili ya kuingia Mwera kuja zake Mjini. Kwa hivyo barabara hii ina umuhimu wake ipo haja ya kuifanyia ukarabati. Mhe. Mwenyekiti, kwa vile muda hauko nasi nitakwenda mbio mbio.

Lakini la pili kwenye ukurasa wa 19 nije kwenye *ZAWA*. Tuwapongeze wenzetu hawa wa *ZAWA* kwa juhudi ambazo wanazozichukuwa za kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma ya maji safi na salama, Jimbo la Fuoni kwa kweli lina visima vingi lakini kwa kweli wananchi wanaopata maji katika Jimbo langu mimi la Fuoni ni asilimia ndogo sana.

Tuwaombe Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Mhe Salama Aboud Talib kwa sababu ni Waziri msikivu, ukimuomba anaombeka basi angalau katika bajeti inayokuja atupatie visima viwili vya *Ras Al Khaimah* katika Jimbo langu la Fuoni vikamilike na sisi viongozi wa Jimbo mimi na Mbunge wangu Mhe. Abbas Mwinyi tuko tayari kuweza kusaidiana na *ZAWA* kuhakikisha visima hivyo vinakamilika na wananchi wetu wanapata maji.(*Makofi*)

Lakini vile vile niende kwenye ukurasa wa 22 kwenye Shirika letu hili la *ZECO* nalo tuwapongeze kwa juhudi, wanazozichukuwa tumeona juhudi wanazozifanya katika eneo la Fuoni Kitongoni wananchi kipindi kirefu hawajapa umeme, lakini sasa hivi *alhamdulillah* juhudi tumeziona. Lakini nna ombi jengine hapa wananchi wangu wa Fuoni Birikani bado tokea Mapinduzi ya Mwaka 1964 hawapajapa umeme. Tukuombe Mhe. Waziri nayo kama haiko katika *plan* kijiji cha Fuoni Birikani basi kitiwe katika mpango ili wananchi wa Fuoni Birikani nao waweze kutumia matunda haya ya Mapinduzi na kupata huduma hii ya nishati ya umeme kwa kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa ukurasa wa 28 kwenye Mamlaka ya *ZURA*. Kwa kweli, *ZURA* inafanyakazi nzuri na tuwapongeze sana kwamba wamewapa faini vile vituo ambavyo vimeficha mafuta. Hivi karibuni tunajua kwamba tumepitisha Sheria Ushindani Halali wa Biashara. Ukiangalia katika sehemu ya nne inazungumzia minendo ya biashara ambayo imekatazwa, kifungu cha 46 Mhe. Mwenyekiti, naomba nikinukuu:

"Ni marufuku kwa mtu yeyote iwe yeye mwenyewe binafsi au kupitia wakala wake au Shirika lolote kwa kushirikiana au kwa njia nyengine yoyote kupitia utaratibu wa makubalianao kuzuia bidhaa ili kuzifanya bidhaa hizo ziwe adimu".

Tumeona baadhi ya vituo mafuta wanayo lakini wameyazuia. Tuwanwapongeza sana *ZURA* kuwapiga faini na tunawataka sisi waendelee hivi hivi wale wote watakaozuaia bidhaa ya mafuta na wanayo basi wawatoze faini na wasioweza bora biashara hii waiache. Tunaomba sana wafanyabiashara wafanye biashara kwa kutumia sheria zilizopo na asiyeweza basi bora awachie biashara hiyo na awaachie wengine wafanyebiashara.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Panya Ali Abdalla nae atumie dakika tano kwa ufupi sana.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa jioni hii. Lakini pia nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe ambaye umenipa nafasi hii pia nichukuwe fursa hii kuwapongeza Mawaziri wetu wote wawili wa wizara hizi ya Mawasilinao na Ardhi.

Lakini pia nimpongeze Mwenyekiti mahiri Mwenyekiti wa Wenyeviti ambaye leo imebainika kuwa ile Hamza kuwa ni shujaa kwamba amepewa cheo chake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 7 kwenye Kamisheni wa Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua wakati wa Sherehe za Mapinduzi Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein alitoa katika hotuba yake katika Sherehe zile za Mapinduzi kwamba Kamisheni hivi karibuni itatoa hati elfu moja mia nne. Sasa mimi nilitaka kujua nipate ufafanuzi kwamba hati hizi ambazo zilikusudiwa kutolewa. Je, zilikuwa ni za utambuzi wa ardhi au ni hati za viwanja. Nilitaka kujua hili ili wananchi wapate kujua na wao kauli ile utekelezaji wake umeendaje. Mhe. Mwenyekiti, hasa niliposemwa lile neno hivi karibuni kwa hiyo Mheshimiwa kama angepata uwezo wa kutupatia kabla ya mwezi wa tisa hili jawabu ingependeza kwa hili kwa sababu imeeleza hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Rais alitoa motisha kwa vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* kwa kuwapatia viwanja. Pia nilitaka kujua

utekelezaji wake umefikia wapi isije ikaleta changamoto kwa vijana wetu. Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa namba 5 Idara ya Utunzaji wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nichukuwe fursa ya kuipongeza sana Idara yetu hii kwa kazi yetu kubwa na nzuri ambazo inazifanya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya *UUB* inakuwa inashughulika sana na matengezo ya barabara na saa nyengine wanapwewa maagizo na Mhe. Rais kama mahala fulani katengenezeni. Lakini uchakavu wa vyombo vyao mashine hizi na vifaa mbali mbali unarejesha nyuma ule utendaji wao wa kazi. Naiomba sana serikali iweze kuwatengea fedha ili waweze kupata mashine hizi na vifaa vyao mbali mbali, ili waendelee kututengenezea barabara zetu. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze katika kipindi hichi ambacho wanashughulikia katika matengenezo ya barabara yetu ya Bububu ambayo iliharibiwa sana na maji.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali katika matengenezo yale ya barabara kwa siku hizi maana siku hizi nchi yetu imeendelea bwana Zanzibar wanaosema hakuna maendeleo wanasema tu. Lakini Zanzibar tumendelea sasa hivi tuna magari mengi sana yaani ukisimama njiani dakika tano tu basi ujue umeshatayarisha foleni kubwa sana. Mimi naipongeza serikali kwa juhudi inayochukuwa lakini ningeomba matengenezo haya basi wangeyafanya kama nyakati za usiku ili kuepusha ule msongamano mkubwa kabisa unasongamana wakati wa mchana na tunaelewa kila mmoja wakati ule ana mahitaji yake anakimbilia, kila mmoja ana umuhimu wake wa kukimbilia mahala. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba na nasema hivyo kwa sababu juzi moja ilitaka kutupata mkasa tulikuwa na mjamzito tunampelekea hospitali nusura ajifungulie barabarani. Kwa hivyo naomba sana serikali wakati wa matengenezo haya basi yangefanywa usiku.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee katika Idara hii ya Matengenezo ya Barabara *UUB*. Pia wameeleza katika changamoto yao hawana wataalamu. Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari kama hatuna wataalamu wa ndani ya nchi yetu wazalendo ni hatari, kwa sababu sasa hivi tunaingia katika mikataba mikubwa mikubwa ya kujenga barabara zetu. Kwa hiyo, wataalamu hawa ni muhimu kwa sababu wao ndio watakaoweza kufatilia ile miradi yetu na kukosoa ni mahala gani pamejengwa vibaya pafumuliwe ili tupate barabara zenye kiwango, tukikosa wataalamu kama hawa tutaendelea kujengewa barabara ambazo hazina viwango. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali izingatie kuhusu hili ili tuweze kupatiwa wataalamu hawa ili waweze kufatilia miradi yetu pale tunapo.....

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa muda wako umemaliza.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Aka ngoja nimalizie!

Mhe. Mwenyekiti, niende katika hoja ambayo wameisema mwenzangu wengi nayo ni meli ya MV. Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, sisi wakati wa ukataji wa bajeti ile sisi ndio tumepitisha hapa. Kwa hivyo, wananchi wetu waliteseka sana kwa kuona mahitaji waliyakosa kupitia upungufu wa bajeti ya katika wizara. Leo tunasema hapanunuliwi kwanza wala hapauzwi meli, tunataka paundwe Kamati ili tuweze kujua ubadhirifu, lazima hapa iundwe Tume ikachunguze tuweze kujua watu ambao wanarejesha nyuma juhudi za serikali.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana na mimi kwa kuwa unasema muda wangu umekwisha nasema, nawapongeza sana. Lakini pia naomba hii Wizara ya Ardhi ambapo ndiko tunapopata maji Mhe. Mwenyekiti wanaongeze juhudi wanajitahidi lakini juhudi

iongezeke kwa sababu maji ni kitu muhimu kwa kila mtu kwa kila kiumbe.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

## MICHANGO YA MAANDISHI

**Mhe. Shehe Hamad Mattar:** Mhe. Spika nachukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uhai na afya. Nakubali na kuunga mkono Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa asilimia mia.

Pia mimi kwa vile nimeikubali na kwasababu kamati imefanya kazi kubwa kupita na kutafuta kila changamoto na mafanikio katika wizara hizo mbili, sasa nitakazia kwa baadhi ya mambo yaliyotajwa ndani ya ripoti.

Kama:

- Naiomba Serikali yetu ifanye juhudi za makusudi kwa kuwapatia Wizara husika kuwa na Wataalamu wa Usimamizi wa Ardhi, Utathmini Ardhi, Mipango Mji, Upimaji na Uchoraji pamoja na ukosefu wa vifaa vya kisasa, ama kwa kuhamisha kutoka taasisi nyengine au kwa kuajiri watu wenye sifa hizo.

- Aidha, Serikali isomeshe vijana wetu katika fani hizo ambazo kwa sasa hatunao au wachache.

- Aidha, suala la eka tatu kusimamiwe na mamlaka mbili na mimi sikubaliani nalo bali iwekwe mamlaka moja tu ambayo ndiyo yenye haki ya kufanya hivyo.

- Pia ni jambo la aibu kwa Afisa Mtambuzi wa Ardhi alieteuliwa na Waziri tena kwa mujibu wa sheria ikawa hadi Kamati inafika hajalipwa mafao yake, hivyo ni vyema jambo hili likamalizika vizuri.

- Vile vile naiomba Serikali kupitia chombo chenye mamlaka kuchukua hatua ya kuhakikisha deni linalipwa kwa haraka na ikibidi kulipa na faini.

- Kwa sababu Kampuni ya Zantel na nyenginezo kama huna malipo au salio kuna huduma na hata ukilipa kwa jeuri zao wanasema wanakupa muda wa bure japo wanasema wanakupa muda wa bure jambo ambalo linaudhi sana.

- Kuhusu Mahkama ya Ardhi naipongeza kwa kazi zake na kufikia kusikiliza kesi 108 na kuzitolea maamuzi.

- Lakini maamuzi yao yanabaki kwenye makaratasi (kwa baadhi) kwa kutopewa hati au kukabidhiwa mali yake (ardhi) ambayo imekuwa ikidaiwa kwa muhusika alieshinda kesi.

- Vile vile Mwenyekiti wa Mahkama ya Ardhi alieteuliwa na Mhe. Rais wetu naomba apatiwe maslahi yake haraka iwezekanavyo.

- Kwani Mhe. Rais alisema unapompa mtu madaraka au dhamana apewe na stahiki zake.

- Hivyo sio vyema kuuza kauli ya Mhe. Rais wetu.
- Suala la Mipango Mjini na Vijijini lifanyiwe kazi lisibaki kuwa ni nyimbo ya kila siku kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo.

- Kuhusu madeni ya umeme yote yalipwe ya Taasisi za Serikali ili Shirika liweze kutimiza majukumu yake.

**Mhe. Ussi Yahya Haji:** Kwanza napenda kuipongeza Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Pili ni kweli usiofichika kuwapongeza Mawaziri wote wawili wa Wizara hizo pamoja na watendaji wao katika wizara hizo.

Naelewa fika kuwa mawaziri hao pamona na watendaji wao wako mbioni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015-2020.

**KAMISHENI YA ARDHI**
Kuna haja ya makusudi kwa wizara hii kuendelea kutoa elimi juu ya matumizi ya ardhi, hasaz kwaz vile idadi ya watu inazidi kuongezeka.

**MAMLAKA YA ARDHI**
Kuiomba Serikali kuipatia mahkama hiyo jengo lake la kudumu kwa taasisi hiyo ni muhimu sana katika jamii yetu.

**SHIRIKA LA UMEME**
Natoa pongezi za dhati katika Shirika hili kwa utendaji wake wa kazi mfano mzuri ni kuwapatia umeme wananchi wa kijiji cha Mlilile na Mbuyumaji, Matemwe katika Jimbo la Mwajuni, mara tu baada ya Ziara ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkr. Ali Mohamed Shein aliyoifanya tarehe 13 Agosti, 2017.

**MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)**
Mamlaka hii nayo inafanya kazi zake kwa juhudi na maarifa. Wizara iendelee kutoa taaluma kwa wananchi, ambao wanaharibu miundo mbinu ya maji Unguja na Pemba, pamoja na kupewa taaluma wananchi hao.

Naipongeza Mamlaka ya Maji kwa utekelezaji kwa vitendo Amri ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliyo ifanya Jimbo la Mkwajuni katika vijiji vyza Mbuyumaji na Mlilile huko Matemwe. Ziara hiyo ilikuwa tarehe 13 Agosti, 2017 umeme huo leo unawaka. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono taarifa hii. Ahsante, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Juma Ali Khatib:** Mhe. Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Ardhi sehemu ya ZAWA kuwa tuna tatizo kubwa kwenye visima, pumpu zinaharibika kila mara hii ni kutokana wahusika wananunuwa pump ambazo hazina kiwango mbovu sasa wizara waagize pump kutoka kiwandani moja kwa moja ili tupate pump zenye uboraz zenye kukidhi shida za wananchi, hii itasaidia sana upungufu wa maji. Naunga mkono ripoti ya kamati yako.

**Mhe. Mjumbe fulani:**

a) Meli isinunuiliwe na pesa zipelekwe katika Miradi ya Maendeleo
b) Kilimo Pemba iwe sehemu ya kulisha Zanzibar hasa mboga mboga.

**Mhe. Zaina Abdalla Salum:** Mhe. Mwenyekiti, nami naomba niwasilishe mchango wangu wa maandishi kwa Ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Nianze kwa kuchangia changamoto ya ukosefu wa wafanyakazi, upungufu wa watendaj. Hii imekuwa ni changamoto sugu au ni kichaka sasa cha kujifichia watendaji wakuu walio ndani ya mawizara kutoweza kutekeleza majukumu yao kwa kisingizio hiki. Niombe sana serikali itatuwe changamoto hii katika mawizara ili tuweze kufanikisha vizuri katika kuimarisha ukuzaji wa uchumi na uimarishaji wa mazingira kwa jumla.

**Umwagaji wa Maji Taka:**

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli umwagaji maji taka katika eneo la Maruhubi ni tatizo kubwa, kwani eneo hilo lina ofisi nyingi ikiwemo pamoja na viwanda, inakera sana na hasa ukizingatia kuwa viwanda vile vyengine ni vya kutengenezea vinywaji. Hivyo, niiombe serikali iangalie eneo jengine ambalo litaweza kufanyiwa kazi hiyo. Naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, nitawapa nafasi mawaziri. Kwanza tutaanza na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais baadae watafuatia waziri wengine kwa dakika tano tano. Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha, niishukuru kamati hii kwa taarifa yake nzuri ya kina yenye maelezo ya kutosha. Vile vile niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, ambao wamechangia hoja hii kwa upana sana. Nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali imesikia maelezo ya wajumbe na naamini kabisa kwamba mawaziri wa sekta watakapopata nafasi japo kwa ufupi watatoa maelezo, lakini maelezo ya kina kutokana na kanuni zetu yatapatikana katika mwezi wa tisa kama kanuni zinavyotaka. Naamini maelezo ya kutosha yapo na tutaeleza.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi ya Waheshimiwa Wajumbe, waliyosema tunaelewa dhamira yake ni kutengeneza ili kuleta manufaa kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, liko jambo lilijitokeza leo katika hoja wakati wa asubuhi, linalohusiana kwa njia moja au nyengine limewagusa viongozi wetu wastaafu.

Mhe. Mwenyekiti, viongozi wetu wastaafu wamefanyakazi kubwa ya kujenga nchi hii na unapofikia muda wa kustaafu wanahitaji kupumzika kwa furaha na kwa amani. Kwa hivyo, sio jambo zuri sana tunapowatia midomoni kwa kuwazungumza kutokana na kazi kubwa waliokwishakuifanya tungeliwaacha wapumzike, ili waendelee kutushauri katika mambo ya msingi pale tunapotaka ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu wa serikali kwa mujibu wa sheria kutoa huduma mbali mbali kwa viongozi wetu wastaafu, kuna stahili zao zimewekwa zinafanywa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Wanafanyiwa hivyo kutokana na kazi kubwa wanayoifanya ya kujenga nchi yetu. Kwa hivyo, serikali siku zote katika bajeti zake imekuwa ikipanga kwa ukamilifu ili kuhakikisha kwamba stahili za viongozi wetu hususan Marais wetu wastaafu, zinapewa kipaumbele ili viongozi wetu wapate utulivu. Pale ambapo panajitokeza jambo lolote linalohusu viongozi wetu, wajibu wa kurekebisha jambo hilo lipo katika mikono ya serikali. Ndio maana Mhe. Mwenyekiti, tukaweka katika Katiba mgawanyo wa madaraka. Serikali ina majukumu yake, Baraza lina majukumu yake na muhimili wa Mahakama una majukumu yake.

Kwa hivyo, sio vizuri kuingilia utendaji wa ndani wa shughuli za serikali kwa Wajumbe. Kama kuna jambo lolote ambalo serikali itahitaji kwa Wajumbe wake, basi inazungumza nao kwa utaratibu uliowekwa. Kwa hivyo nipende kutoa wito kwa viongozi wetu hususan Waheshimiwa Wajumbe kutumia busara sana katika utekelezaji wa shughuli zetu na hususan kwa vile wananchi wetu katika majimbo wanatuhitaji sana, yapo mambo mengi ambayo wananchi kwenye majimbo yetu wanahitaji tuwatekelezee. Serikali ina mipango yake ya kibajeti ya kutekeleza yake.

Kwa hivyo, hili jambo ambalo lilitokea na likazungumzwa kinyume kabisa na ambavyo majibu ya Katibu wetu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi ni kinyume kabisa na maelezo yaliyotoka hapa. Ukitizama barua ambayo Katibu Mkuu Kiongozi aliijibu kwa Mhe. Raza, ilikuwa barua iliyoandikwa kwa nidhamu kabisa na ilikuwa haina haja ya kuvutia malumbano ya aina yoyote katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ningependa niisome ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na wananchi waelewe kilichojibiwa, kwa misingi ya kutunza nidhamu, kwa misingi ya kutunza heshima na kwa msingi ya kuutambua wajibu wa viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, barua ilikuwa inasema hivi ambayo ilijibiwa tarehe 13 Disemba.

> "Kuhusu Viongozi Wastaafu kuingizwa katika orodha ya wadaiwa sugu wa umeme na Shirika la Umeme *ZECO*.
>
> Kwa heshima rejea barua yako namba PS/786/110 ya tarehe 8 Disemba, 2017 kuhusiana na maneno hayo hapo juu.
>
> Naomba ufahamu kwamba Viongozi Wakuu Wastaafu wanazo stahili zao kwa mujibu wa sheria zinazolipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwa ni pamoja na kulipiwa umeme.
>
> Kwa kuelewa wajibu wake huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwalipia umeme viongozi waliotajwa katika barua yako, kila mwezi kadiri ya *ZECO* inavyowasilisha *bill* zao Wizara ya Fedha na Mipango. Kama ni deni, basi lilikuwa ni lile ambalo

*ZECO* ilikuwa hawajaliwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango na kwa mujibu wa tarehe ambayo taasisi zinazohusika zilikubaliana ilikuwa bado haijafika. Kwa hivyo ni vyema ukapata maelezo zaidi huko *ZECO* kama hicho kinachoelezwa ni sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kadri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyohusika, hakuna deni lakuitwa sugu na hata kama ingekuwa hivyo, haikupaswa deni hilo kuhusishwa na viongozi hao, kwa sababu wajibu wa kulipa upo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na imekuwa ikiutimiza wajibu huo kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi hapakuwa na sababu ya wewe kulipa deni hilo kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikushindwa na imekuwa ikilipa *bill* za umeme za viongozi hao kila mwezi kama kawaida". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sio kulipa deni la umeme tu, viongozi hao wana stahili nyingi zinazofanywa na serikali, ikiwemo huduma za za afya na mambo mengine. Kwa hivyo, sio vizuri hata kidogo leo kujadili hapa kuzungumza mambo haya, ambapo viongozi wetu wamefanyakazi kubwa sana. Wanapohasikia hapa ni kama kuwadhalilisha kwa upande mwengine na kuyasema maneno haya, sio tu unawadhalilisha wao lakini pia unaidhalilisha serikali ambayo inafanyakazi kubwa ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niseme wazi kwamba sisi viongozi tuwe na busara sana katika maelezo yetu tunayotoa katika chombo hiki kikubwa. Serikali yetu ni sikivu, inaendelea kusikiliza mengi na inaendelea kukubali mashauri mengi, lakini jambo ambalo litakuwa likiwadhalilisha viongozi wetu wastaafu, basi serikali haitoweza

kuvumilia tena. Leo tunaomba tuufunge mjadala huu kuhusiana na viongozi wetu hao ili viongozi wetu hao waendelee kuishi kwa amani na furaha baada ya kazi kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mkopo wa shilingi milioni 200 ambao Mhe. Raza alimuandikia Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Niseme tu kwamba serikali tuna bajeti zetu, tumejipanga kulishughulikia tatizo la maji nchini kwa ukamilifu sana, ni fedha nyingi sana zinazotumika na zitakazotumika kuondoa tatizo la maji. Shilingi milioni 200 ni sawa sawa na kilo ya sukari katika maji chumvi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuna mipango ya mamilioni ya dola katika kushughulikia tatizo la maji nchini na mipango hiyo imeanza rasmi na itaendelea kufanyiwa kazi na tutahakikisha katika kipindi chetu hiki kabla ya mwaka 2020 tatizo la maji nchini litakuwa ni historia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kama wanazo fedha zao basi wangezitumia zaidi katika kutatua matatizo yaliomo kwenye majimbo yao. Wajibu wa serikali utabakia kuwa wajibu wa serikali kutekeleza majukumu yake kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, sasa namwita Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili na yeye aweze kutoa machache. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kwanza nianze kuishukuru sana Kamati ya Ardhi na Mawasiliano

kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kutayarisha ripoti hii. Shukrani za pekee ziende kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Wajumbe wake wote kwa sababu wamefanyakazi kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kazi kubwa ya kuichambua ripoti hii na kuona umuhimu wa sekta zote zilizokuwemo ndani ya wizara hii na kuweza kuzichangia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamesema mengi na tumeyasikia kama wizara, tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Wakati wa majumuisho ya kuleta taarifa ya ripoti hii ikifika basi haya yote yaliyojadiliwa tutayachambua kwa kina na tutayafanyia utekelezaji wake. Utekelezaji wake na majibu yake yote yatakuja wakati huo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuru na wewe binafsi lakini niishukuru na kamati, haya yote sisi tumeyapokea. Vile vile naomba nimshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye amekuwa akituongoza kila siku na akitupa miongozo mbali mbali, ili kuhakikisha kwamba wizara hii inakwenda kwa mafanikio makubwa na kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, amekuwa karibu sana wakati wote na kuhakikisha kwamba matatizo ya wananchi tunayatatua. Kwa hivyo naomba niwashukuru kwa ujumla wake. Lakini nitakuwa mkosefu wa fadhila sana leo hii nimesimama hapa, kama sitowashukuru sana watendaji wangu na viongozi ndani ya wizara. Niseme kwamba kufanikiwa kwa Kamati hii basi wizara yangu kwa asilimia kubwa watendaji wote wafanyakazi wameshiriki kwa njia moja au nyengine, ili kuhakikisha kwamba

wanafanikisha. Pia wananipa mashirikiano ya kutosha nawashukuru sana na mwezi wa tisa *Inshaallah* tutaleta ripoti kwa mafanikio makubwa.

Naomba niwashukuru. Naomba kuunga mkono hoja ya kamati. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ya muda wetu hautatosha mwenyekiti kuweza kumalizia, nitamuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aongeze muda, atenguwe kanuni ya muda ili tuweze kumaliza shughuli yetu.

*(Hapa Wajumbe walipiga makofi kwa kutoridhika na maelezo ya Mhe Mwenyekiti wa Baraza)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwenyekiti, anahitaji muda. Naomba musikilize, Mhe. Mwenyekiti, anahitaji muda na yeye amalizie. Kuna Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji hatujampa muda na yeye anaweza kutoa lolote lile, ni lazima tumpe na yeye haki kama ni waziri husika. Mhe. Waziri karibu.

## KUONGEZA MUDA WA BARAZA

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda uliombele yetu hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu, kwa hivyo naomba tuweke Knuni ya muda kando ili tutowe nafasi kwa viongozi waliobaki pamoja na mwenyekiti kufanya majumuisho ya taarifa yake. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa wale wanaokubaliana na hoja. Wale wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, karibu.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru sana kwa kunipatia muda na mimi kidogo nizungumzie hii ripoti nzuri sana ambayo ilitengenezwa na Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ambaye namfahamu sana, tunafanya naye kazi pamoja, namshukuru Makamu Mwenyekiti na pia Wajumbe wote wa hii kamati, huwa tunafanyakazi sana pamoja ili kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinafanyika vile ambavyo wananchi wanatutegemea kuwahudumia.

Pia ningependa na mimi nitowe shukrani zangu kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa hii leo kutuongoza vizuri sana na pia niwashukuru Wajumbe wote waliotoa hoja mbali mbali. Wajumbe wengi wamezungumzia mambo ambayo tunayajua na tunayafanyia kazi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumshukuru Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake imara kabisa ambao anatusaidia katika kutatua matatizo mengi ambayo tunayapata kwenye wizara hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nitasema tu mambo mawili au matatu ya kwamba hii Wizara yetu ya Ujenzi,

Mawasiliano na Usafirishaji ni wizara ambayo inaendeshwa kitaalamu na kuna wataalamu wengi wanashughulikia matatizo haya. Imani yangu ni kwamba ingekuwa sio wale wataalamu wetu basi haya matatizo yangekuwa zaidi ya mara milioni. Kwa hivyo nawashukuru sana wataalamu wetu na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi yao wanayoifanya usiku na mchana, ili kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinafanikiwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika nia ya kuwatendea haki wataalamu wetu hawa, basi nisingetaka kujibu maswali haya ya kitaalamu. Maswali mengi yaliyoulizwa Mhe. Mwenyekiti, ni ya kitaalamu na mimi simtaalamu wa mambo haya, mimi ni mwanasiasa. Kwa hivyo katika kuwatendea haki nilikuwa naomba tuwape muda kutokana na Kanuni zinavyosema, wataleta majibu ya kitaalamu utakapofika wakati wake mwezi wa tisa na tuwe na subra tusubiri mpaka wakati huo.

Isipokuwa tu kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kusema maneno mawili au matatu kuhusu suala hili ambalo lilizungumzwa sana hapa kuhusu meli yetu ya MV Mapinduzi II. Nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kutuletea ripoti ile inaitwa Tamko Rasmi la Serikali kuhusu suala hilo. *(Makofi)*

Napenda kukuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Baraza lako tukufu kwamba Mhe. Waziri atakuja hapa na tamko rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuhusu hali ya hii meli ya Mapinduzi II *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *Terminal II* ya *Airport* inajengwa na kazi za kujenga zimeshaanza. Vile vile kuhusu suala la *Kengeja Road* njia ile ya Pemba inajengwa wala msiwe na wasi wasi tutaimaliza. Kuhusu matatizo ya utengenezaji wa njia, ujenzi na utunzaji wa barabara. Tunakiri kwamba *UUB* kitengo hicho

ambacho kinashughulikia masuala haya kidogo wana matatizo ya vifaa, lakini wataalamu tunao, vifaa tumeshaagiza na imani yetu ni kwamba tutaendelea kufanya hizi kazi za kutunza na kujenga barabara kama kawaida.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoahidi sina haja ya kujibu maswali, nimesimama hapa kutoa shukrani sana kwako wewe na kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutusaidia mawazo mengi sana na ninawahakikishia kwamba mawazo mengi tuliopewa na ushauri mwingi tuliopewa tutaufanyia kazi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*...

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Waziri sasa ninamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ili aweze kuja kumalizia.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kunipa nafasi hii kwa haraka haraka naomba niokoe muda nawapongeza wote wote ambao waliochangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweka *Hansard* sawa kama utaniruhusu niombe niwataje tu Waheshimiwa Wajumbe ambao waliochangia au kama utaniruhusi nisiwataje nitoe maelezo tu machache ili baadae waingie kwenye *Hansard*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Endelea kuwataja.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Mwenyekiti naomba niwataje wajumbe waliochangia ripoti ya kamati yangu kama ifutavyo.

1. Mhe. Mohammediraza Hasanali Mohammedali

2. Mhe. Ali Suleiman Ali *(Shihata)*
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
4. Mhe. Simai Mohamed Said *(Mpakabasi)*
5. Mhe. Bahati Khamis Kombo
6. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
7. Mhe. Mussa Foum Mussa
8. Mhe. Machano Othman Said
9. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
10. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
11. Mhe. Suleiman Makame Ali
12. Mhe. Asha Abdalla Mussa
13. Mhe. Shaib Said Ali
14. Mhe. Omar Seif Abeid
15. Mhe. Ali Khamis Bakari *(Doholo)*
16. Mhe. Said Omar Said
17. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu *(Bhaa)*
18. Mhe. Mussa Ali Mussa *(Mr. X)*
19. Mhe. Ame Haji Ali
20. Mhe. Yussuf Hassan Iddi *(Masharubu)*
21. Mhe. Panya Ali Abdalla
22. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais *(Mild field)*
23. Mhe. Waziri wa Ardhi Maji, Nishati, na Mazingira.
24. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna Wajumbe wengine ambao kutokana na muda walichangia kwa maandishi naomba nimtambue.

1. Mhe. Ali Juma Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
2. Mhe. Ussi Yahya Haji
3. Mhe. Hamad Shehe Mattar
4. Mhe. Zainab Abdalla Salum
5. Mhe. Shamata Shaame Khamis

6. Mhe. Miraji Khamis Mussa
7. Mhe. Rashid Makame Shamsi
8. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
9. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma
11. Mhe. Hassan Hamis Khafidh.

Mhe.Mwenyekiti, kwa kweli Wajumbe wamechangia mambo mengi na kwa sababu kama walivyosema Waheshimiwa Mawaziri wanakwenda kukaa masuala ni kweli ya kitaalam, kwa sababu Kamati ilifanya kazi ya kitaalamu. Kwa hivyo tunaamini wataweza kuleta majibu wakati ukifika. Isipokuwa tu Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba masuala machache kidogo niwaombe Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo ambayo jawabu yake tunajua itakuja mwezi wa Septemba lakini utekelezaji wake sasa tunaiomba kamati kwamba haya yatekelezwe kabla ya bajeti inayokuja.

Nitaanza na Mhe. Waziri wa Ardhi kuna stahiki za Hakimu wa Mahakama ya Ardhi lakini vile vile kuna stahiki za Mrajis wa Utambuzi wa Ardhi. Hawa ni watu ambao kwa mujibu wa sheria wamepata nafasi ya uteuzi, lakini zile haki zao stahiki zao za uteuzi bado hawajazipata. Sasa hili si la kusubiri mpaka mwezi wa Septemba huo, hili naomba Mhe. Waziri alifanyie kazi kwa haraka ili na wenzetu wale waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Lakini jengine ambalo nilikuwa naomba lisifike mwezi wa tisa katika utekelezaji wake kuhusu suala tulilolitaja mkataba wa *ZMA* kule Dubai. Naamini Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshatikisha kichwa anajua nini kamati ambavyo ilivyokusudi, kama

alivyosema Mhe. Waziri kwamba haya ni masuala ya kitaalamu yanahitaji busara na umakini wa hali ya juu.(*Makofi*).

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kwamba suala la upungufu wa mafuta nafikiri Mhe. Waziri amelifanyia kazi tunakushukuru sana. Lakini tunaishukuru zaidi Kampuni ya *ZP* kwa sababu katika kipindi ambacho meli za Bakharesa kituo chake kilipokuwa kimekosa mafuta, walijitahidi sana kuweza kugawanya mafuta kwa vituo vyengine ili hali ya mafuta iweze kupatikana, na kama alivyosema Mhe. Waziri tunategemea pengine meli ya Bakharesa pengine kesho itaingia mafuta yatakuwepo katika vituo kama kawaida. Kwa hivyo tunaendelea kuwapongeza waingizaji wa mafuta ili kuweza kuondoa tatizo katika nchi yetu.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mawili ya mwisho ya kumalizia. Kwanza suala la mirathi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shaibu alizungumza kwamba Kamati imetaja suala la mirathi na masuala ya mirathi yapo katika Wizara inayoshughulikia masuala ya Katiba, lakini hili imebidi tulieleze ili tuweze kulifahamu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana Mhe. Waziri wa Ardhi naomba utuandalie semina na Mrajis wa Usajili wa Ardhi pamoja na Uhakiki wa maeneo yetu. Sasa hivi bila ya kujijua wengi sana tunakula mali za mayatima. Mhe. Mwenyekiti, hili nalisisitiza sana sisi tumepata taaluma ndogo lakini kwa kweli machozi yalitutoka, wengi wetu tunakaa katika nyumba za urithi, nyumba ambazo walituachia wazee wetu lakini nyumba hizi baada ya kufariki wazee wetu hatukwenda kuripoti zikagawiwa mirathi, ina maana pale tunakula mali za mayatima, tunakaa kwenye mali za urithi.(*Makofi*).

Sasa hili ukiangalia familia zetu nyingi Mhe. Mwenyekiti, hatuzijui tunaweza tukajikuta umefanya mambo mengi ya thawabu siku ya siku ukiletewa orodha ya mali uliyoikalia kwa

maisha yako yote nyumba ya urithi Mhe. Mwenyekiti ni moto mkubwa sana. Kwa hivyo hili nimekuwa naomba dozi hii kamati tuliipata kwa kweli sote tulisikitika, kwa sababu tukiangalia familia karibu zaidi ya hamsini, kuna mali za urithi za wazee wao baada ya wazee wao kufariki hazikurudi kugawanywa kila mmoja akapata haki yake. Matokezeo yake mtu anakaa yeye pengine anamuachia ndugu yake na nani kumbe tunakula mali za mayatima.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hili nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati aandae siku waje ili watu wake watupe hiyo dozi ili tuondokane na hiyo.

Sasa la mwisho kabisa mimi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kadhi iliyojitokeza kwa kweli sisi kama Kamati tunasikitika sana kwa sababu aliyetoa hoja hii ni Mjumbe wangu wa kamati. Kwa bahati nzuri au kwa bahati mbaya ninayo barua mjumbe wangu huyu aliniaga kwamba anaumwa anakwenda kwenye matibabu na katika kipindi chote tulichoshiriki katika Kamati hakuwahi kushiriki. Kwa hivyo yale aliyoyasema sisi Kamati yametushitua kwa kweli.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hili lazima tuliweke sawa kwa sababu inawezekana yale maelezo yake wakaja wakachukuliwa hatua za kinidhamu watendaji wa Shirika la Umeme wakati hawana makosa, kamati kitu ambacho inachopelekewa sisi tumewaambia tuleteeni madeni ya umeme, madeni ya umeme ni sawa sawa kusema tuleteeni bili. Kwa hivyo ina maana kama deni la mwezi uliopita lilikwisha kuwahi kulipwa, lakini la mwezi huu bado halijalipwa, sasa lile linaingia katika deni, sio deni sugu.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwamba sasa hivi utaratibu wa madeni ya viongozi wetu wa kitaifa Serikali inashughulikia *direct*

*ZECO* wanatakiwa wapeleke *Invoice*, wapeleke bili serikali inalipa. Kwa hivyo yale sio sehemu ya madeni sugu. Sasa hili kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, lilivyojitokeza sisi Kamati halikutupa afya nzuri ni jambo ambalo kwa kweli limetusikitisha.(*Makofi*).

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, suala la *ZAWA* kupewa pesa shilingi milioni mia mbili. Mimi Mjumbe wangu huyu alinieleza kabla ya kuingia kwenye ukumbi na nikamuambia suala hilo wewe huna haja ya kutoa hizo shilingi milioni mia mbili. Sisi kama Kamati baada ya kuona tatizo kubwa la maji tulikwenda kwa Makamo wa Pili wa Rais, tukakaa naye tukamwambia *ZAWA* walihitaji shilingi bilioni nane kwa ajili ya kufunga visima vyote vya Rasi El Khaimah, sisi tukaiomba Serikali tunaziomba hizi pesa zitolewe haraka kwa sababu huo mpango wa bilioni nane ni mpango wa miaka mitatu ili kuvimaliza visima vyote. Sisi kama kamati tukaeleza kwamba Serikali tunaomba hivi visima vya Ras El Khaimah vipatiwe fedha kwa haraka viungiwe. Serikali imekubali kutoa shilingi bilioni mbili ili kuwapa *ZAWA* waweze kufanya *installation* ya visima vya maji vya Ras El Khaimah.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama Mjumbe wangu angelikuwa ameshiriki kikamilifu katika kamati, haya angaliyajua. Sasa ukifanya hesabu bilioni mbili na milioni mia mbili wapi na wapi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nikiwa kama mwenyekiti wa kamati kwa kweli sikufurahi na nimesikitishwa na wajumbe wangu wamesikitika sana. Lakini nataka kuwaambia kwamba mpaka sasa hivi sisi tuna mkataba baina ya *ZECO* na Serikali. Mkataba wetu na kamati kwamba Serikali itoe pesa kwa *ZAWA* ili waweze kufanya *installation* ya visima vya Ras El Khaimaha. Serikali wamesema tutatoa bilioni mbili lakini hatutozitoa kwa pamoja, tutatoa kwa awamu, tuone kazi inayofanywa *impact* yake halafu tutakupeni nyengine. Sasa sisi hilo ndio tunalolisubiri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo baada ya hayo najua nimechukua muda wako nimechukua muda wa Wajumbe lakini nia yangu kwa kweli ilikuwa kuweka mambo haya sawa. Kamati yangu inafanya kazi kwa mashirikiano na Wizara zote mbili na tutaendelea kufanya mashirikiano na nakuomba Mwenyekiti, mwambie Mhe. Spika anirejeshe tena kwenye kamati hii ili kuweza kusimamia yale tuliyokubaliana na Mhe. Waziri.

Ahsanteni sana.*(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekit:** Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na ripoti ya mwenyekiti, wale wanaokubaliana na ripoti ya Mwenyekiti, wanaokataa waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe kwa umakini wenu katika kujadili ripoti na kuweza kukamilisha na hatimae tukaikubali ripoti hii. Sasa naomba niahirishe Baraza hili kwa siku ya leo hadi kesho saa 3.00 asubuhi panapo majaaliwa.

*(Saa 1.50 usiku Baraza liliahirishwa mpaka*
*tarehe 22/2/2018 Saa 3.00 asubuhi)*